ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR
MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

1.Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	MBM/Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa na Rais
2.Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Dimani.
3.Mhe. Omar Yussuf Mzee	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo/ Kuteuliwa na Rais
4.Mhe. Haji Omar Kheri	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora/Jimbo la Tumbatu
5.Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa
6.Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	MBM/Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais/Kuteuliwa
7.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
8.Mhe. Rashid Seif Suleiman	MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Ziwani.
9.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge
10.Mhe. Juma Duni Haji	MBM/Waziri wa Afya/Kuteuliwa

11.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Ustawi wa Jamii na Maendeleo ya Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa
12.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo/Jimbo la Gando
13.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	MBM/Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Kuteuliwa.
14.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Jimbo la Jang'ombe
15.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni
16.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni
17.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi na Ushirika/Jimbo la Makunduchi
18. Mhe. Shawana Bukheti Hassan	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/ Jimbo la Dole
19. Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni
20.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.
21.Mhe. Othman Masoud Othman	Mwanasheria Mkuu

22.Mhe. Issa Haji Ussi	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka
23.Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake
24.Mhe. Dr. Sira Ubwa Mamboya	Naibu Waziri wa Afya/Kuteuliwa na Rais
25.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari,Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake
26.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/Jimbo la Nungwi
27.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni
28.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili/Nafasi za Wanawake
29. Mhe. Mohammed Said Mohammed	Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi/ Jimbo la Mpendae
30.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
31.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
32. Mhe. Ali Mzee Ali	Kuteuliwa
33.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
34.Mhe. Ali Abdalla Ali	Jimbo la Mfenesini
35. Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
36.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake

37. Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
38.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake
40.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake
41.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
42.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
43.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
44.Mhe. Hamad Masoud Hamad	Jimbo la Ole
45.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
46.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
47.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
48.Mhe. Hussein Ibrahim Makungu	Jimbo la Bububu
49.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
50.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni
51.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake
52.Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa	Jimbo la Kikwajuni
53.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope
54.Mhe. Mansoor Yussuf Himid	Jimbo la Kiembesamaki
55.Mhe. Marina Joel Thomas	Kateuliwa na Rais
56.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa	Jimbo la Mkwajuni
57.Mhe. Mgeni Hassan Juma	Nafasi za Wanawake
58.Mhe. Mlinde Mbarouk Juma	Jimbo la Bumbwini

59.Mhe. Mohammed Haji Khalid Jimbo la Mtambile

60.Mhe. Mohammed Mbwana Hamad Jimbo la Chambani

61.Mhe. Mussa Ali Hassan Jimbo la Koani

62.Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali Jimbo la Uzini

63.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa Nafasi za Wanawake

64.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi Nafasi za Wanawake

65.Mhe. Nassor Salim Ali Jimbo la Rahaleo

66.Mhe. Omar Ali Shehe Jimbo la Chake-Chake

67.Mhe. Panya Ali Abdalla Nafasi za Wanawake

68.Mhe. Raya Suleiman Hamad Nafasi za Wanawake

69.Mhe. Rufai Said Rufai Jimbo la Tumbe

70.Mhe. Saleh Nassor Juma Jimbo la Wawi

71.Mhe. Salim Abdalla Hamad Jimbo la Mtambwe

72.Mhe. Salma Mohammed Ali Nafasi za Wanawake

73.Mhe. Salma Mussa Bilali Nafasi za Wanawake

74.Mhe. Salmin Awadh Salmin Jimbo la Magomeni

75.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman Nafasi za Wanawake

76.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha Jimbo la Mwanakwerekwe
77.Mhe. Subeit Khamis Faki Jimbo la Micheweni
78.Mhe. Suleiman Hemed Khamis Jimbo la Konde
79.Mhe. Ussi Jecha Simai Jimbo la Chaani
80.Mhe. Viwe Khamis Abdalla Nafasi za Wanawake
81.Mhe. Wanu Hafidh Ameir Nafasi za Wanawake

Ndugu Yahya Khamis Hamad Katibu wa Baraza la Wawakilishi

Kikao cha Kumi na Tatu – Tarehe 2 Julai, 2013

(Kikao kilianza saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Mwenyekiti (Mahmoud Muhammed Mussa) alisoma dua

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 116

Tunzo ya Nishani kwa Maafisa wa Vikosi vya Ulinzi na Usalama

Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa (Kny. Mhe. Mohammed Haji Khalid) - Aliuliza:-

Kwenye kuadhimisha miaka 49 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar, Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliwatunuku nishani zao watumishi waliotukuka, utumishi wa muda mrefu na ukakamavu kwa maafisa 30 wa Vikosi vya Ulinzi na Usalama.

(a) Je, ni Maafisa wangapi Wazanzibari waliotunukiwa nishani hizo.

(b) Ni vigezo gani vilivyotumika kuwapata watunukiwa hao.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais - Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako napenda nimjibu Mhe. Mwakilishi swali lake nambari 116 lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, ni kawaida ya Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwatunuku nishani za utumishi uliotukuka, utumishi wa muda mrefu na ukakamavu kwa Maafisa wa Vikosi vua Ulinzi na Usalama wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

a) Mhe. Mwenyekiti, katika sherehe za kuadhimisha miaka 49 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzíbar, Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliwatunuku nishani hizo maafisa 26 kutoka Zanzíbar.

b) Aidha, Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anatoa nishani hizo kutokana na madaraka na mamlaka aliyonayo kisheria.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru kwa kupata nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Mhe. Mwenyekiti, swali mama linasema waliotunukiwa nishani hii ya utumishi uliotukuka pia ni pamoja na utumishi wa muda mrefu na ukakamavu wa maafisa 30 lakini yeyé kasema ni 26.

a) Kama lilivyoulizwa ambapo sikupata jibu ni maafisa wangapi Wazanzibari waliotunukiwa nishani hiyo naona hakulijibu Mhe. Waziri.

b) Na langu mimi la pili ni kuwa huu muda mrefu ni muda wa miaka mingapi, ina maana hao waliopewa nishani wote waliingia kwa mwaka mmoja na wakatoka kwa mwaka mmoja na wakapata nishani ya aina hiyo, kuwa walianza pamoja au ni muda tofauti mpaka miaka mingapi.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, tatizo letu ni lile lile Waheshimiwa hawakubali kusema kwenye spika, usiposema kwenye spika mimi sisikii nitakuwa namuuliza nikimuuliza tukirudiana. Yeyé anajua utaratibu ni kusema kwenye spika, akisema kwenye spika mimi nitamsikia hivi itakuwa tatizo naomba arudie.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Mwenyekiti, ni kuwa swali la mwanzo la swali mama ni kuwa je, ni maafisa wangapi Wazanzibari katika hao waliotunukiwa walipata nishani zao? Hili halikujibiwa.

Na la pili niliuliza huu muda mrefu ni kuanzia miaka mingapi, ina maana hao waliotunukiwa wote walianza mwaka mmoja wakatimiza umri huo au ni miaka tofauti.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, sasa namshukuru kwanza kwa kuiakaribia spika na kumsikia. Mheshimiwa kama angekuwa ananisikiliza vizuri kwenye swali langu la msingi nilisema Mhe. Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliwatunuku nishani hizo maafisa 26 kutoka Zanzibar.

Kuhusu muda mrefu maana yake Mhe. Mwenyekiti, mufa mrefu ni wale watumishi waliotumikia jeshi kwa muda zaidi ya miaka mitano. Hao wanakuwa *categorize* kwamba ni muda mrefu.

Nam. 64

Ujenzi wa Uzio kwa Vyuo vya Mafunzo ya Amali Mkokotoni na Vitongoji

Mhe. Saleh Nassor Juma - Aliululiza:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa huzuni kubwa na masikitiko ya hali ya juu sana kabla ya kuuliza swali langu la msingi naomba nitoe malalamiko yangu kwa kutonipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza na ni swali ambalo linahusu mambo ya Muungano ni suala ambalo linaitakia maslahi sana Zanzibar hii ambayo tunaelekea katika Zanzibar huru yenye mamlaka kamili.

Baada ya dibaji hiyo Mhe. Mwenyekiti naomba kwa heshima kubwa na taadhima ya hali ya juu sana swali langu Nam. 64 hivi sasa lijibiwe.

Vyuo vya Mafunzo ya Amali vilivyopo Mkokotoni Unguja na Vitongoji Pemba, sio tu kuwa vinajitahidi kutoa elimu ya ufundi ambayo itawasaidia sana vijana wetu kujiajiri wenyewe na hatimae kuweza kupunguza tatizo la ajira nchini. Kwa kuwa vyuo hivi vipo makusudi kwa ajili ya ufundi, hulazimika kutafuta vifaa vya thamani kwa ajili ya kufundishia na hivyo kuhitaji usalama na ulinzi wa hali ya juu, na kwa kuwa vyuo hivi havina uzio na kuhatarisha usalama wa mali za wanafunzi kwa kiasi kikubwa.

(a) Je, ni lini serikali itajenga uzio katika vyuo hivi ili kuweka mazingira mazuri ya wanafunzi na mali za chuo.

(b) Kwa kuwa Chuo cha Mafunzo ya Amali kilichopo Vitongoji hakifundishi taaluma ya ufundi wa mashine pamoja na kwamba vijana wetu wanajitahidi sana. Je, ni lini Chuo hicho kitaanzisha mafunzo hayo

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali - Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako sasa naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake namba 64 lenye sehemu (a) na (b).

Mhe. Mwenyekiti, Mafunzo ya Amali yanayotolewa katika vyuo vyetu vya Mkokotoni na Vitongoji, vina madhumuni ya kuwapatia vijana ujuzi utakaowawezesha kujiajiri na kuajiriwa na hatimae kuweza kupunguza tatizo la ukosefu wa ajira miongoni mwa vijana. Pia ni kweli kuwa vituo hivyo havina uzio jambo ambalo linaweza kuhatarisha usalama wa mali za vyuo na wanafunzi.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi kama hivi ifuatavyo:-

a) Katika mwaka 2013/2014, wizara yangu inakusudia kuanza ujenzi wa uzio wa kuzunguka katika vituo hivyo. Ujenzi huo utafanywa hatua kwa hatua na kwa kuanzia katika kituo kimoja na baadae kuendelea katika kituo chengine kutegemea na uwezo wetu wa fedha.

b) Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kuwa Kituo cha Mafunzo ya Amali cha Vitongoji hakifundishi fani ya mashine (*auto mechanical*). Haikuwa lengo la wizara kuwa vituo vyote vifundishe fani za aina moja. Baadhi ya fani zinafundishwa katika kituo kimoja na nyengine katika kituo chengine. Kwa mfano, Kituo cha Mafunzo ya Amali cha Vitongoji kinafundisha fani ya umeme, fani ambayo haifundishwi katika Kituo cha Mafunzo ya Amali cha Mkokotoni ambacho nacho kinafundisha fani ya *electronic* ambayo haifundishwi katika kituo cha Vitongoji. Wizara inakusudia kujenga Kituo cha Mafunzo ya Amali katika Mkoa Kaskazini Pemba, itazingatia ushauri wa Mhe. Mwakilishi kuanzisha fani hiyo katika Kituo cha Mkoa Kaskazini, Pemba. Nakushukuru Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri sana aliyoyatoa Mhe. Naibu Waziri kwa mambo haya ya *taalim wal-maarif*, naomba kuuliza swali dogo la nyongeza kama ifuatavyo. Kwa kuwa Mhe. Waziri amesema kwamba wana lengo la kujenga uzio katika hivi vyuo hivi viwili, na hakutafafanulia ni lini na wataanza chuo kipi.

(a) Je, Mhe. Waziri anaweza akatwambia mambo yakiwa sawa ataanzia chuo kipi kujenga uzio Mkokotoni au Vitongoji.

(b) Kwa kuwa lengo na dhamira la kuwafundisha watoto hawa ni kujiajiri wenyewe na wakati mwengine kutafuta ajira kwa wale walio na fani hizo wanazosomea, na kwa kuwa kuna wanafunzi tayari wameshatoka katika vyuo hivi *intake* ya mwanzo nafikiri, lakini hadi leo hii vyeti vyao vya kumalizia mafunzo haya hawajapewa jambo ambalo halitoi ushahidi kwamba wamefaulu katika fani walizosomea na hatimaye kujiajiri au kujipatia ajira kwa wenye ajira. Je, ni lini Wizara ya Elimu itatoa vyeti kuwathibitisha kama hawa ni wahitimu katika vyuo hivyo vya mafunzo ya amali kusudi waweze kupata ajira pale wanapoomba.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, nilizungumza kwenye swali langu mama kwamba tunatarajia kujenga katika mwaka huu wa fedha, bajeti yetu ya mara hii ndio itaonesha tumetenga kiasi gani katika kuhakikisha kama tunajenga uzio katika kuta hizi. Nilizungumza pia tutatizama ni wapi tuanze kutokana na fedha zenyewe sio nyingi hazitoshelezi kujenga vyuo vyetu vyote hivi viwili. Kwa hivyo, naomba Mhe. Mwakilishi anikubalie hilo, tutatizama ni wapi tutaanza kujenga kwa kuzingatia ni wapi ambapo kuna tatizo kubwa zaidi.

Suala lake la pili ni kweli Mhe. Mwenyekiti, kama toka tuanzishe vyuo vyetu hivi vya amali mwaka huu ni mwaka wa tatu ambapo wanafunzi wamehitimu tayari na nimhakikishie Mhe. Mwakilishi kwa vile wamehitimu katika mwaka huu wamemaliza basi taratibu zinaandaliwa na wakati wowote watapewa vyeti vyao.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nashukuru na mimi kunipatia nafasi ya kuuliza swali moja dogo la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri ningependa kuuliza kwamba kwa kuwa Chuo cha Amali cha Mkokotoni wakati wa ufunguzi waliahidiwa wanafunzi kupatiwa mitaji ya kujiendeleza kujikwamua kiajira.

Je, lini serikali itaweza kuwapatia mitaji hiyo ili vijana wetu hawa waweze kupata ajira lakini pia waweze kujinasua katika umaskini.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kama alivyozungumza Mhe. Mjumbe kuwa katika ufunguzi wa chuo kile tuliahidi wanafunzi kuwapatia mikopo na mpango huo upo na tuna mfuko ambao wenzetu wa *ADB* wametupa kama mkopo kuweza kuwapa wanafunzi wetu hao. Tayari wameji-*organize* wenyewe kwa sababu sharti muunde vikundi na hivi sasa tayari maombi yao yako kwenye meza yetu.

Lakini kama nilivyoeleza kwa sababu wamemaliza mara hii mwaka huu ndio wamemaliza. Kwa hivyo, tuko katika mchakato wa kuwapatia hiyo mikopo na tayari kama ambavyo nimesema kuna mambo ambayo yako juu ya meza.

Mhe. Jaku Hashim Ismail: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, ni lini wizara anayoongoza Mhe. Naibu Waziri itakuwa *serious*. Kuna waziri mmoja hapa anasema siku zote huyo *you* are *serious*? Maeneo hayo kuvamiwa na watu kujenga ni lini watapata hati miliki ikiwemo Vitongoji na Mkokotoni.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, sidhani kama suala mama kama lilikuwa linazungumza *issue* ya hati miliki, ninalokumbuka mimi ilikuwa ni kuhusu habari ya uzio na nilizungumza kama

tutajenga. Lakini kama unaniruhusu nimjibu Mhe. Mjumbe basi tuko katika mpango wa kutafuta hati miliki katika skuli zetu zote kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi, Mkaazi, Maji na Nishati. Nakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti.

Nam. 112

Athari za Mifuko ya Plastiki katika Mazingira

Mhe. Mohammed Haji Khalid - Aliuliza:-

Seikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imechukua juhudi mbali mbali katika kukabiliana na tatizo la uchafuzi wa mazingira, miongoni mwa juhudi hizo ni kupiga marufuku utumiaji wa mifuko ya plastiki na kuuwa kunguru.

(a) Je, vifuko vya plastiki vinavyotumika kutia *juice* havina athari yoyote na mazingira

(b) Katika zoezi la kuuwa kunguru lengo ni kuuwa wangapi na wangapi wameshauliwa mpaka sasa.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais - Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake namba 112 lenye sehemu (a) na (b) ambayo kila sehemu inajitegemea si maswali yanayohusiana kama ifuatavyo:

a) Vifuko vya plastiki vinavyotumika kutia *juice* vina athari kwa mazingira sawa na mifuko ya *plastic,* isipokuwa ukubwa wa athari utapungua katika kifuko kidogo kimoja ukilinganisha na mfuko mkubwa mmoja.

b) Kutokana na utafiti uliofanywa mwaka 2009 na Wizara ya Kilimo na Maliasili kupitia Idara ya Misitu na Maliasili zisizorejesheka kwa ufadhili wa mradi wa *MACEMP*. Imekisiwa kuwa Zanzibar ina jumla ya kunguru weusi 1,189,262; kati ya hao 1,077,640 wapo Unguja na 111,622 wako Pemba. Hivyo katika zoezi la kuuwa kunguru, lengo ni kuwauwa kunguru wote weusi waliopo Zanzibar. Hadi kufikia mwezi wa Aprili 2013, jumla ya kunguru weusi 638,864 wameuliwa kama ifuatavyo:-

i) Kiasi cha kunguru 500,000 waliuliwa na Idara ya Misitu na Maliasili zisizorejesheka katika kipindi cha mwaka 2009 hadi 2011 kwa ufadhili wa mradi wa *MACEMP*.

ii) Kiasi cha kunguru weusi 138,864 wameuliwa kwa mashirikiano kati ya Idara ya Mazingira na Idara ya Misitu na Maliasili zisizorejesheka katika kipindi cha mwaka 2012 hadi Aprili 2013, ambapo Idara ya Mazingira imekuwa ikitumia fedha za Serikali na Idara ya Misitu imetumia fedha za washirika wa maendeleo, yaani Serikali ya Finland kupitia Jamhuri ya Uhifadhi wa Wanyamapori (*Wild Conservation Society – WCS*).

Mhe. Mohammed Haji Khalid: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, nakuomba kwanza utupie macho huku na kule kabla ya kumpa mtu nafasi. Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri nina swali moja dogo la nyongeza. Kwa kuwa amekubali kuwa vifuko hivi vinavyofungiwa *juice* navyo vina athari fulani kwa mazingira, na kwa kuwa hii ni biashara kubwa katika nchi hii pamoja na udogo wake lakini vifuko hivi vinaongezeka siku hadi siku.

Je, ofisi yake ina mpango gani wa kuwapatia wafanyabiashara hawa chombo mbadala kwa kufungia *juice* zao badala ya vifuko hivi ambavyo vina athari ya mazingira.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, ni lazima nikiri kwamba kanuni ya kupiga marufuku mifuko ya plastiki ambayo ni ya mwaka 2011 imefanywa kwa kuzingatia sheria yetu ya mazingira ya mwaka 1996 ina changamoto zake katika kuitekeleza na hasa ukizingatia kwamba vifuko hivi vidogo vya plastiki vinatumiwa na wajasiriamali wetu wakiwemo vijana lakini zaidi wanawake ambao wanajikwamua katika suala zima la kujiondoa katika umaskini.

Ni kweli kanuni yetu imepiga marufuku mifuko ya aina yote na ya *size* zote lakini katika utekelezaji wa sheria hii na kwa kutumia busara Mhe. Mwenyekiti, tumekaa na wahusika ambao ni wajasiriamali pamoja na wadau wengine wakiwemo wafanyabiashara kuweza kuangalia njia mbadala ambayo wajasiriamali wetu wataweza kutumia na kuondokana kabisa na mifuko hii ya plastiki. Tatizo liliopo ni kwamba mifuko hii haitumiwi tu kwa kutia *juice* na malai, hivi sasa nyote ni mashahidi kuna malai ambayo yanatengenezwa bila ya kutumia plastiki, unayatia katika chombo fulani na baadae unatoa malai

bila ya kuwemo kwenye kifuko cha plastiki na *juice* sasa hivi zinatumiwa kwenye chupa.

Changamoto tuliyonayo kubwa katika matumizi ya vifuko hivi vya plastiki ni vile ambavyo tunatumia kwa kuwekea viungo (*spices*). Hapa bado ni tatizo kwa sababu wajasiriamali wanadai kwamba bidhaa yao ikiwemo kwenye vifuko vya karatasi basi itapoteza thamani. Njia mbadala ya kutia kwenye vikopo vya ufuniko ni njia ambayo wajasiriamali wetu bado hawajaweza kuimudu. Hivi sasa ofisi yangu inataka kujifunza zaidi kwa nchi ambazo zimefanikiwa kama Rwanda kuweza kuona wao jinsi gani waliweza kukabiliana na tatizo hili.

Mhe. Asha Bakari Makame: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kabla ya yote nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametuwezesha siku hii ya leo kufika hapa katika hali ya uzima na afya. Pia nikushukuru wewe kwa kunipatia nafasi hii pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Waziri nitamuuliza swali (a) na (b) la nyongeza.

(a) Kwa kuwa kunguru wana mitego maalum ya kutegwa na kwa kuwa baadhi ya kunguru wanapewa dawa kama ya sumu. Je, Mhe. Waziri ataliambiaje Baraza lako tukufu ni dawa ya aina gani ya kuuliwa kunguru hao.

(b) Kama ni kwa mitego sawa lakini kama ni kuwapa sumu ya kuweza kuwauwa ajue kama Mhe. Waziri sumu hiyo haimuuwi kunguru tu, sumu hiyo inaweza ikauwa vinyama mbali mbali wakati anapoanguka nguru yule. Ahsante.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kwamba tunatumia mitego, chambo pamoja na sumu katika kuwanasa kunguru hawa weusi ambao ni waharibifu. Nilieleza juzi wakati nafanya majumuisho ya michangio ya bajeti yangu kwamba sumu ile ndio iliyokubaliwa katika viwango vya kimataifa kwamba ina athari ndogo ukilinganisha na nyengine. Sumu hii imepimwa na ipo katika ubora.

Na ni kweli kwamba sumu ni sumu na inaweza sana kuwauwa wanyama wengine. Kinachofanyika kwamba mitego hii inakuwa katika uangalifu mkubwa wa wale ambao wanatumiwa katika maeneo yao katika kuiweka na kuiondosha. Mara nyingi sana mitego hii huwekwa katika sehemu hizo wakati wa alfajiri ambapo kunguru hawa ndio kwa wingi sana wanakwenda katika maeneo ambayo wamezowea kuwepo. Kwa hivyo, athari zipo lakini ni ndogo mno, hakuna sumu ambayo haina athari.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Mwenyekiti, nashukuru kwa kupata nafasi hii ya kuuliza swali hili la mwisho la nyongeza katika swali hili. Kwanza nimpongeze Mhe. Waziri kwa kuweza kujua idadi ya kunguru waliopo Unguja na walioko Pemba na idadi ya kunguru waliyouliwa. Nashukuru kwa utafiti mkubwa aliyoufanya. Kwa sababu lengo ni kuwauwa kunguru wote na Mhe. Waziri ameshaeleza idadi ya kunguru aliyokwishawauwa ambao ni zaidi ya asilimia 50. Je, katika wale waliobakia mpaka hivi leo wamezaana kunguru wangapi wapya wakati takwimu anazo.

Swali la pili hivyo katika utafiti wake hakuna dawa yoyote ambayo itatumika kwa kuwapa kunguru hawa ili wasizaane tena kuwa na uhakika wa kuwa wataondoka moja kwa moja.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais: Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Mjumbe ametaka kujua takwimu ya jinsi gani kunguru hawa wameongezeka kwa kuzaana. Mhe. Mwenyekiti, kwa sasa hivi takwimu hiyo sina isipokuwa inapatikana kwa kufanyiwa makisio sio hasa kwa kuwafuata kunguru mmoja mmoja, lakini kitaalamu zipo *data* na *ratio* ambazo wana-*calculate* na wanajua kiasi gani cha kunguru wameweza kuongezeka kama ambavyo waliweza kuhesabiwa kunguru wenyewe.

Swali la pili Mhe. Mjumbe bado hakuna utafiti uliofanyika na kuweza kuonesha kwamba kuna dawa ambayo inaweza kutumika kwa kuwazuia kunguru hao uzazi. Utafiti huo bado haujafanyika.

Nam. 11

Huduma ya Umeme Kijiji cha Kiuyu Minungwini

(Mhe. Mjumbe aliyetaka kuuliza swali hili ameliondoa)

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2013/2014 – Wizara ya Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, kabla ya kuwasilisha hotuba yangu naomba nitoe taarifa kupitia kwako niwaombe Wajumbe wa Baraza lako tukufu kwamba nitakapoanza kuwasilisha utekelezaji wa kila idara sitasoma majukumu ya kila idara badala yake nitaanza na utekelezaji wa malengo ambapo majukumu ya kila idara yapo kwenye *paragraph* ya kwanza katika kila maelezo ya idara.

Waheshimiwa Wajumbe nawaomba mchukulie kuwa ibara hizo nimezisoma na ziwe sehemu ya kumbukumbu za kikao hiki kama ilivyo katika vitabu mlivyonavyo vya hotuba yangu kwa ajili ya kupata michango na miongozo yenu. Hii ni kwa sababu ya kuokoa muda tu.

Mhe. Mwenyekiti, sasa kwa heshima naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako tukufu sasa likae kama kamati kwa madhumuni ya kupokea, kujadili na hatimae kuidhinisha makadirio ya mapato na matumizi ya fedha ya Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa mwaka wa fedha 2013/2014.

Mhe. Mwenyekiti, Awali ya yote sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu, Mwingi wa Rehma, kwa kutujaalia uzima na afya njema na kutuwezesha kufika hapa kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli hii muhimu kwa maendeleo ya taifa letu.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu, naomba kutumia nafasi hii kumpongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein kwa umahiri wake katika kuiongoza Zanzibar. Chini ya uongozi wake, Serikali kwa kipindi kifupi imetekeleza kwa kiwango kikubwa ahadi alizotoa kwa wananchi wakati wa uchaguzi mkuu kama zilivyoainishwa katika Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya Mwaka 2010. Mafanikio yaliyopatikana chini ya uongozi wake yameongeza kasi ya maendeleo ya nchi yetu na kuwavutia wawekezaji kuendelea kuwekeza nchini na washirika wa maendeleo kuona umuhimu wa kuendelea kuiunga mkono serikali.

Mhe. Mwenyekiti, napenda vile vile kumpongeza Makamu wa Kwanza Rais Mhe. Maalim Seif Sharif Hamad kwa mashirikiano na ushauri anaotupa. Aidha napenda pia kumpongeza Makamu wa Pili wa Rais, Mhe. Balozi Seif Ali Iddi kwa kusimamia vyema shughuli za Serikali na utekelezaji wake. Hotuba yake iliyowasilishwa na Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwenye Baraza lako tukufu wakati akiwasilisha hotuba ya bajeti ya mwaka 2013/2014 ni kielelezo cha ukomavu wake katika uongozi na imeonesha mwelekeo na dira ya utekelezaji wa shughuli za serikali kwa mwaka 2013/2014.

Mhe. Mwenyekiti, naomba pia nikupongeze wewe binafsi kwa kuongoza Baraza letu Tukufu kwa busara na hekma. Nampongeza pia Naibu Spika Mhe. Ali Abdalla Ali, Mwakilishi wa Jimbo la Mfenesini, pamoja na wenyeviti wa Baraza kwa kuendesha vyema shughuli za Baraza.

Mhe. Mwenyekiti, napenda pia kumpongeza Mhe. Ussi Jecha Simai, Mwakilishi wa Jimbo la Chaani, kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Baraza la Wawakilishi ya Katiba, Sheria na Utawala. Pia nampongeza Mhe. Abdalla Juma Abdalla Mwakilishi wa Jimbo la Chonga, kwa kuchaguliwa kuwa Makamu Mwenyekiti na Wajumbe wote walioteuliwa katika Kamati hiyo. Aidha, nawapongeza Wenyeviti, Makamu Wenyeviti na Wajumbe walioteuliwa kwenye Kamati mbali mbali za Baraza lako Tukufu katika zoezi lililofanyika hivi karibuni.

Mhe. Mwenyekiti, namshukuru Mhe. Omar Ali Shehe Mwenyekiti wa Kamati ya Kuchunguza Hesabu za Serikali (*PAC*), Makamu Mwenyekiti wa *PAC* Mhe. Fatma Mbarouk Said na wajumbe wote wa Kamati hii kwa kuipitia na kutoa ushauri wao kuhusu bajeti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali Zanzibar kwa mwaka wa Fedha 2013/14.

Mhe. Mwenyekiti, nachukua fursa hii kutoa shukrani maalum kwa Kamati ya Baraza la Wawakilishi ya Katiba, Sheria na Utawala chini ya Mwenyekiti na Makamu wake kwa ushirikiano, maelekezo na ushauri mzuri iliyotoa wakati wa kupitia taarifa ya utekelezaji wa mpango na bajeti ya mwaka wa fedha 2012/2013 na mapendekezo ya makadirio ya mapato na matumizi ya fedha kwa mwaka 2013/2014, hatua ambayo imetuwezesha kuandaa na kuwasilisha hotuba hii ya bajeti. Mhe. Mwenyekiti, naomba nitumie fursa hii kumshukuru Maalim Abdulhamid Yahya Mzee, Katibu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi ambaye pia ni Mkuu wa Utumishi wa Umma kwa ushirikiano ulioniwezesha kutekeleza majukumu yangu. Nawashukuru pia wananchi wa Jimbo langu la Tumbatu kwa ushirikiano wao wanaonipa na kuniwezesha kutekeleza majukumu yangu ya kutumikia nchi yetu.

MAJUKUMU MAKUU YA WIZARA YA NCHI, OFISI YA RAIS, UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA

Mhe. Mwenyekiti, Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora ina jukumu la kusimamia haki na wajibu wa watumishi wa umma ili waweze kuwahudumia wananchi kwa kiwango cha juu, kuleta ufanisi na kuimarisha utawala bora. Wizara pia ina jukumu la kusimamia, kudhibiti, kuratibu na kutathmini utekelezaji na uongozaji wa utumishi wa umma na utawala bora.

Mhe. Mwenyekiti, utekelezaji wa mpango na bajeti kwa mwaka 2012/2013 umezingatia dira ya maendeleo ya Zanzibar ya mwaka 2020, Awamu ya Pili ya Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umasikini-Zanzibar (MKUZA II), Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2010–2015, mpango mkakati wa maendeleo wa

wizara pamoja na mikataba ya kikanda na kimataifa ambayo nchi yetu imeridhia.

MUUNDO WA WIZARA YA NCHI, OFISI YA RAIS, UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA

Mhe. Mwenyekiti, utekelezaji wa malengo na shughuli za Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora unasimamiwa na Idara na Taasisi zifuatazo pamoja na Ofisi ya Afisa Mdhamini Pemba. Idara hizo ni:-

i. Mipango, Sera na Utafiti,

ii. Uendeshaji na Utumishi,

iii. Mipango ya Raslimali Watu,

iv. Mafunzo na Maendeleo ya Raslimali Watu,

v. Miundo ya Taasisi, Utumishi na Maslahi ya Watumishi,

vi. Utawala Bora,

vii. Nyaraka na Kumbukumbu za Taifa,

viii. Teknolojia ya Habari na Mawasiliano na

ix. Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora-Pemba,

x. Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali,

xi. Kamisheni ya Utumishi wa Umma,

xii. Tume ya Utumishi Serikalini,

xiii. Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi Zanzibar,

xiv. Chuo cha Utawala wa Umma

MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU KWA KIPINDI CHA MWAKA 2012/2013 NA MUELEKEO WA MALENGO KWA MWAKA 2013/2014 KWA KILA IDARA NA TAASISI

Mhe. Mwenyekiti, sasa naomba nichukue nafasi hii kuelezea utekelezaji wa bajeti ya Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa mwaka wa fedha 2012/2013 pamoja na mwelekeo wa malengo ya mwaka wa fedha 2013/2014. Katika kulitekeleza hilo, hotuba yangu itazungumzia maeneo matatu makubwa kwa kila Idara na Taasisi ambayo ni:-

i. Mapitio ya Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2012/2013

ii Mpango wa Utekelezaji wa Majukumu ya Wizara kwa mwaka wa fedha 2013/2014 na maombi ya fedha kwa utekelezaji wa majukumu hayo kwa mwaka wa fedha 2013/2014.

Mhe. Mwenyekiti, utekelezaji wa kazi za Wizara hii kwa kila taasisi ulikuwa kama ifuatavyo:-

IDARA YA MIPANGO, SERA NA UTAFITI:

Majukumu ya Idara:

Mhe. Mwenyekiti, Idara hii ina jukumu la kutoa huduma na utaalamu wa uandaaji wa mipango ya maendeleo, bajeti, ufuatiliaji na tathmini ya programu na miradi ya Ofisi ya Rais - Utumishi wa Umma na Utawala Bora, kutayarisha na kuzifanyia mapitio sera na kufanya tafiti. Vile vile, Idara ina jukumu la kusimamia mageuzi ya utumishi wa umma - Zanzibar na kuandaa mbinu za kutafuta raslimali na misaada mbali mbali kutoka kwa washirika wa maendeleo.

Malengo ya mwaka 2012/2013

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2012/2013, Idara ilipanga kuimarisha mfumo wa mawasiliano ya teknolojia ya habari na mawasiliano, kuandaa mipango ya ofisi, kuratibu na kufuatilia utekelezaji wa shughuli za ofisi ikiwemo programu na miradi. Kutayarisha programu na miradi mipya, kutayarisha mpango mkakati wa utekelezaji wa sera ya usafiri na sera ya mawasiliano ya elektroniki na kusimamia uanzishwaji wa Bima ya afya Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, ili kutekeleza majukumu iliyojipangia katika mwaka wa fedha 2012/2013, Baraza lako tukufu lilidhinisha matumizi ya TZS. 305,621,100. Kati ya fedha hizo, TZS170,621,100 ni kwa utekelezaji wa kazi za kawaida na TZS135,000,000 ni kwa kazi za maendeleo. Aidha, Idara ilitarajia kukusanya mapato ya TZS 1,440, 000, 000.

Utekelezaji wa malengo ya 2012/2013.

Mhe. Mwenyekiti, Idara imeandaa mipango ya kibajeti ya mwaka 2013/2014 na kufanya mapitio ya utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2012/2013. Rasimu ya Mpango Mkakati wa utekelezaji wa Sera ya Serikali Mtandao *(e-Government*) imekamilika na inatarajiwa kuwasilishwa kwa wahusika wengine Unguja na Pemba ili kupata maoni. Aidha, mapitio ya programu ya mageuzi ya utumishi wa umma yamekamilika sambamba na gharama za utekelezaji wa programu hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, katika kuimarisha raslimali fedha, Ofisi ya Rais inaendelea na mazungumzo na Shirika la *USAID* kwa ajili ya kupata fedha za kuendeshea mradi wa kuwajengea uwezo wananchi wa Zanzibar juu ya kuelewa haki zao za msingi na dhana nzima ya utawala bora yanaendelea vizuri. Mazungumzo na *UNDP* kuhusu kusaidia mradi wa kuimarisha Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi yamekamilika na Mkataba wa Makubaliano umeshatiwa saini na pande zote mbili. Mkataba huo utatekelezwa kwa kipindi cha miaka mitatu. mazungumzo na Serikali ya Oman juu ya kugharamia mradi wa "*Digitization of Zanzibar Archives"* yamefanyika na tunategemea karibuni mkataba huo utasainiwa.

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa uanzishwaji wa Bima ya afya Zanzibar, Rasimu ya awali ya upembuzi yakinifu imekamilika na kuonesha wahusika wengi wamekubaliana na azma ya uanzishwaji wa mfuko wa Bima ya Afya. Aidha, takwimu zilizokusanywa zinaonesha kwamba mfuko huo unaweza kuanzishwa na kuhudumia wateja wake kwa ufanisi.

Mhe. Mwenyekiti, hadi kufikia mwezi wa Machi 2013, Idara imetumia jumla ya TZS.98,737,130 kwa kazi za kawaida na TZS 57,249,900 kwa utekelezaji wa kazi za maendeleo. Kutokana na kuchelewa kuanza kwa matumizi ya huduma za mkonga wa mawasiliano ya *ICT* hakuna makusanyo yaliyopatikana na kwa sasa ukusanyaji wa mapato hayo umehamishiwa Ofisi ya Rais Fedha Uchumi na Mipango ya Maendeleo Zanzibar.

Muelekeo na Malengo ya mwaka 2013/2014.

Mhe. Mwenyekiti, idara imepanga kuimarisha mfumo wa habari na Mawasiliano wa wizara ikiwemo kuwawezesha wananchi kuwasiliana na kupata majibu ya huduma zinazotolewa na wizara-*"Interactive Website"*. Kuandaa mipango ya kibajeti na tathmini ya utekelezaji wake, kuibua programu na miradi mipya, kuibua maeneo ya utafiti, kuratibu na kusimamia zoezi la upatikanaji wa mfuko wa Bima ya Afya Zanzibar. Kuandaa sera ya malipo ya mishahara, sera ya uhifadhi wa kumbukumbu

na nyaraka na kutayarisha mpango mkakati wa utekelezaji wa sera ya usafiri wa watumishi wa umma.

Mhe. Mwenyekitii ili kutekeleza majukumu iliyojipangia katika mwaka wa fedha 2013/2014, Idara imepanga kutumia jumla ya TZS 162,956,000 kwa kazi za kawaida na TZS 75,000,000 kwa kazi za maendeleo.

IDARA YA UENDESHAJI NA UTUMISHI

Mhe. Mwenyekiti, idara hii ina jukumu la kutoa huduma za utumishi na uendeshaji katika Ofisi ya Rais - Utumishi wa Umma na Utawala Bora, zikiwemo ajira, maendeleo ya watumishi, kupandisha vyeo na kufanya tathmini ya watumishi, kuhakikisha kuwepo kwa watendaji wa kutosha na wenye sifa pamoja na kuweka kumbukumbu za masuala mbali mbali yanayohusu watumishi. Aidha, Idara inatoa huduma za manunuzi, uhifadhi wa vifaa, huduma za uhasibu na ukaguzi wa ndani, uwekaji wa kumbukumbu za hesabu mapato na matumizi na matayarisho ya ulipaji wa mishahara.

Malengo ya mwaka 2012/2013.

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2012/2013, Idara ilipanga kuhakikisha kuwa ofisi inaweka mazingira bora na ustawi mzuri wa watumishi, kuratibu na kuwezesha kufanya mikutano ya kamati mbali mbali zinazosimamia majukumu ya ofisi, ikiwemo Kamati ya Uongozi wa Ofisi, Kamati ya Ukaguzi, Kamati ya Zabuni na Kamati ya Fedha. Vile vile kuratibu na kutayarisha mikutano ya ushirikiano kati ya Ofisi ya Rais - Utumishi wa Umma na Utawala Bora Zanzibar na Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Wizara ya Fedha na Uchumi na Ofisi ya Rais Utawala Bora SMT, kuwapatia mafunzo wafanyakazi wa ofisi katika viwango mbali mbali ndani na nje ya nchi, kusimamia ujenzi wa makao makuu ya ofisi inayokusudiwa kujengwa katika eneo la Mazizini na kuimarisha kamati maalum inayoshughulikia masuala mtambuka.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2012/2013, Baraza lako tukufu liliidhinisha jumla ya TZS1,034,974,900/= kati ya hizo TZS. 974,974,900/= ni kwa kazi za kawaida na TZS 60,000,000/= ni kwa kazi za maendeleo.

Utekelezaji wa Malengo ya Mwaka 2012/2013.

Mhe. Mwenyekiti, Ofisi ya Rais Utumishi wa Umma na Utawala Bora na Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi zinakusudia kujenga jengo jipya la ofisi katika eneo la Mazizini Unguja. Zoezi la

kumpata Mkandarasi kwa ajili ya ujenzi wa ofisi limekamilika. Kampuni ya *CRJE* ya China imeshinda zabuni ya ujenzi wa jengo hilo na mkataba wa ujenzi tayari umeshatiwa saini.

Mhe. Mwenyekiti, Ofisi katika kuwaendeleza watumishi wake, jumla ya watumishi 19 wanapatiwa mafunzo ya muda mrefu katika ngazi mbali mbali na watumishi 15 walihudhuria mafunzo ya muda mfupi katika vyuo mbali mbali ndani na nje ya nchi.

Mhe. Mwenyekiti, Ofisi na kusimamia Mkutano wa Jumuia ya Kiafrika ya Utumishi wa Umma na Uendeshaji (*AAPAM*) ambapo washiriki **702** walihudhuria, kati ya hao wageni ni 421 na wenyeji ni 281 kutoka nchi mbali mbali duniani walihudhuria mkutano huo (orodha ya washiriki iko katika kiambatisho Namba 1). Kutokana na kufanyika kwa mkutano huo hapa Zanzibar, tumeweza kunufaika sana kiutalii kwa kuitangaza nchi yetu, wajasiriamali waliweza kutangaza na kuuza bidhaa zao, wenye mahoteli na vyombo vya usafiri pia walinufaika kwa kiasi kikubwa na mkutano huo.

Mhe. Mwenyekiti, Idara pia imeanzisha kamati inayosimamia masuala ya Mtambuka na kufanya vikao vya kuandaa mpango kazi na muongozo wa Kamati hiyo. Vile vile, Idara imesimamia vikao kati ya Ofisi ya Rais-Utumishi wa Umma na Utawala Bora Zanzibar na Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma ya Serikali ya Muungano ya Tanzania kuhusu utekelezaji wa makubaliano ya muda ya mgao wa ajira katika taasisi za muungano. Katika utekelezaji wa makubaliano hayo Sekreterieti ya ajira imepatiwa Ofisi katika jengo la Makamo wa Rais wa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania liliopo Tunguu. Aidha, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma imeshatoa toleo kwa taasisi za muungano kuhusu utekelezaji wa makubaliano hayo.

Mhe. Mwenyekiti, hadi kufikia mwezi wa Machi 2013, Idara imetumia jumla ya TZS.791,860,668 kwa kazi za kawaida. Vile vile Idara imetumia TZS 41,644,903 kwa utekelezaji wa kazi za maendeleo.

Muelekeo na Malengo ya mwaka 2013/2014.

Mhe. Mwenyekiti, Idara hii inakusudia kuweka mazingira bora ya ustawi wa watumishi wake kwa kuwapatia huduma bora na kuwajengea uwezo kwa kuwapatia mafunzo kwa mujibu wa kada zao, kuimarisha ushirikiano kati ya Ofisi hii na Ofisi ya Rais-Menejimati ya Utumishi wa Umma ya SMT, kuendelea na usimamizi wa ujenzi wa Ofisi mpya ya Wizara - Mazizini, kuimarisha utekelezaji wa majukumu ya Wizara kupitia Kamati ya Uongozi, Kamati ya Zabuni na Kamati ya Ukaguzi.

Mhe. Mwenyekiti, ili kutekeleza majukumu iliyojipangia katika mwaka wa fedha 2013/2014, Idara imepanga kutumia TZS 886,548,000/= kwa kazi za kawaida.

IDARA YA MIPANGO YA RASLIMALI WATU.

Idara hii ina majukumu ya kupanga, kuratibu na kusimamia mipango ya raslimali watu, kuandaa mpango wa urithishaji uongozi (*Succession Plan)* katika Wizara na Taasisi za umma kwa madhumuni ya kukidhi malengo na mahitaji ya utumishi wa umma.

Mhe. Mwenyekiti, majukumu mengine ya Idara hii ni kuchunguza uwezo uliopo wa raslimali watu (*Human Resource Capacity Assessement*) ili kugundua mahitaji ya rasilimali watu katika utumishi wa umma, kuandaa, kuratibu na kusimamia mpango wa miaka mitano wa raslimali watu na mpango wa kila mwaka, kuweka kumbukumbu za watumishi wa Umma (*Human Resource Database*) na kuidhinisha ikama (*Norminal Roll*) za watumishi wa umma.

Malengo ya mwaka 2012/2013.

Kwa mwaka wa fedha 2012/2013 Idara ilipanga kufanya mapitio ya Ikama ya mwaka 2012/2013 na kuidhinisha Ikama ya mwaka 2013/2014, kuendesha mafunzo ya utayarishaji wa Ikama, umuhimu wa taarifa sahihi na kuziweka katika mfumo wa elektroniki (*database*), maadili ya utumishi wa umma kwa maafisa utumishi na kuandaa mpango wa miaka mitano wa raslimali watu. Aidha, kutayarisha taarifa juu ya hali halisi ya uwezo uliopo wa raslimali watu na kukamilisha mpango wa urithishaji wa uongozi katika utumishi wa umma.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2012/2013, Baraza lako tukufu lilidhinisha jumla ya TZS 138,868,000/= kwa kazi za kawaida.

Utekelezaji wa malengo ya 2012/2013.

Mhe. Mwenyekiti, idara imeendesha mafunzo ya siku 2 kwa maafisa utumishi na wasaidizi maafisa utumishi wa Wizara, idara na taasisi za serikali juu ya namna bora ya utayarishaji wa Ikama, umuhimu wa taarifa sahihi za watumishi na maadili ya utumishi wa umma. Rasimu ya mpango wa miaka mitano ya rasilimali watu iliandaliwa.

Mhe. Mwenyekiti, ripoti ya awali ya taarifa juu ya hali halisi ya uwezo uliopo wa raslimali watu imekamilika. Aidha, muongozo wa mpango wa urithishaji wa uongozi katika utumishi wa umma umekamilika. Vikao vya majadiliano kwa wizara 16 kujadili Ikama vimefanyika ambapo jumla ya maombi ya nafasi mpya 6937 za ajira yaliwasilishwa. Kati ya

maombi hayo nafasi 2464 zilikubaliwa kama inavyoonekana katika kiambatisho Namba 2. Wafanyakazi 449 wanatarajiwa kustaafu kwa kufikia umri wa lazima na katika kuimarisha utendaji kazi jumla ya watumishi 87 walifanyiwa uhamisho katika wizara za serikali. kiambatisho Namba 3.

Mhe. Mwenyekiti, hadi kufikia mwezi wa Machi 2013, idara imetumia jumla ya TZS. 79,502,000 kwa kazi za kawaida.

Muelekeo na Malengo ya mwaka 2013/2014.

Mhe. Mwenyekiti, idara kwa mwaka wa fedha 2013/2014 imepanga kupata maoni ya wahusika wengine juu ya muongozo wa mpango wa raslimali watu katika utumishi wa umma, kutoa taaluma juu ya namna bora ya kutayarisha mpango wa raslimali watu wa miaka mitano na mwaka mmoja mmoja kwa taasisi zote za umma, kuendesha mafunzo kwa maafisa utumishi na maafisa utumishi wasaidizi juu ya utayarishaji bora wa Ikama, kufanya mapitio ya Ikama ya mwaka 2013/2014 na kuidhinisha Ikama ya mwaka 2014/2015. Kuendesha mafunzo ya urithishaji uongozi kwa maafisa waandamizi wa wizara 16. Aidha, Idara itaendelea kukusanya taarifa za kiutumishi na kuziingiza katika mfumo wa Elekroniki (*Human Resource Data Base)*. Kuandaa taarifa za kiutumishi kuanzia 1964-2014 kwa miaka 50 ya mapinduzi na kujifunza mbinu bora za kiutumishi kikanda na kimataifa.

Mhe. Mwenyekiti, ili kutekeleza majukumu iliyojipangia katika mwaka wa fedha 2013/2014 idara imepanga kutumia TZS.177,696,000/= kwa kazi za kawaida na TZS.25,000,000/= kwa kazi za maendeleo.

Malengo ya mwaka 2012/2013.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2012/2013, idara ilipanga kusimamia na kuratibu mafunzo ya watumishi wa umma, kuimarisha uhusiano na mashirikiano na vyuo mbali mbali vya kitaaluma na washirika wa maendeleo ili kuimarisha upatikanaji wa fursa za mafunzo kwa watumishi wa umma. Idara pia imepanga kukamilisha sera ya mafunzo na kuandaa mpango wa utekelezaji na kuanzisha mfumo wa uwekaji wa taarifa za mafunzo ya watumishi wa umma.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kupitia programu ya kitaifa ya kujenga uwezo katika taasisi za serikali, idara ilipanga kukamilisha zoezi la tathmini ya mahitaji ya mafunzo na kuandaa mpango mkuu wa mafunzo kwa watumishi wa umma. idara pia ilipanga kutoa mafunzo mafupi ya ndani kwa watumishi wa kada mbali mbali Unguja na Pemba. Mafunzo hayo yalipangwa kuendeshwa kwa kushirikiana na Chuo cha Utawala wa Umma kwa lengo la kujenga uwezo wa watumishi hasa wa ngazi za chini. Aidha, kwa kupitia nchi wafadhili na washirika wa maendeleo,

idara ilitarajia kuwapatia watumishi 150 mafunzo ya muda mfupi, wa kati na ya muda mrefu katika nchi za Korea, China, Japan, Singapore, India, Thailand, Indonesia na Israel.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2012/2013, Baraza lako tukufu liliidhinisha jumla ya TZS. 313, 430,000/= kati ya hizo TZS 113,430,000/= ni kwa kazi za kawaida na TZS 200,000,000/= ni kwa kazi za maendeleo.

Utekelezaji wa Malengo ya Mwaka 2012/13.

Mhe. Mwenyekiti, Idara imekamilisha rasimu ya sera ya mafunzo hatua inayofuata ni kuiwasilisha kwa Kamati ya Makatibu Wakuu ili kupata maoni zaidi. Katika kuwajengea uwezo watumishi wa umma, jumla ya watumishi 243 wamepatiwa nafasi za mafunzo mbali mbali ndani na nje ya nchi kama kinavyoonesha kiambatanisho namba 4. Kati ya hao watumishi 9 wamepata mafunzo ya shahada ya pili nchini Korea, China na India. Watumishi 234 wamepata mafunzo ya muda mfupi nchini China, India, Korea, Ethiopia, Australia, Japan na Israel.

Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wa mafunzo ya ndani makatibu muhtasi 36 wa mawaziri na makatibu wakuu wa SMZ wamepatiwa mafunzo juu ya utunzaji wa siri na miiko ya kazi katika Chuo cha Utawala wa Umma. Maafisa wawili wa Ofisi ya Rais Utumishi wa Umma walipata mafunzo Dar-es salaam na Zanzibar katika usimamizi wa wakati na mbinu za uandishi wa sheria. Kwa kupitia program za *ITEC*, wanawake wanne (4) kutoka kijiji cha Kandwi walipatiwa mafunzo ya miezi sita huko India kuhusu kutengeneza umeme wa jua na uvunaji wa maji ya mvua. Baada ya kupata mafunzo wamekuwa wataalamu wa kufunga umeme wa jua kijijini kwao na nyumba zaidi ya 100 zimefaidika na mradi huo

Mhe. Mwenyekiti, idara pia iliandaa na kuratibu mafunzo kwa watendaji wakuu wa Serikali ambapo Mawaziri wawili na Makatibu Wakuu wawili walipata mafunzo mafupi nchini China, Wakurugenzi wanne walipata mafunzo mafupi ya uongozi kwa viongozi wanawake huko Morogoro na wakurugenzi watano walipata mafunzo juu ya uandishi bora wa ripoti huko Morogoro.

Idara imeweza kukusanya taarifa za watumishi wa serikali waliopo masomoni kwa mwaka 2012/2013 ambapo jumla ya watumishi 728 wapo katika mafunzo mbali mbali ndani na nje ya nchi. Aidha mkataba wa mafunzo baina ya muajiri na muajiriwa umekamilika na umesambazwa katika taasisi zote za serikali na umeanza kutumika kuanzia Januari 2013, usarifu wa daftari la kumbukumbu za mafunzo ya watumishi umekamilika.

Mhe. Mwenyekiti, hadi kufikia mwezi wa Machi 2013, Idara imetumia jumla ya TZS.67,117,700 kwa kazi za kawaida. Vile vile Idara imetumia TZS 15,074,000 kwa utekelezaji wa kazi za maendeleo.

Muelekeo na Malengo ya mwaka 2013/2014.

Mhe. Mwenyekiti, idara imepanga kusimamia na kuratibu mafunzo ya watumishi wa umma kwa kada mbali mbali yanayotolewa na nchi wahisani, kuandaa mafunzo mafupi kwa kada zilizo chini ya utumishi kama vile madereva, wahudumu na maafisa utumishi, kuichapisha na kuandaa mpango mkakati wa utekelezaji wa sera ya mafunzo. Vile vile, idara imepanga kuendesha mafunzo mafupi ya viongozi wa ngazi mbali mbali. Aidha, Idara kwa kushirikiana na Chuo cha Utawala wa Umma imepanga kuratibu mafunzo mafupi ya maadili ya kazi kwa watumishi wapya.

Mhe. Mwenyekiti, idara kwa kupitia programu ya kitaifa ya kujenga uwezo, imepanga kuendesha mafunzo ya ujasiriamali kwa watumishi 449 ambao wanatarajiwa kustaafu mwaka 2013/2014 ili kuwajengea uwezo wa kuwa na mipango mizuri.

Baada ya kustaafu. Idara itakamilisha mpango mkuu wa mafunzo kwa watumishi wa serikali.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2013/2014, idara inaomba jumla ya TZS111,698,000/= kwa kazi za kawaida na TZS125,000,000/= kwa kazi za maendeleo.

IDARA YA MIUNDO YA TAASISI, UTUMISHI NA MASLAHI YA WATUMISHI.

Malengo ya mwaka 2012/2013

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2012/2013 Idara ilipanga kutoa muongozo juu ya utayarishaji wa mkataba wa kutoa huduma kwa wateja *(Client Service Charter)*, kuratibu na kushauri ajira za wageni ndani ya utumishi wa umma, kuanzisha na kufuatilia utekelezaji wa mfumo wa kupima utendaji kazi katika wizara, idara na taasisi za umma.

Mhe. Mwenyekiti, idara ilipanga kuimarisha mfumo wa taarifa za malipo ya watumishi wa umma, kuwajengea uwezo maafisa utumishi kutumia mfumo wa taarifa za malipo ya watumishi wa umma, kutengeneza sera ya malipo ya watumishi wa umma. Aidha, Idara ilipanga kuwajengea uwezo watumishi wa umma juu ya sheria na kanuni za utumishi wa umma na kufanya tathmini ya kazi na viwango (*Job evaluation and grading*) na kufanya mapitio ya majukumu ya wizara, idara na taasisi za serikali.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2012/2013 jumla ya TZS439,804,000/= ziliidhinishwa kutumika. Kati ya hizo TZS 151,804,000/= ni kwa kazi za kawaida na TZS 288,000,000/= ni kwa kazi za maendeleo.

Utekelezaji wa Malengo ya 2012/2013.

Mhe. Mwenyekiti, idara imetoa mafunzo ya sheria ya utumishi wa umma kwa taasisi 5 imetayarisha muungozo wa utayarishaji wa mkataba wa huduma kwa mteja na kutoa

Nam603

IMESAHIHISHWA

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora: (Anaendelea) Idara imetoa mafunzo ya Sheria ya Utumishi wa Umma kwa Taasisi tano. Imetayarisha muongozo wa utayarishaji wa mkataba wa huduma kwa mteja na kutoa mafunzo ya utayarishaji wa mkataba huo kwa Wizara ya Afya, Wizara ya Kilimo na Maliasili na Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Muongozo wa upimaji wa utendaji kazi (*Performance Appraisal)* katika Wizara na Idara za Serikali umetayarishwa na kujumuishwa katika kanuni za Utumishi wa Umma.

Mhe. Mwenyekiti, rasimu ya mapendekezo ya majukumu ya kazi za Wizara 16 imeandaliwa. Aidha, katika kuimarisha mfumo wa taarifa za watumishi, zoezi la kuunganisha taarifa za watumishi na mfumo wa malipo ya mishahara linaendelea katika hatua za mwisho kwa kuweka taarifa muhimu zikiwemo tarehe za kuzaliwa, tarehe ya kuthibitishwa kazi, kuanza ajira, kiwango cha elimu, ngazi ya mshahara, eneo la kazi pamoja na kada ya mtumishi.

Mhe. Mwenyekiti, hadi kufikia mwezi wa Machi 2013, Idara imetumia jumla ya TZS. 79,707,840 kwa kazi za kawaida na TZS 325,137,000 kwa utekelezaji wa kazi za maendeleo.

Muelekeo na Malengo ya mwaka 2013/2014.

Mhe. Mwenyekiti, Idara imepanga kufanya tathmini na ufuatiliaji wa utekelezaji wa miundo ya utumishi kwa Wizara za Serikali na Taasisi zote za

umma, kufanya mapitio ya mishahara na malipo mengine ya watumishi wa umma. Kuandaa muongozo wa kufanya tathmini ya uchambuzi wa kazi na madaraja (*Job Evaluation and Grading*), kutoa elimu kwa watendaji wa Wizara 16 kuhusu Sheria ya Utumishi wa Umma na kanuni zake katika maslahi na usimamizi wa watumishi wa umma, kukamilisha zoezi la kupitia majukumu ya serikali na kufanya tathmini ya idadi ya watumishi wa umma na mahitaji ya taasisi (*Staffing levels*). Vile vile kuendelea na kazi ya kutoa taaluma ya utayarishaji wa mkataba wa utoaji huduma kwa mteja kwa Taasisi zilizobakia na kufanya ufuatiliaji kwa wizara zilizopatiwa mafunzo ya uandaaji wa mkataba.

Mhe. Mwenyekiti, ili kutekeleza majukumu iliyojipangia katika mwaka wa fedha 2013/2014, idara inaliomba Baraza lako tukufu kuidhinisha TZS163, 834, 000/= kwa kazi za kawaida na TZS 25,000,000/= kwa kazi za maendeleo.

IDARA YA UTAWALA BORA.
Majukumu ya Idara

Mhe. Mwenyekiti, idara ina jukumu la kuratibu na kutathmini utekelezaji wa misingi mbali mbali ya utawala bora ikiwa ni pamoja na kuratibu na kusimamia sera, sheria na Kanuni katika kuhakikisha haki za binadamu zinalindwa, maadili ya viongozi yanakuwepo na amani na utulivu vinaimarishwa. Majukumu mengine ya Idara hii ni kutoa elimu ya uraia kwa wananchi ili kuhakikisha wananchi wanashirikishwa moja kwa moja au kwa kupitia viongozi wao waliowachagua katika kufanya maamuzi pamoja na kuelewa haki na wajibu kwa kuzingatia misingi ya utawala bora.

Malengo ya mwaka 2012/2013
Mhe. Mwenyekiti, Idara katika mwaka 2012/2013 ilipanga kutoa mafunzo, kufuatilia na kutathmini juu ya uwazi na uwajibikaji kwa watendaji wa utumishi wa umma, kutayarisha vipindi vya elimu ya uraia na kuvirusha hewani kwa kutumia vikundi vya sanaa na ziara za vijijini. Aidha Idara ilipanga kufanya kampeni za ushajiishaji wa haki za binadamu kwa njia ya semina, makongamano, kalenda, mikutano na kutoa vipeperushi kwa wananchi, kuadhimisha siku ya haki za binadamu na siku ya kupambana na rushwa duniani, kufanya mikutano ya robo mwaka kwa Kikundi-Kazi cha utawala bora, na kutoa ripoti ya mwaka ya utawala bora Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, ili kutekeleza malengo hayo kwa mwaka wa fedha 2012/2013, Baraza lako tukufu liliidhinisha matumizi ya jumla ya TZS 186,161,000 kwa ajili ya utekelezaji wa kazi za kawaida.

Utekelezaji wa Malengo ya 2012/2013.
Mhe. Mwenyekiti, katika kutekeleza sera ya utawala bora, idara ilifanya mikutano mitano ya kikundi kazi cha utawala bora na kutoa mafunzo ya namna ya uandaaji wa viashiria, vigezo vya kupima utawala bora na uandishi wa ripoti ya utawala bora. Idara imerusha hewani vipindi vya elimu ya uraia kupitia Shirika la Utangazaji Zanzibar. Aidha Idara imetoa elimu kwa njia ya radio na televisheni kuhusu sera ya utawala bora na kuzuia rushwa kupitia vikundi vya sanaa. Idara pia imetoa elimu ya uraia na haki za binadamu kwa Shehia tano za Unguja ambazo ni Chaani kubwa, Matetema, Kazole, Pwanimchangani na Kiwengwa. Elimu kama hiyo ilitolewa katika Shehia tatu na taasisi mbili kisiwani Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, ripoti ya utawala bora ya mwaka 2012 imekamilika na mapendekezo ya kuimarisha misingi ya utawala bora nchini yametolewa. Aidha, Mswada wa Sheria ya Maadili ya Viongozi umetayarishwa na umeshapelekwa katika Kamati ya Makatibu Wakuu kwa kujadiliwa na baadae kufuatiwa na hatua nyengine za utungaji wa Sheria. Utayarishaji wa maadili ya kitaifa ambayo yatasomeka pamoja na sheria ya maadili ya viongozi umekamilika.

Mhe. Mwenyekiti, idara ilitoa mafunzo kwa watendaji kuhusu masuala ya kuzuia rushwa na utayarishaji wa mkakati wa kuzuia rushwa. Midahalo na wanasheria kutoka taasisi mbali mbali za serikali, jumuiya za kiraia pamoja na wataalamu na wanafunzi wa vyuo vikuu vya Zanzibar ilifanyika kwa lengo la kujua mianya ya rushwa kwa ajili ya kuisaidia Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi katika kutekeleza kazi zake pamoja na kutoa makala zenye kutoa ujumbe wa kuzuia rushwa na uhujumu wa uchumi.

Mhe. Mwenyekiti, hadi kufikia mwezi wa Machi 2013, idara imetumia jumla ya TZS. 106,600,300 kwa kazi za kawaida. Vile vile idara imetumia TZS 150,863,559 kutoka *UNDP* kwa utekelezaji wa kazi za maendeleo.

Muelekeo na Malengo ya mwaka 2013/2014.
Mhe. Mwenyekiti, Idara imepanga kuandaa Mpango wa mafunzo ya utawala bora na Serikali ya Umoja wa Kitaifa (*GNU*), kuendelea kutoa mafunzo juu ya misingi ya utawala bora kwa viongozi wa kisiasa na kiutendaji, kufanya tafiti ndogo ndogo za utawala bora zitakazosaidia kuimarisha ripoti ya mwaka ya utawala bora, kuinua uelewa wa Kikundi Kazi kinachoshughulikia masuala ya kijamii hasa kwa kuangalia muongozo wa viwango vya kimataifa juu ya majukumu ya kijamii kwa Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, idara imepanga kutayarisha vipindi vya elimu ya uraia na kuvirusha hewani kwa kupitia vyombo vya habari na kufanya ziara vijijini,

kufanya kampeni za ushajiishaji wa haki za binadamu kwa wananchi, kufanya mikutano ya robo mwaka kwa kikundi kazi cha utawala bora, pamoja na kutayarisha na kusambaza ripoti ya mwaka ya utawala bora.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2013/2014 Idara imepanga kutumia jumla ya TZS 216,504,000 kwa kazi za kawaida.

IDARA YA NYARAKA NA KUMBUKUMBU ZA TAIFA

Majukumu ya Idara:

Mhe. Mwenyekiti, Idara hii ina majukumu ya kuhifadhi Nyaraka na kumbukumbu muhimu za taifa, kuhifadhi nyaraka muhimu za kihistoria na kutoa huduma za utafiti, kutumia mbinu za kitaalamu kwa kuzifanyia matengenezo nyaraka zilizo katika hali mbaya, kuendeleza, kusimamia na kuelekeza utumiaji bora wa kumbukumbu katika ofisi za serikali. Idara pia ina jukumu la kutoa taaluma juu ya umuhimu wa kutunza kumbukumbu ili zipewe umuhimu unaostahili.

Malengo ya mwaka 2012/2013

Mhe. Mwenyekiti, Idara kwa mwaka wa fedha 2012/2013 ilipanga kufanya ukaguzi katika ofisi za kuhifadhia kumbukumbu katika Mikoa na Wilaya, kuzifanyia matengenezo nyaraka na kumbukumbu chakavu na kuweka mitambo ya *CCTV* kwa ajili ya kuimarisha usalama wa jengo la Idara ya Nyaraka na Kumbukumbu. Idara pia ilipanga kutayarisha sera ya menejimenti ya kumbukumbu na nyaraka, kutayarisha mfumo bora wa usimamizi wa kumbukumbu na nyaraka pamoja na kuimarisha mfumo bora wa utunzaji kumbukumbu katika masjala za wizara, taasisi na mashirika ya serikali. Vile vile kuwapatia mafunzo, warsha na semina wafanyakazi wa idara na kuwapatia maslahi na kuwaekea mazingira bora ya kazi.

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2012/2013 Idara ya Nyaraka na Kumbukumbu za Taifa ilipanga kutumia jumla ya TZS. 671,155,500/=, kati ya hizo TZS. 245,649,500 kwa kazi za kawaida na TZS. 425,506,000/= kwa kazi za maendeleo.

Utekelezaji wa malengo ya 2012/2013.

Mhe. Mwenyekiti, idara imezifanyia matengenezo jumla ya nyaraka 128, watafiti 236 wamehudumiwa kati ya hao watafiti 197 ni Watanzania na 39 ni wageni kutoka nchi za nje. Wanafunzi 31 wamepatiwa mafunzo ya kinadharia na kivitendo juu ya uhifadhi kumbukumbu na nyaraka. (Kiambatisho Namba 5 kinatoa uchambuzi zaidi)

Mhe. Mwenyekiti, ukaguzi wa awali umefanyika pamoja na kutoa mafunzo mafupi, ushauri na maelekezo muhimu kuhusiana na mfumo bora wa utunzaji na uhifadhi kumbukumbu katika wizara na taasisi tano za serikali, Ofisi za Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya na za Halmashauri katika Mikoa yote mitatu ya Unguja.

Mhe. Mwenyekiti, semina ya mafunzo ya usimamizi wa kumbukumbu kwa wanamasjala na watunza kumbukumbu 30 kutoka katika Ofisi za Mikoa, Wilaya na Halmashauri kwa Unguja imetolewa. Watumishi 12 walipatiwa mafunzo ya muda mfupi na kufanya ziara za kubadilishana uzoefu Tanzania Bara pamoja na kutayarisha muongozo wa usimamizi wa masjala (*Standard Operating Procedures*), daftari la uhai wa kumbukumbu na muongozo wa ufuatiliaji na tathmini kwa kazi za usimamizi wa kumbukumbu.

Mhe. Mwenyekiti, hadi kufikia mwezi wa Machi 2013, Idara imetumia jumla ya TZS. 130,277,348 kwa kazi za kawaida. Vile vile idara imetumia TZS 62,133,760 kwa utekelezaji wa kazi za maendeleo.

Muelekeo na Malengo ya mwaka 2013/2014.
Mhe. Mwenyekiti, idara imepanga kutayarisha mfumo wa uhifadhi nyaraka kwa njia ya elektroniki, kutayarisha mgawanyo wa majalada (*File Classification*) na daftari la uhai wa kumbukumbu (*Retention Schedule)* kulingana na majukumu ya msingi ya wizara, idara, mashirika na taasisi za umma.

Mhe. Mwenyekiti, katika kuimarisha ulinzi na usalama wa nyaraka na kumbukumbu, Idara imepanga kununua mtambo wa *CCTV* pamoja na kufanya matengenezo madogo madogo ya jengo, kuimarisha mfumo bora wa usimamizi wa kumbukumbu pamoja na kutoa mafunzo ya mfumo wa usimamizi wa kumbukumbu kwa wafanyakazi wa masjala na wasimamizi wa kumbukumbu kwa Wizara 11 zilizobakia.

Mhe. Mwenyekiti, idara itaendelea kufanya kazi za ukaguzi wa kumbukumbu na nyaraka katika taasisi za umma, kuwajengea uwezo wafanyakazi kwa kushiriki katika semina, mikutano ya kitaifa na kimataifa, kuratibu vikao vinne vya Bodi ya Ushauri wa Nyaraka na Kumbukumbu za Taifa na kuweka mazingira bora ya ofisi pamoja na kuwapatia watumishi ustawi na mazingira bora ya kazi.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka 2013/2014 Idara imepanga kutumia TZS 525,565,000/= kwa kazi za kawaida.

IDARA YA TEKNOLOJIA YA HABARI NA MAWASILIANO

Majukumu ya Idara

Mhe. Mwenyekiti, majukumu ya idara hii ni kusimamia kumbukumbu za utumishi wa umma na matumizi, uendeshaji na usimamizi wa teknolojia ya habari na mawasiliano katika utumishi wa umma, kuhakikisha kuwa usimamizi wa kumbukumbu teknolojia ya habari na mawasiliano unakuwa na utoaji bora wa huduma katika utumishi wa umma, kutoa miongozo ya utoaji, uthibitishaji, usajili, uwekaji na uenezaji wa taarifa ulipo kwenye mfumo wa elektroniki katika utumishi wa umma, kutoa miongozo na kanuni kuhusu usimamizi wa kumbukumbu za utumishi wa umma, kuanzisha mfumo wa pamoja utakaotumika na taasisi zote za umma na kuweka mazingira mazuri ya utekelezaji wa jumla ya dhana ya serikali iliyounganishwa kielektroniki.

Muelekeo na Malengo ya Mwaka 2013/2014

Mhe. Mwenyekiti, Idara imepanga kuandaa miongozo na viwango vya kiusalama kwa matumizi ya mifumo na vifaa vya kompyuta – (*Guidelines and Standards of Computer program and devices*), kuimarisha mfumo wa umeme uliopo, kuwapatia mafunzo ya muda mfupi wafanyakazi wa idara, kutoa elimu kwa viongozi wa serikali, viongozi wa siasa, viongozi wengine wa kijamii, watu wenye mahitaji maalum na wananchi juu ya dhana nzima ya serikali mtandao.

Mhe. Mwenyekiti, idara imepanga kufanya upembuzi yakinifu juu ya utayari wa serikali pamoja na wananchi juu ya matumizi ya huduma za kijamii zitakazotolewa na kupatikana katika mfumo wa kompyuta (*e-services*), kushirikiana na wahusika wengine kuhakikisha taasisi zote za serikali zinaunganishwa katika kituo cha Serikali Mtandao na kujenga vituo vya huduma za kijamii (*Community center)* mijini na vijijini, kushiriki katika semina, makongamano na mikutano ya kitaifa na kimataifa ya mashirikiano ya uimarishaji wa huduma za Serikali Mtandao.

Mhe. Mwenyekiti, ili kutekeleza majukumu iliyojipangia kwa mwaka wa fedha 2013/2014, tunaliomba Baraza lako tukufu kuidhinishia matumizi ya jumla ya TZS. 812,751,000 ambapo TZS. 362,751,000 kwa kazi za kawaida na TZS 450,000,000 kwa kazi za maendeleo.

OFISI YA RAIS, UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA – PEMBA.

Majukumu ya Ofisi:

Mhe. Mwenyekiti, Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora - Pemba ina jukumu la kuratibu na kusimamia masuala ya utawala na uendeshaji, mipango, sera na utafiti, mipango ya raslimali watu na maendeleo ya watumishi, mishahara na maslahi ya watumishi, kuimarisha utawala bora na haki za binadamu na kusimamia shughuli za kuratibu hifadhi ya nyaraka na kumbukumbu na kuratibu mafunzo ya muda mfupi na mrefu kwa watumishi wa umma.

Malengo ya mwaka 2012/2013.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2012/2013, Ofisi Kuu Pemba ilipanga kuimarisha mfumo wa teknolojia ya habari na mawasiliano, kuratibu utayarishaji wa sera ya malipo ya mishahara kwa watumishi, kuratibu warsha juu ya matumizi ya Sheria ya Utumishi wa Umma na Kanuni zake, kuratibu mafunzo ya namna bora ya utayarishaji wa Ikama, kuratibu mafunzo kwa maafisa Wadhamini juu uandaaji wa mpango wa raslimali watu na mafunzo ya kuwaandaa maafisa waandamizi kushika nafasi za uongozi.

Mhe. Mwenyekiti, Ofisi Kuu Pemba pia ilipanga kuwapatia mafunzo ya muda mrefu wafanyakazi wanne (4) wa ofisi kwa ngazi ya shahada na stashahada, kuratibu mafunzo ya muda mrefu na mfupi ndani na nje ya nchi kwa watumishi wa umma Pemba, kuandaa na kutoa mafunzo juu ya mapambano dhidi ya VVU/UKIMWI kwa wafanyakazi wa ofisi, kuweka mazingira mazuri ya kazi kwa kuhakikisha kwamba vifaa na mahitaji mengine ya ofisi yanapatikana na kutoa huduma kwa wakati.

Aidha ofisi ilipanga kuratibu mikutano ya wazi ya kutoa mafunzo ya elimu ya uraia kwa wananchi katika Shehia 6 na kushauriana na wahusika wengine juu ya haki za binadamu, kufanya kampeni juu ya haki za binadamu na kutoa mafunzo ya utawala bora kwa viongozi wa serikali kwa upande wa Pemba. Vile vile ofisi ilipanga kuimarisha uhifadhi wa nyaraka na kumbukumbu kwa kuwapatia mafunzo watunza kumbukumbu wa taasisi zote za serikali na kufanya ukaguzi wa utunzaji wa kumbukumbu katika taasisi za serikali.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2012/2013, Baraza lako tukufu liliidhinisha TZS 468,881,000/= kwa ajili ya kutekeleza kazi za kawaida.

Utekelezaji wa malengo ya 2012/2013.
Mhe. Mwenyekiti, Ofisi Kuu Pemba iliendesha warsha ya siku moja juu ya utayarishaji wa Ikama kwa maofisa utumishi wa wizara na taasisi zote za serikali-Pemba. Pia ufuatiliaji ulifanywa kwa wizara zote 16 kuangalia utekelezaji wa kazi hiyo.

Aidha, ofisi ilikamilisha zoezi la uhakiki wa majalada binafsi ya wafanyakazi, kwa lengo la kupata taarifa sahihi za wafanyakazi ambapo wizara zote kwa Pemba zimefanyiwa uhakiki huo. Ofisi imeratibu warsha ya siku moja juu ya mpango wa urithishwaji uongozi, kwa Maofisa Wadhamini, Maofisa Tawala na Maofisa Mipango wa Mikoa.

Mhe. Mwenyekiti, ofisi iliendelea kufanya ukaguzi na ukusanyaji wa kumbukumbu katika Ofisi ya Mrajis Mkuu wa Serikali Wete, Ofisi ya Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana Pemba, Wizara ya Afya Wete na Hosptali ya Abdalla Mzee Mkoani. Vile vile, Ofisi iliendelea kuhamisha "*Indexes*" kutoka mfumo wa kawaida kwenda mfumo wa elektroniki. Aidha, Ofisi iliendesha semina ya siku moja ya Sheria ya Utumishi wa Umma Na. 2 ya mwaka 2011, kwa Maofisa Utumishi wa Taasisi zote za Serikali Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, Ofisi ilitoa mafunzo ya utawala bora na haki za binadamu kwa wananchi katika Shehia tatu na taasisi mbili, nazo ni Shehia ya Ndagoni, Piki na Ngwachani, Chuo cha Kiislamu Micheweni na Skuli ya Kengeja Ufundi. Aidha, mafunzo ya utawala bora yalitolewa kwa wafanyakazi wa ngazi za chini wakiwemo maofisa mishahara, maofisa kalamazoo na maofisa uendeshaji kwa Wizara tano za SMZ. Ofisi iliendesha semina ya siku moja kuhusu utawala bora kwa maofisa uendeshaji na utumishi.

Pia ilitoa huduma mbali mbali za kiutawala na uendeshaji. Katika kuwajengea uwezo watumishi wa ofisi, wafanyakazi wawili wanaendelea na mafunzo ya shahada ya kwanza na wawili stashahada. Aidha, ofisi ilitoa mafunzo juu ya elimu ya Ukimwi na jinsia kwa wafanyakazi wake wote.

Mhe. Mwenyekiti, Ofisi iliratibu mafunzo ya muda mfupi kwa watumishi wa umma ambapo watumishi kumi wamepatiwa mafunzo mbali mbali nje ya nchi. Aidha ofisi imeratibu warsha ya kujadili 'Sera ya mafunzo" kwa Maofisa Wadhamini na Maofisa wa mafunzo.

Mhe. Mwenyekiti, hadi kufikia mwezi wa Machi 2013, Ofisi imetumia jumla ya TZS. 239,546,023 kwa utekelezaji wa kazi za kawaida.

Muelekeo na Malengo ya mwaka 2013/2014

Mhe. Mwenyekiti, Ofisi Kuu Pemba imepanga kuimarisha misingi ya utawala bora kwa kutoa mafunzo ya watendaji wakuu wa taasisi za Serikali na jumuiya za kiraia. Pia kwa kushirikiana na Idara ya Utawala Bora, Ofisi itaandaa mpango wa mafunzo ya utawala bora, kutoa elimu juu ya misingi ya utawala bora pamoja na Serikali ya Umoja wa Kitaifa (*GNU*) kwa viongozi wa kisiasa na wa kiutendaji kwa taasisi za serikali na jumuiya za kiraia.

Vile vile, itaratibu mafunzo kwa kamati za Shehia juu ya masuala ya haki za binadamu, kufanya tafiti, kuandaa programu ya elimu ya uraia, kuandaa vipindi vya redio, kutoa elimu ya uraia kwa makundi maalum na Kamati za Shehia, kuweka mazingira mazuri ya Idara kwa kununua vitendea kazi.

Mhe. Mwenyekiti, Ofisi itaratibu warsha ya kujadili na kupata maoni juu ya muongozo wa mpango wa raslimali watu, kuratibu warsha ya kutoa taaluma juu ya namna bora ya kutayarisha mpango wa raslimali watu (miaka mitano na mwaka mmoja mmoja), kuratibu mafunzo ya urithishaji uongozi kwa wizara 16- Pemba, kuratibu mafunzo kwa maafisa utumishi juu ya utayarishaji bora wa Ikama.

Mhe. Mwenyekiti, Ofisi imepanga kuendelea na kazi za uhifadhi wa kumbukumbu kwa njia ya elektroniki, kufanya mgawanyo wa majalada na daftari la uhai wa kumbukumbu kulingana na majukumu ya msingi ya wizara, idara na taasisi za serikali.

Mhe. Mwenyekiti, ofisi itafanya tathmini ya utekelezaji wa miundo ya utumishi, kuratibu mafunzo juu ya matumizi ya Sheria ya Utumishi wa Umma na Kanuni zake kwa Wizara 5-Pemba, kuimarisha huduma za kiutawala kwa wafanyakazi wa ofisi na kuweka mazingira mazuri ya ofisi.

Mhe. Mwenyekiti, Ofisi Kuu Pemba kwa mwaka wa fedha 2013/2014 inategemea kutumia TZS 434,448,000 kwa kazi za kawaida.

OFISI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI

Majukumu ya Ofisi:

Mhe. Mwenyekiti, jukumu la ofisi hii ni kuidhinisha utoaji fedha kutoka Mfuko Mkuu wa Hazina ya Serikali, kufanya ukaguzi wa matumizi ya fedha hizo na raslimali nyengine kutoka serikalini, washirika wa maendeleo kupitia miradi, programu mbali mbali na kutoa taarifa za ukaguzi kwa mujibu wa Katiba na Sheria. Lengo kuu la ukaguzi ni kuleta ufanisi katika upatikanaji wa raslimali za umma na matumizi yake ili kuondoa ubadhirifu, wizi, matumizi

mabaya ya raslimali na kutotimiza wajibu wakati wa utekelezaji wa majukumu.

Malengo ya mwaka 2012/2013

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2012/2013, Ofisi ilipanga kufanya ukaguzi wa hesabu za Serikali kwa wizara na taasisi zote za umma, kuwajengea uwezo watumishi wake katika fani mbali mbali, kupitia na kurekebisha muongozo maalum wa ukaguzi na kutoa mafunzo mbali mbali kwa wafanyakazi na wahusika wengine na kushajihisha utumiaji wa viwango vilivyowekwa kimataifa katika ufungaji na uwekaji wa kumbukumbu.

Mhe. Mwenyekiti, ofisi ilipanga kufanya marekebisho ya Sheria ya Ukaguzi Nam.11 ya 2003, kuimarisha mawasiliano na wahusika wengine juu ya majukumu na malengo ya Ofisi kwa kutumia njia tofauti za mawasiliano kama vile tovuti, majarida, vipeperushi, mikutano, makongomano na semina kwa wahusika wengine juu ya muongozo wa ukaguzi.

Vile vile, Ofisi ilipanga kutoa mafunzo ya ukaguzi kwa kompyuta, ukaguzi yakinifu, ukaguzi wa mazingira na aina nyengine za ukaguzi. Pamoja na kutumia muongozo wa kazi za ukaguzi, mafunzo hayo yana azma ya kuongeza ubora wa ripoti za ukaguzi zinazotolewa.

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2012/2013, Ofisi iliidhinishiwa TZS1,889,000,000/= kwa ajili ya matumizi ya kawaida na kukusanya TZS 10,000,000/=.

Utekelezaji wa malengo ya 2012/2013.
Mhe. Mwenyekiti, ofisi imeendelea na majukumu yake ya ukaguzi wa hesabu za mwaka 2011/2012 katika taasisi mbali mbali za Serikali kwa kufuata muongozo wa ukaguzi. Ripoti ya ukaguzi ya mwaka 2010/2011 imekamilika na tayari imeshawasilishwa katika Baraza la Wawakilishi, watendaji saba wameshiriki katika mafunzo yanayoendeshwa na taasisi kuu za ukaguzi duniani. Aidha, Mjumbe mmoja wa Kamati ya Kuchunguza Hesabu (*PAC*) alihudhuria mkutano wa *SADCOPAC*.

Mhe. Mwenyekiti, ofisi imeendelea kuwawekea mazingira mazuri watumishi wake ambapo ada ya masomo pamoja na gharama nyengine zimelipwa kwa wafanyakazi 13 waliojiunga na vyuo 2012/2013 na 17 wanaoendelea na masomo yao ya muda mrefu katika vyuo mbali mbali. Kwa upande wa mafunzo ya muda mfupi, jumla ya wafanyakazi 30 wamepatiwa mafunzo ya ukaguzi yakinifu pamoja na tathmini ya kugundua maeneo hatarishi ya ukaguzi (*Risk Based Audit*) sambamba na mafunzo ya viwango vya ukaguzi

vya kimataifa. Aidha, ofisi imepitia na kurekebisha muongozo maalum wa ukaguzi.

Mhe. Mwenyekiti, hadi kufikia mwezi wa Machi 2013, Ofisi imetumia jumla ya TZS. 1,257,913,540 kwa utekelezaji wa kazi za kawaida.

Muelekeo na Malengo ya mwaka 2013/2014

Mhe. Mwenyekiti, **o**fisi itaendelea kufanya ukaguzi wa hesabu za serikali za wizara na taasisi zake zote, kuimarisha uwezo wa wafanyakazi kitaaluma katika fani mbali mbali za ukaguzi. Vile vile, kufanya matengenezo makubwa ya jengo la ofisi kuu iliyopo Pemba, kutoa mafunzo mbali mbali kwa wafanyakazi, kuwashajihisha wahusika wengine juu ya utumiaji wa viwango vilivyowekwa kimataifa katika ufungaji wa hesabu na uwekaji wa kumbukumbu.

Mhe. Mwenyekiti, katika kuimarisha ukaguzi kwa kutumia mfumo wa elektroniki, ofisi imepanga kufanya ununuzi wa "s*oftware* na *server*", kutoa mafunzo ya kompyuta na uchambuzi wa taarifa za kiukaguzi kwa kompyuta na ukaguzi yakinifu na kutumia muongozo wa kazi za ukaguzi. Mafunzo hayo yana azma ya kuongeza ubora wa ripoti za ukaguzi.

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2013/2014 Ofisi imepanga kutumia jumla ya TZS1,911,000,000/= kwa ajili ya kutekeleza malengo yake iliyojipangia na kukusanya TZS.15,000,000/=

KAMISHENI YA UTUMISHI WA UMMA
Majukumu ya Kamisheni.

Mhe. Mwenyekiti, majukumu makuu ya taasisi hii ni kutoa ushauri kwa Mhe. Rais kuhusu masuala yote ya Utumishi wa Umma, kuwezesha utendaji wa watendaji wakuu wa taasisi za umma kufikia utawala unaolenga matokeo bora, kufuatilia na kutathmini usimamizi wa watendaji wakuu kwa kufanya uchunguzi na ukaguzi wa raslimali watu katika utumishi wa umma, kupokea na kushughulikia rufaa na malalamiko dhidi ya maamuzi yanayotolewa na mamlaka za ajira na nidhamu katika utumishi wa umma.

Malengo ya mwaka 2012/2013

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2012/2013, Kamisheni ilipanga kutekeleza majukumu yake ya kuzitangaza Sheria na Kanuni za Utumishi wa Umma, kutoa miongozo, ufafanuzi na mafunzo kwa mamlaka za ajira na washirika wengine juu ya kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu za Utumishi

wa Umma. Aidha, Kamisheni ilipanga kufanya uchunguzi na ukaguzi wa raslimali watu katika utumishi wa umma, kupitia na kuidhinisha miundo ya utumishi, miundo ya taasisi na miundo ya mishahara kama itakavyopendekezwa na Tume za Utumishi.

Mhe. Mwenyekiti, Kamisheni ilipanga kufuatilia na kutathmini utendaji wa watendaji wakuu wa taasisi za umma. Vile vile, ilipanga kutayarisha na kuwasilisha kwa Mhe. Rais ripoti ya mwaka ya hali halisi ya utumishi wa umma kama ilivyoelekezwa na Sheria ya Utumishi wa Umma Nam.2 ya mwaka 2011. Pia ilipanga kufanya ziara za kikazi kwenye mamlaka za ajira na nidhamu katika utumishi wa umma.

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2012/2013, Kamisheni iliidhinishiwa kiasi cha TZS 737,000,000/= kwa kazi za kawaida.

Utekelezaji wa Malengo ya 2012/2013.

Mhe. Mwenyekiti, Kamisheni imefanya vikao 20 kwa lengo la kuwaelimisha watendaji wakuu wa Wizara, Idara Maalum, Bodi za Mashirika ya Umma, Wakala wa Serikali, Mikoa, Wilaya, Manispaa, Mabaraza ya Miji na Halmashauri zote Unguja na Pemba kuhusu majukumu ya Kamisheni na Tume za Utumishi.

Pia Kamisheni imetayarisha rasimu za awali za miongozo kuhusu uchunguzi na ukaguzi wa raslimali watu, utayarishaji na uwasilishaji wa taarifa za raslimali watu na ripoti ya mwaka ya hali halisi ya utumishi wa umma. Vile vile, iliidhinisha miundo ya utumishi ya Wizara 16 za SMZ, ilipokea na kuzingatia mapendekezo ya miundo ya utumishi kutoka Tume ya Utumishi ya Baraza la Wawakilishi, Tume ya Utumishi ya Mahakama na Tume ya Utumishi ya Idara Maalum.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu mapendekezo ya miundo ya taasisi, Kamisheni imepokea mapendekezo ya Bodi ya Mamlaka ya Mafunzo ya Amali na Taasisi ya Sayansi na Teknolojia na mapendekezo ya kuanzishwa kwa Shirika la Nyumba Zanzibar na Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar na hatua za kuyafanyia kazi mapendekezo hayo zinaendelea.

Mhe. Mwenyekiti, Kamisheni pia ilipokea na kuzifanyia kazi rufaa saba za masuala ya nidhamu kutoka Benki ya Watu wa Zanzibar, Idara ya Mahakama Pemba, Shirika la Utangazaji Zanzibar, Shirika la Bandari Zanzibar na Wizara ya Kilimo na Maliasili Zanzibar.

Aidha, malalamiko matano ya kinidhamu kutoka taasisi mbali mbali zikiwemo Idara Maalum, Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo, Shirika la Bima, Tume ya Utumishi Serikalini na Shirika la Umeme yalipokelewa na kufanyiwa kazi. Kamisheni pia imewajengea uwezo wa kiuongozi Makamishna saba na uwezo wa kiutendaji watumishi wanane kwa kuwapatia ziara za mafunzo ya muda mfupi ndani ya nchi.

Mhe. Mwenyekiiti, hadi kufikia mwezi wa Machi 2013, Kamisheni imetumia jumla ya TZS. 268,475,230 kwa utekelezaji wa kazi za kawaida.

Muelekeo na Malengo ya mwaka2013/2014

Mhe. Mwenyekiti, Kamisheni imepanga kuandaa na kuratibu mikutano 15 na ziara 15 kwa ajili ya kushughulikia na kutoa maamuzi ya masuala ya miundo ya utumishi,

Nam904

IMESAHIHISHWA

Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: (anaendelea) imetayarisha muongozo wa utayarishaji wa mkataba wa huduma kwa mteja na kutoa mafunzo ya utayarishaji wa mkataba huo kwa Wizara ya Afya, Wizara ya Kilimo na Maliasili na Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Muongozo wa upimaji wa utendaji kazi (*Performance Appraisal)* katika Wizara na Idara za Serikali umetayarishwa na kujumuishwa katika kanuni za Utumishi wa Umma.

Mhe. Mwenyekiti, rasimu ya mapendekezo ya majukumu ya kazi za Wizara 16 imeandaliwa. Aidha, katika kuimarisha mfumo wa taarifa za watumishi, zoezi la kuunganisha taarifa za watumishi na mfumo wa malipo ya mishahara linaendelea katika hatua za mwisho kwa kuweka taarifa muhimu zikiwemo tarehe za kuzaliwa, tarehe ya kuthibitishwa kazi, kuanza ajira, kiwango cha elimu, ngazi ya mshahara, eneo la kazi pamoja na kada ya mtumishi.

Mhe. Mwenyekiti, hadi kufikia mwezi wa Machi 2013, Idara imetumia jumla ya shilingi 79,707,840/= kwa kazi za kawaida na shilingi 325,137,000/= kwa utekelezaji wa kazi za maendeleo.

Muelekeo na Malengo ya mwaka 2013/2014.

Mhe. Mwenyekiti, Idara imepanga kufanya tathmini na ufuatiliaji wa utekelezaji wa miundo ya utumishi kwa Wizara za Serikali na Taasisi zote za umma, kufanya mapitio ya mishahara na malipo mengine ya watumishi wa umma.

Kuandaa muongozo wa kufanya tathmini ya uchambuzi wa kazi na madaraja (*Job Evaluation and Grading*), kutoa elimu kwa watendaji wa Wizara 16 kuhusu Sheria ya Utumishi wa Umma na kanuni zake katika maslahi na usimamizi wa watumishi wa umma, kukamilisha zoezi la kupitia majukumu ya Serikali na kufanya tathmini ya idadi ya watumishi wa umma na mahitaji ya taasisi (*Staffing levels*). Vile vile kuendelea na kazi ya kutoa taaluma ya utayarishaji wa mkataba wa utoaji huduma kwa mteja kwa taasisi zilizobakia na kufanya ufuatiliaji kwa Wizara zilizopatiwa mafunzo ya uandaaji wa mkataba huo.

Mhe. Mwenyekiti, ili kutekeleza majukumu iliyojipangia katika mwaka wa fedha 2013/2014, Idara inaliomba Baraza lako tukufu kuidhinisha TZS 163,834,000/= kwa kazi za kawaida na TZS 25,000,000/= kwa kazi za maendeleo.

IDARA YA UTAWALA BORA.

Malengo ya mwaka 2012/2013

Mhe. Mwenyekiti, Idara katika mwaka 2012/2013 ilipanga kutoa mafunzo, kufuatilia na kutathmini juu ya uwazi na uwajibikaji kwa watendaji wa utumishi wa umma, kutayarisha vipindi vya elimu ya uraia na kuvirusha hewani kwa kutumia vikundi vya sanaa na ziara za vijijini.

Aidha Idara ilipanga kufanya kampeni za ushajiishaji wa haki za binadamu kwa njia ya semina, makongamano, kalenda, mikutano na kutoa vipeperushi kwa wananchi, kuadhimisha siku ya haki za binadamu na siku ya kupambana na rushwa duniani, kufanya mikutano ya robo mwaka kwa Kikundi-Kazi cha Utawala Bora, na kutoa ripoti ya mwaka ya Utawala Bora Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, ili kutekeleza malengo hayo, kwa mwaka wa fedha 2012/2013 Baraza lako tukufu liliidhinisha matumizi ya jumla ya shilingi 186,161,000/= kwa ajili ya utekelezaji wa kazi za kawaida.

Utekelezaji wa Malengo ya 2012/2013

Mhe. Mwenyekiti, idara imetoa mafunzo ya sheria ya Utumishi wa Umma kwa taasisi 5 imetayarisha muungozo wa utayarishaji wa mkataba wa huduma kwa mteja na kutoa katika kutekeleza Sera ya Utawala Bora, Idara ilifanya

mikutano mitano ya kikundi kazi cha Utawala Bora na kutoa mafunzo ya namna ya uandaaji wa viashiria, vigezo vya kupima Utawala Bora na uandishi wa ripoti ya Utawala Bora. Idara imerusha hewani vipindi vya elimu ya uraia kupitia Shirika la Utangazaji Zanzibar.

Aidha Idara imetoa elimu kwa njia ya radio na televisheni kuhusu sera ya utawala bora na kuzuia rushwa kupitia vikundi vya sanaa. Idara pia imetoa elimu ya uraia na haki za binadamu kwa Shehia tano za Unguja ambazo ni Chaani kubwa, Matetema, Kazole, Pwanimchangani na Kiwengwa. Elimu kama hiyo ilitolewa katika Shehia tatu na taasisi mbili kisiwani Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, ripoti ya utawala bora ya mwaka 2012 imekamilika na mapendekezo ya kuimarisha misingi ya utawala bora nchini yametolewa. Aidha, Mswada wa Sheria ya Maadili ya Viongozi umetayarishwa na umeshapelekwa katika Kamati ya Makatibu Wakuu kwa kujadiliwa na baadae kufuatiwa na hatua nyengine za utungaji wa Sheria. Utayarishaji wa maadili ya kitaifa ambayo yatasomeka pamoja na sheria ya maadili ya viongozi umekamilika.

Mhe. Mwenyekiti, idara ilitoa mafunzo kwa watendaji kuhusu masuala ya kuzuia rushwa na utayarishaji wa mkakati wa kuzuia rushwa. Midahalo na Wanasheria kutoka Taasisi mbali mbali za Serikali, jumuiya za kiraia pamoja na wataalamu na wanafunzi wa Vyuo Vikuu vya Zanzibar ilifanyika kwa lengo la kujua mianya ya rushwa kwa ajili ya kuisaidia Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi katika kutekeleza kazi zake pamoja na kutoa makala zenye kutoa ujumbe wa kuzuia rushwa na uhujumu wa uchumi.

Mhe. Mwenyekiti, hadi kufikia mwezi wa Machi 2013, Idara imetumia jumla ya shilingi 106,600,300/= kwa kazi za kawaida. Vile vile Idara imetumia shilingi 150,863,559/= kutoka *UNDP* kwa utekelezaji wa kazi za maendeleo.

Muelekeo na Malengo ya mwaka 2013/2014.

Mhe. Mwenyekiti, Idara imepanga kuandaa mpango wa mafunzo ya utawala bora na Serikali ya Umoja wa Kitaifa (*GNU*), kuendelea kutoa mafunzo juu ya misingi ya utawala bora kwa viongozi wa kisiasa na kiutendaji, kufanya tafiti ndogo ndogo za utawala bora zitakazosaidia kuimarisha ripoti ya mwaka ya Utawala Bora, kuinua uelewa wa Kikundi Kazi kinachoshughulikia masuala ya kijamii hasa kwa kuangalia muongozo wa viwango vya kimataifa juu ya majukumu ya kijamii kwa Zanzibar.

IDARA YA NYARAKA NA KUMBUKUMBU ZA TAIFA

Mhe. Mwenyekiti, idara hii ina majukumu ya kuhifadhi nyaraka na kumbukumbu muhimu za taifa, kuhifadhi nyaraka muhimu za kihistoria na kutoa huduma za utafiti, kutumia mbinu za kitaalamu kwa kuzifanyia matengenezo nyaraka zilizo katika hali mbaya, kuendeleza, kusimamia na kuelekeza utumiaji bora wa kumbukumbu katika Ofisi za Serikali. Idara pia ina jukumu la kutoa taaluma juu ya umuhimu wa kutunza kumbukumbu ili zipewe umuhimu unaostahili.

Malengo ya mwaka 2012/2013

Mhe. Mwenyekiti, idara kwa mwaka wa fedha 2012/2013 ilipanga kufanya ukaguzi katika ofisi za kuhifadhia kumbukumbu katika Mikoa na Wilaya, kuzifanyia matengenezo nyaraka na kumbukumbu chakavu na kuweka mitambo ya *CCTV* kwa ajili ya kuimarisha usalama wa jengo la Idara ya Nyaraka na Kumbukumbu. Idara pia ilipanga kutayarisha sera ya menejimenti ya kumbukumbu na nyaraka, kutayarisha mfumo bora wa usimamizi wa kumbukumbu na nyaraka pamoja na kuimarisha mfumo bora wa utunzaji kumbukumbu katika masjala za wizara, taasisi na mashirika ya serikali. Vile vile, kuwapatia mafunzo, warsha na semina wafanyakazi wa Idara na kuwapatia maslahi na kuwaekea mazingira bora ya kazi.

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2012/2013 Idara ya Nyaraka na Kumbukumbu za Taifa ilipanga kutumia jumla ya shilingi 671,155,500/=, kati ya hizo shilingi 245,649,500/= kwa kazi za kawaida na shilingi 425,506,000/= kwa kazi za maendeleo.

Utekelezaji wa malengo ya 2012/2013.

Mhe. Mwenyekiti, Idara imezifanyia matengenezo jumla ya nyaraka 128, watafiti 236 wamehudumiwa kati ya hao watafiti 197 ni Watanzania na 39 ni wageni kutoka nchi za nje. Wanafunzi 31 wamepatiwa mafunzo ya kinadharia na kivitendo juu ya uhifadhi kumbukumbu na nyaraka. (Kiambatisho Namba 5) kinatoa uchambuzi zaidi)

Mhe. Mwenyekiti, ukaguzi wa awali umefanyika pamoja na kutoa mafunzo mafupi, ushauri na maelekezo muhimu kuhusiana na mfumo bora wa utunzaji na uhifadhi kumbukumbu katika wizara na taasisi tano za serikali, Ofisi za Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya na za Halmashauri katika Mikoa yote mitatu ya Unguja.

Mhe. Mwenyekiti, semina ya mafunzo ya usimamizi wa kumbukumbu kwa wanamasjala na watunza kumbukumbu 30 kutoka katika Ofisi za Mikoa, Wilaya na Halmashauri kwa Unguja imetolewa. watumishi 12 walipatiwa

mafunzo ya muda mfupi na kufanya ziara za kubadilishana uzoefu Tanzania Bara pamoja na kutayarisha muongozo wa usimamizi wa masjala (*Standard Operating Procedures*), daftari la uhai wa kumbukumbu na muongozo wa ufuatiliaji na tathmini kwa kazi za usimamizi wa kumbukumbu.

Mhe. Mwenyekiti, hadi kufikia mwezi wa Machi 2013, Idara imetumia jumla ya shilingi 130,277,348/= kwa kazi za kawaida. Vile vile Idara imetumia shilingi 62,133,760/= kwa utekelezaji wa kazi za maendeleo.

Muelekeo na Malengo ya mwaka 2013/2014.

Mhe. Mwenyekiti, idara imepanga kutayarisha mfumo wa uhifadhi nyaraka kwa njia ya elektroniki, kutayarisha mgawanyo wa majalada (*File Classification*) na daftari la uhai wa kumbukumbu (*Retention Schedule*) kulingana na majukumu ya msingi ya Wizara, Idara, Mashirika na Taasisi za Umma.

Katika kuimarisha ulinzi na usalama wa nyaraka na kumbukumbu, Idara imepanga kununua mtambo wa *CCTV* pamoja na kufanya matengenezo madogo madogo ya jengo, kuimarisha mfumo bora wa usimamizi wa kumbukumbu pamoja na kutoa mafunzo ya mfumo wa usimamizi wa kumbukumbu kwa wafanyakazi wa masjala na wasimamizi wa kumbukumbu kwa wizara 11 zilizobakia.

Mhe. Mwenyekiti, Idara itaendelea kufanya kazi za ukaguzi wa kumbukumbu na nyaraka katika taasisi za umma, kuwajengea uwezo wafanyakazi kwa kushiriki katika semina, mikutano ya kitaifa na kimataifa, kuratibu vikao vinne vya Bodi ya Ushauri wa Nyaraka na kumbukumbu za taifa na kuweka mazingira bora ya ofisi pamoja na kuwapatia watumishi ustawi na mazingira bora ya kazi. Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka 2013/2014 Idara imepanga kutumia TZS 525,565,000/= kwa kazi za kawaida.

IDARA YA TEKNOLOJIA YA HABARI NA MAWASILIANO.
Muelekeo na Malengo ya Mwaka 2013/2014

Mhe. Mwenyekiti, Idara imepanga kuandaa miongozo na viwango vya kiusalama kwa matumizi ya mifumo na vifaa vya kompyuta – (*Guidelines and Standards of Computer program and devices*), kuimarisha mfumo wa umeme uliopo, kuwapatia mafunzo ya muda mfupi wafanyakazi wa Idara, kutoa elimu kwa viongozi wa Serikali, viongozi wa siasa, viongozi wengine wa kijamii, watu wenye mahitaji maalumu na wananchi juu ya dhana nzima ya Serikali Mtandao.

Mhe. Mwenyekiti, Idara imepanga kufanya upembuzi yakinifu juu ya utayari wa Serikali pamoja na wananchi juu ya matumizi ya huduma za kijamii zitakazotolewa na kupatikana katika mfumo wa kompyuta *(e-services)*, kushirikiana na wahusika wengine kuhakikisha taasisi zote za serikali zinaunganishwa katika kituo cha Serikali Mtandao na kujenga vituo vya huduma za kijamii (*Community center)* mijini na vijijini, kushiriki katika semina, makongamano na mikutano ya kitaifa na kimataifa ya mashirikiano ya uimarishaji wa huduma za Serikali Mtandao.

Mhe. Mwenyekiti, ili kutekeleza majukumu iliyojipangia kwa mwaka wa fedha 2013/2014, tunaliomba Baraza lako tukufu kuidhinishia matumizi ya jumla ya shilingi 812,751,000/= ambapo shilingi 362,751,000/= kwa kazi za kawaida na shilingi 450,000,000/= kwa kazi za maendeleo.

OFISI YA RAIS, UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA – PEMBA.
Malengo ya mwaka 2012/2013.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2012/2013, Ofisi Kuu Pemba ilipanga kuimarisha mfumo wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano, kuratibu utayarishaji wa sera ya malipo ya mishahara kwa watumishi, kuratibu warsha juu ya matumizi ya Sheria ya Utumishi wa Umma na kanuni zake, kuratibu mafunzo ya namna bora ya utayarishaji wa Ikama, kuratibu mafunzo kwa Maafisa wadhamini juu uandaaji wa Mpango wa raslimali watu na mafunzo ya kuwaandaa maafisa waandamizi kushika nafasi za uongozi.

Mhe. Mwenyekiti, Ofisi Kuu Pemba, pia ilipanga kuwapatia mafunzo ya muda mrefu wafanyakazi wanne (4) wa ofisi kwa ngazi ya shahada na stashahada, kuratibu mafunzo ya muda mrefu na mfupi ndani na nje ya nchi kwa watumishi wa umma Pemba, kuandaa na kutoa mafunzo juu ya mapambano dhidi ya VVU/UKIMWI kwa wafanyakazi wa Ofisi, kuweka mazingira mazuri ya kazi kwa kuhakikisha kwamba vifaa na mahitaji mengine ya Ofisi yanapatikana na kutoa huduma kwa wakati.

Aidha Ofisi ilipanga kuratibu mikutano ya wazi ya kutoa mafunzo ya elimu ya uraia kwa wananchi katika Shehia 6 na kushauriana na wahusika wengine juu ya haki za binadamu, kufanya kampeni juu ya haki za binadamu na kutoa mafunzo ya utawala bora kwa viongozi wa Serikali kwa upande wa Pemba. Vile vile ofisi ilipanga kuimarisha uhifadhi wa nyaraka na kumbukumbu kwa kuwapatia mafunzo watunza kumbukumbu wa taasisi zote za serikali na kufanya ukaguzi wa utunzaji wa kumbukumbu katika taasisi za serikali.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2012/2013, Baraza lako tukufu liliidhinisha shilingi 468,881,000/= kwa ajili ya kutekeleza kazi za kawaida.

Utekelezaji wa malengo ya 2012/2013.

Mhe. Mwenyekiti, Ofisi Kuu Pemba iliendesha warsha ya siku moja juu ya utayarishaji wa Ikama kwa maofisa utumishi wa wizara na taasisi zote za Serikali-Pemba. Pia ufuatiliaji ulifanywa kwa wizara zote 16 kuangalia utekelezaji wa kazi hiyo. Aidha, ofisi ilikamilisha zoezi la uhakiki wa majalada binafsi ya wafanyakazi, kwa lengo la kupata taarifa sahihi za wafanyakazi ambapo wizara zote kwa Pemba zimefanyiwa uhakiki huo. Ofisi imeratibu warsha ya siku moja juu ya mpango wa urithishwaji uongozi, kwa maofisa wadhamini, maofisa tawala na maofisa mipango wa mikoa.

Mhe. Mwenyekiti, Ofisi iliendelea kufanya ukaguzi na ukusanyaji wa kumbukumbu katika Ofisi ya Mrajis Mkuu wa Serikali Wete, Ofisi ya Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana Pemba, Wizara ya Afya Wete na Hosptali ya Abdalla Mzee Mkoani. Vile vile, Ofisi iliendelea kuhamisha "*Indexes*" kutoka mfumo wa kawaida kwenda mfumo wa elektroniki. Aidha, ofisi iliendesha semina ya siku moja ya Sheria ya Utumishi wa Umma Na. 2 ya mwaka 2011, kwa maofisa utumishi wa taasisi zote za Serikali Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, ofisi ilitoa mafunzo ya utawala bora na haki za binadamu kwa wananchi katika Shehia tatu na taasisi mbili, nazo ni Shehia ya Ndagoni, Piki na Ngwachani, Chuo cha Kiislamu Micheweni na Skuli ya Kengeja Ufundi. Aidha, mafunzo ya utawala bora yalitolewa kwa wafanyakazi wa ngazi za chini wakiwemo maofisa mishahara, maofisa kalamazoo na maofisa uendeshaji kwa wizara tano za SMZ.

Ofisi iliendesha semina ya siku moja kuhusu utawala bora kwa maofisa uendeshaji na utumishi. Pia ilitoa huduma mbali mbali za kiutawala na uendeshaji. Katika kuwajengea uwezo watumishi wa ofisi, wafanyakazi wawili wanaendelea na mafunzo ya shahada ya kwanza na wawili stashahada. Aidha, ofisi ilitoa mafunzo juu ya elimu ya Ukimwi na jinsia kwa wafanyakazi wake wote.

Mhe. Mwenyekiti, ofisi iliratibu mafunzo ya muda mfupi kwa watumishi wa umma ambapo watumishi kumi wamepatiwa mafunzo mbali mbali nje ya nchi. Aidha ofisi imeratibu warsha ya kujadili 'sera ya mafunzo" kwa maofisa wadhamini na maofisa wa mafunzo.

Mhe. Mwenyekiti, hadi kufikia mwezi wa Machi 2013, ofisi imetumia jumla ya shilingi 239,546,023/= kwa utekelezaji wa kazi za kawaida.

Muelekeo na Malengo ya mwaka 2013/2014

Mhe. Mwenyekiti, Ofisi Kuu Pemba imepanga kuimarisha misingi ya tawala bora kwa kutoa mafunzo ya watendaji wakuu wa taasisi za serikali na jumuiya za kiraia. Pia kwa kushirikiana na Idara ya Utawala Bora, ofisi itaandaa mpango wa mafunzo ya utawala bora, kutoa elimu juu ya misingi ya utawala bora pamoja na Serikali ya Umoja wa Kitaifa (*GNU*) kwa viongozi wa kisiasa na wa kiutendaji kwa taasisi za serikali na jumuiya za kiraia.

Vile vile utaratibu mafunzo kwa kamati za Shehia juu ya masuala ya haki za binadamu, kufanya tafiti, kuandaa programu ya elimu ya uraia, kuandaa vipindi vya redio, kutoa elimu ya uraia kwa makundi maalum na Kamati za Shehia, kuweka mazingira mazuri ya Idara kwa kununua vitendea kazi.

Mhe. Mwenyekiti, ofisi itaratibu warsha ya kujadili na kupata maoni juu ya muongozo wa mpango wa raslimali watu, kuratibu warsha ya kutoa taaluma juu ya namna bora ya kutayarisha mpango wa raslimali watu (miaka mitano na mwaka mmoja mmoja), kuratibu mafunzo ya urithishaji uongozi kwa wizara 16- Pemba, kuratibu mafunzo kwa maafisa utumishi juu ya utayarishaji bora wa Ikama.

Mhe. Mwenyekiti, ofisi imepanga kuendelea na kazi za uhifadhi wa kumbukumbu kwa njia ya elektroniki, kufanya mgawanyo wa majalada na daftari la uhai wa kumbukumbu kulingana na majukumu ya msingi ya Wizara, Idara na Taasisi za Serikali.

Mhe. Mwenyekiti, ofisi itafanya tathmini ya utekelezaji wa miundo ya utumishi, kuratibu mafunzo juu ya matumizi ya sheria ya utumishi wa umma na Kanuni zake kwa Wizara 5-Pemba, kuimarisha huduma za kiutawala kwa wafanyakazi wa ofisi na kuweka mazingira mazuri ya ofisi.

Mhe. Mwenyekiti, Ofisi Kuu Pemba kwa mwaka wa fedha 2013/2014 inategemea kutumia shilingi 434,448,000/= kwa kazi za kawaida.

OFISI YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI.
Malengo ya mwaka 2012/2013

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2012/2013, ofisi ilipanga kufanya ukaguzi wa hesabu za Serikali kwa Wizara na Taasisi zote za Umma, kuwajengea uwezo watumishi wake katika fani mbali mbali, kupitia na kurekebisha muongozo maalum wa ukaguzi na kutoa mafunzo mbali mbali

kwa wafanyakazi na wahusika wengine na kushajihisha utumiaji wa viwango vilivyowekwa kimataifa katika ufungaji na uwekaji wa kumbukumbu.

Mhe. Mwenyekiti, ofisi ilipanga kufanya marekebisho ya Sheria ya Ukaguzi Nam.11 ya 2003, kuimarisha mawasiliano na wahusika wengine juu ya majukumu na malengo ya Ofisi kwa kutumia njia tofauti za mawasiliano kama vile tovuti, majarida, vipeperushi, mikutano, makongomano na semina kwa wahusika wengine juu ya muongozo wa ukaguzi. Vile vile, Ofisi ilipanga kutoa mafunzo ya ukaguzi kwa kompyuta, ukaguzi yakinifu, ukaguzi wa mazingira na aina nyengine za ukaguzi. Pamoja na kutumia muongozo wa kazi za ukaguzi, mafunzo hayo yana azma ya kuongeza ubora wa ripoti za ukaguzi zinazotolewa.

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2012/2013, Ofisi iliidhinishiwa shilingi 1,889,000,000/= kwa ajili ya matumizi ya kawaida na kukusanya shilingi 10,000,000/=.

Utekelezaji wa malengo ya 2012/2013.

Mhe. Mwenyekiti, ofisi imeendelea na majukumu yake ya ukaguzi wa hesabu za mwaka 2011/2012 katika taasisi mbali mbali za serikali kwa kufuata muongozo wa ukaguzi. Ripoti ya ukaguzi ya mwaka 2010/2011 imekamilika na tayari imeshawasilishwa katika Baraza la Wawakilishi, watendaji saba wameshiriki katika mafunzo yanayoendeshwa na taasisi kuu za ukaguzi duniani. Aidha, Mjumbe mmoja wa Kamati ya Kuchunguza Hesabu (*PAC*) alihudhuria mkutano wa *SADCOPAC*.

Mhe. Mwenyekiti, ofisi imeendelea kuwawekea mazingira mazuri watumishi wake ambapo ada ya masomo pamoja na gharama nyengine zimelipwa kwa wafanyakazi 13 waliojiunga na vyuo 2012/2013 na 17 wanaoendelea na masomo yao ya muda mrefu katika vyuo mbali mbali. Kwa upande wa mafunzo ya muda mfupi, jumla ya wafanyakazi 30 wamepatiwa mafunzo ya ukaguzi yakinifu pamoja na tathmini ya kugundua maeneo hatarishi ya ukaguzi (*Risk Based Audit*) sambamba na mafunzo ya viwango vya ukaguzi vya kimataifa. Aidha, Ofisi imepitia na kurekebisha muongozo maalum wa ukaguzi.

Mhe. Mwenyekiti, hadi kufikia mwezi wa Machi 2013, Ofisi imetumia jumla ya shilingi 1,257,913,540/= kwa utekelezaji wa kazi za kawaida.

Muelekeo na Malengo ya mwaka 2013/2014

Mhe. Mwenyekiti, Ofisi itaendelea kufanya ukaguzi wa hesabu za Serikali za Wizara na Taasisi zake zote, kuimarisha uwezo wa wafanyakazi kitaaluma katika fani mbali mbali za ukaguzi. Vile vile, kufanya matengenezo makubwa ya jengo la Ofisi Kuu iliyopo Pemba, kutoa mafunzo mbali mbali kwa wafanyakazi, kuwashajihisha wahusika wengine juu ya utumiaji wa viwango vilivyowekwa kimataifa katika ufungaji wa hesabu na uwekaji wa kumbukumbu.

Mhe. Mwenyekiti, katika kuimarisha ukaguzi kwa kutumia mfumo wa elektroniki ofisi imepanga kufanya ununuzi wa *"Software* na *Server*", kutoa mafunzo ya kompyuta na uchambuzi wa taarifa za kiukaguzi kwa kompyuta na ukaguzi yakinifu na kutumia muongozo wa kazi za ukaguzi. Mafunzo hayo yana azma ya kuongeza ubora wa ripoti za ukaguzi.

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2013/2014 Ofisi imepanga kutumia jumla ya shilingi 1,911,000,000/= kwa ajili ya kutekeleza malengo yake iliyojipangia na kukusanya shilingi 15, 000,000/= .

KAMISHENI YA UTUMISHI WA UMMA.

Malengo ya mwaka 2012/2013

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2012/2013, Kamisheni ilipanga kutekeleza majukumu yake ya kuzitangaza Sheria na Kanuni za Utumishi wa Umma, kutoa miongozo, ufafanuzi na mafunzo kwa mamlaka za ajira na washirika wengine juu ya kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu za Utumishi wa Umma. Aidha, Kamisheni ilipanga kufanya uchunguzi na ukaguzi wa raslimali watu katika utumishi wa umma, kupitia na kuidhinisha miundo ya utumishi, miundo ya taasisi na miundo ya mishahara kama itakavyopendekezwa na Tume za Utumishi.

Mhe. Mwenyekiti, Kamisheni ilipanga kufuatilia na kutathmini utendaji wa watendaji wakuu wa taasisi za umma. Vile vile ilipanga kutayarisha na kuwasilisha kwa Mhe. Rais ripoti ya mwaka ya hali halisi ya utumishi wa umma kama ilivyoelekezwa na Sheria ya Utumishi wa Umma Nam.2 ya mwaka 2011. Pia ilipanga kufanya ziara za kikazi kwenye mamlaka za ajira na nidhamu katika utumishi wa umma.

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2012/2013, Kamisheni iliidhinishiwa kiasi cha shilingi 737,000,000/= kwa kazi za kawaida.

Utekelezaji wa Malengo ya 2012/2013.

Mhe. Mwenyekiti, Kamisheni imefanya vikao 20 kwa lengo la kuwaelimisha watendaji wakuu wa Wizara, Idara Maalum, Bodi za Mashirika ya Umma, Wakala wa Serikali, Mikoa, Wilaya, Manispaa, Mabaraza ya Miji na Halmashauri zote Unguja na Pemba kuhusu majukumu ya Kamisheni na Tume za Utumishi.

Pia Kamisheni imetayarisha rasimu za awali za miongozo kuhusu uchunguzi na ukaguzi wa raslimaliwatu, utayarishaji na uwasilishaji wa taarifa za raslimali watu na ripoti ya mwaka ya hali halisi ya utumishi wa umma. Vile vile, ilidhinisha miundo ya utumishi ya wizara 16 za SMZ, ilipokea na kuzingatia mapendekezo ya miundo ya utumishi kutoka Tume ya Utumishi ya Baraza la Wawakilishi, Tume ya Utumishi ya Mahakama na Tume ya Utumishi ya Idara Maalum.

Mhe. Mwenyekiti, kuhusu mapendekezo ya miundo ya taasisi, Kamisheni imepokea mapendekezo ya Bodi ya Mamlaka ya Mafunzo ya Amali na Taasisi ya Sayansi na Teknologia na mapendekezo ya kuanzishwa kwa Shirika la Nyumba Zanzibar na Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar na hatua za kuyafanyia kazi mapendekezo hayo zinaendelea.

Mhe. Mwenyekiti, Kamisheni pia ilipokea na kuzifanyia kazi rufaa saba za masuala ya nidhamu kutoka Benki ya Watu wa Zanzibar, Idara ya Mahakama Pemba, Shirika la Utangazaji Zanzibar, Shirika la Bandari Zanzibar na Wizara ya Kilimo na Maliasili Zanzibar.

Aidha, malalamiko matano ya kinidhamu kutoka taasisi mbali mbali zikiwemo Idara Maalum, Wizara ya Habari, Utamaduni, Utalii na Michezo, Shirika la Bima, Tume ya Utumishi Serikalini na Shirika la Umeme yalipokelewa na kufanyiwa kazi. Kamisheni pia imewajengea uwezo wa kiuongozi Makamishna saba na uwezo wa kiutendaji watumishi wanane kwa kuwapatia ziara za mafunzo ya muda mfupi ndani ya nchi.

Mhe. Mwenyekiti, hadi kufikia mwezi wa Machi 2013, Kamisheni imetumia jumla ya shilingi 268,475,230/= kwa utekelezaji wa kazi za kawaida.

Muelekeo na Malengo ya mwaka2013/2014

Mhe. Mwenyekiti, Kamisheni imepanga kuandaa na kuratibu mikutano 15 na ziara 15 kwa ajili ya kushughulikia

Nam 105

IMESAHIHISHWA

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora: (Anaendelea) ni matumizi ya fungu 48 ya Tume ya Utumishi serikalini na TZS 810,000,000 ni matumizi ya fungu 50 kwa ajili ya Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi. Aidha, ofisi imepanga kutumia jumla ya TZS 1,210,000,000 kupitia fungu 44 kwa kazi za maendeleo. Uchambuzi zaidi unapatikana katika kiambatanisho nambari 7 hadi 9.

Mhe. Mwenyekiti, hotuba hii na viambatisho vyake vinapatikana katika tovuti ya Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora Zanzibar ambayo ni www.utumishi-utawalabora.go.tz

Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

Mhe. Ussi Jecha Simai (Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala): Mhe. Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha muhtasari wa hotuba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ya Baraza la Wawakilishi kuhusu makadirio mapato na matumizi ya Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais Utumishi wa Umma na Utawala Bora ya mwaka 20013/2014

Mhe. Mwenyekiti, naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mtukufu kwa kutujaalia afya njema na uzima wa kuweza kusimama mbele ya Baraza lako tukufu katika kutekeleza majukumu ya kulijenga taifa letu. Aidha napenda kwa moyo wa dhati nikushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii muhimu ya kutoa maoni ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa mwaka wa fedha 2013/2014.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nichukue fursa hii kukushukuru tena kwa kuweza kuiteua Kamati hii ya Katiba na Sheria na kuipatia Wajumbe mahiri na makini ambao wanafanya kazi kwa kujituma. Aidha Kamati katika utendaji wake wa kazi katika wizara zote mbili imepokelewa vizuri na kutokana na hilo, Kamati inapenda kuchukua nafasi hii kuziahidi wizara hizo kuwa Kamati imeridhishwa na mapokezi yao na itaendeleza mashirikiano hayo kwa muda wote wa uhai wa Kamati. Aidha nisiwe mkosefu wa shukurani kwa kutowashukuru wajumbe wa Kamati hii kwanza kwa kunipa imani yao ya kunichagua kuwa Mwenyekiti wa Kamati hii yenye majukumu muhimu katika nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, naamini kuwa Kamati yetu hii ina wajumbe wote wenye uwezo unaolingana, upeo na uzoefu katika ngazi mbali mbali za uongozi, hivyo nategemea kupata mengi ya kujifunza kutoka kwao na kuendeleza mashirikiano mazuri ya kazi ambayo imeanza tokea tulipoanza kazi zetu kwenye kamati hii. Nawashukuru sana.

Mhe. Mwenyekiti, shukurani hizo pekee hazitatosha iwapo sitowataja wajumbe wa Kamati hii kwa majina yao kama ifuatavyo:

1.	Mhe. Ussi Jecha SImai	Mwenyekiti
2.	Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Makamo Mwenyekiti
3.	Mhe. Wanu Hafidh Ameir	Mjumbe
4.	Mhe. Nassor Salim Ali	Mjumbe
5.	Mhe. Mansoor Yussuf Himid	Mjumbe
6.	Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Mjumbe
7.	Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Mjumbe
8.	Ndg. Aziza Wazir Kheir	Katibu
9.	Ndg. Khamis Hamad Haji	Katibu

Mhe. Mwenyekiti, Wizara ya Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora ndiyo kiungo cha utendaji kazi wa serikali nzima ambao unategemea zaidi nguvu kazi ya wataalamu katika kada mbali mbali za utumishi wa umma.

Mhe. Mwenyekiti, watumishi wa umma ndiyo daraja la huduma za serikali kuwafikia wananchi wetu, huduma ambazo zinatokana na mipango, mikakati na vipaumbele tunavyovipanga na kuamua katika chombo hiki. Kazi kubwa ya watumishi wa umma ni kuhakikisha kuwa wanatumia utaalamu na ujuzi wao kuisaidia serikali kufikisha huduma hizo kwa wananchi kwa ufanisi.

Idara ya Mipango, Sera na Utafiti

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majukumu mengine ya msingi, kazi kubwa ya idara hii katika mwaka huu wa fedha ni kuandaa sera ya malipo ya mishahara, sera ya uhifadhi wa kumbukumbu na nyaraka na kuandaa mpango mkakati wa utekelezaji wa sera ya usafiri wa watumishi wa umma.

Mhe. Mwenyekiti, mpango wa malipo ya mishahara kwa hivi ulivyo bado haujakaa vizuri. Kamati yangu inaishauri wizara kuharakisha utengenezaji wa sera ya malipo ya mishahara kwa haraka ili kurekebisha dosari zinazoonekana wazi katika utaratibu usiokuwa wa uwiano wa malipo ya watumishi wa umma wa fani mbali mbali. Kamati yangu imekuwa shahidi

baada ya kutembelea baadhi ya taasisi zilizo chini ya kamati hii, kukimbiwa na wataalamu wa fani adimu kutokana na mishahara midogo isiyolingana na utaalamu wa fani walionao na hasa ikilinganishwa na taasisi nyengine za umma na binafsi ambapo wataalamu hao wanakwenda katika taasisi nyengine ambazo wanalipwa vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, kamati imekuta taasisi moja ya umma ambayo imekimbiwa na wataalamu wake hadi kufikia kubakia bosi wa taasisi hiyo peke yake, mwelekeo huu sio mzuri kwani fedha nyingi za walipa kodi zinatumika kuwatayarisha wataalamu hawa halafu tija yake haionekani kwa kushindwa kutumika serikalini.

Mhe. Mwenyekiti, mkakati wa utekelezaji wa sera ya *e-Government* unahitaji umakini mkubwa. Kamati yangu imepata fursa ya kutembelea miundombinu ya taarifa za serikali mtandao na kugundua kuwa ipo haja ya kutolea taaluma ya kutosha kuwezesha mpango huo kuleta tija inayokusudiwa.

Mhe. Mwenyekiti, malengo makubwa ya huduma za serikali mtandao ni kumsaidia mwananchi kupunguza gharama za upataji wa huduma na kuleta unafuu wa maisha ya mwananchi huyo. Kamati yangu inapendekeza fungu la kutosha la fedha liwekwe na kampeni kubwa ya taaluma ifanyike kuwafahamisha wananchi ni vipi wanaweza kutumia huduma za kimtandao na huduma za aina gani kupitia mtandao watarajie zitapatikana.

Mhe. Mwenyekiti, sambamba na hilo, kamati inashauri kuwa wizara zote za serikali zianze kufanya matayarisho mapema sana ya huduma ambazo zitapatikana kwa njia ya mtandao na kutoa taaluma kwa wananchi juu ya upatikanaji wa huduma hizo kupitia mtandao. Mpango huu utasaidia wananchi kuuelewa utaratibu huo mapema na hatimaye kurahisisha upatikanaji wa huduma za serikali.

Mhe. Mwenyekiti, kamati inaikumbusha serikali kujitayarisha vya kutosha kwenye matumizi ya utoaji wa huduma zake kupitia mtandao, kwani wataalamu wa *ICT/IT* watahitajika ambao nilitangulia kusema kuwa wamekuwa adimu kutokana na mishahara midogo wanayolipwa. Kamati yangu inatoa rai kwa serikali kurekebisha maslahi ya wataalamu kwa vile tunategemea wawepo muda wote kuendesha huduma za kimtandao ambazo zinatakiwa ziwe endelevu.

Idara ya Uendeshaji na Utumishi

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha unaomalizika, Idara hii ilikadiriwa kutumia kiasi cha Tsh. 134,974,900/= kati ya hizo shilingi milioni mia tisa na

sabini na nne laki tisa na sabini na nne elfu na mia tisa kwa kazi za kawaida na shilingi milioni sitini kwa kazi za maendeleo ambapo hadi kufikia mwezi Machi, 2013, fedha zilizotumika ni shilingi milioni arubaini na moja laki sita elfu arubaini na nne mia tisa na tatu, kutokana na fedha hizo kuwa pungufu kamati inataka kujua fedha hizo nyengine zimetumika vipi. Tunaomba tupatiwe ufafanuzi.

Kazi kubwa muhimu iliyopangiwa idara kwa mwaka huo wa fedha ni kufanya maandalizi ya ujenzi wa ofisi mpya ya Wizara ya Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora ambayo imepangwa kujengwa kwenye eneo la Mazizini.

Mhe. Mwenyekiti, makadirio ya mwaka huu wa fedha kwa idara hii ni Tsh.886,548,000/= ambazo pamoja na kutelekeza majukumu mengine ya kiutawala, fedha hizo hizo zinategemewa zitumike katika usimamizi wa ujenzi wa jengo jipya la ofisi mpya ya wizara. Mhe. Mwenyekiti, kamati yangu inapendekeza kwa serikali kuwa, ingawa fedha hizo zilizokadiriwa zipatikane kwa kiwango hicho ili shughuli za usimamizi wa ujenzi wa jengo jipya na utawala ziende vizuri, ushauri huu tunautoa kutokana na fedha zilizokadiriwa katika mwaka wa fedha unaomalizika zilikuwa ni kidogo na hazikupatikana kama zilivyokadiriwa.

Idara ya Mipango na Raslimali Watu

Mhe. Mwenyekiti, suala kubwa ambalo kamati yangu inataka kusisitiza hapa ni maadili ya watumishi wa umma. Ingawa tunapiga kelele hapa maslahi ya watumishi wa umma yaimarishwe bado kuna tatizo la kuporomoka kwa kasi maadili ya utumishi wa umma hasa katika sekta zinazohusika moja kwa moja na huduma kwa wananchi.

Mhe. Mwenyekiti, baadhi ya vipaumbele na mipango ya utekelezaji tunayoipanga na kuamua katika chombo hiki haitekelezeki siyo kwa sababu ya ufinyu wa bajeti peke yake, bali mengine yanakwamishwa kutokana na utendaji kazi ulio chini ya kiwango na kutojali kwa baadhi ya watumishi wa umma katika utekelezaji wa majukumu yao ya msingi.

Mhe. Mwenyekiti, uporomokaji huu wa maadili kwa baadhi ya watumishi wa serikali umechangiwa sana na mifumo yetu mibovu ya uajiri huko nyuma ambayo haikuweka mkazo wa mtu anajua nini bali anamjua nani ili apate kazi. Kamati inashauri Wizara kupitia bajeti ya mwaka huu kufanya kampeni maalumu na kuchukua hatua za lazima inapobidi kwa mujibu wa sheria, kuwashughulikia watumishi wa umma wasiozingatia maadili ya utumishi.

Idara ya Miundo ya Taasisi, Utumishi na Maslahi ya Watumishi

Mhe. Mwenyekiti, bado utekelezaji wa miundo ya taasisi za umma haujaonesha mabadiliko makubwa. Hali hii inatokana na kutokuwepo kwa mwongozo wa kupima na kutathmini viashiria vya utendaji kazi kwa watumishi wetu yaani *(key performance indicators)*.

Mhe. Mwenyekiti, huu sio wakati tena wa kuwa na watumishi ambao tokea wanaingia kazini asubuhi mpaka wanatoka hawana kazi ya kufanya. Kamati yangu inapendekeza kuwa ili utekelezaji wa mipango ya kibajeti tunayoiidhinisha hapa kwa fedha za walipa kodi itekelezwe kwa ufanisi lazima kuwepo na mpango unaotekelezeka wa kuweka viashiria vya utendaji kazi kwa kila taasisi ya umma na kusimamiwa muda wote kupima ufanisi wake.

Idara ya Utawala Bora

Mhe. Mwenyekiti, kamati inasubiri kwa hamu kubwa Mswada wa Sheria ya Maadili ya Viongozi ambao hivi sasa upo katika ngazi ya Makatibu Wakuu. Mswada huu ni muhimu kwani katika kuimarisha utawala bora ni vyema iwepo njia ya kuhakikisha kuwa maadili ya viongozi yanachungwa kwa mujibu wa sheria ili wanaoongozwa nao wawe na imani na kufuata maadili mema kama viongozi wao.

Idara ya Nyaraka na Kumbukumbu za Kitaifa

Mhe. Mwenyekiti, kamati yangu inapongeza mikakati na juhudi za wizara kutatua changamoto mbali mbali zinazoikabili Idara hii. Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala inaahidi kushirikiana na Idara hii katika kuhakikisha inafikia malengo ya kuwa na hifadhi ya kisasa ya kumbukumbu na nyaraka inayokwenda na wakati.

Mhe. Mwenyekiti, wito wa kamati yangu kwa idara hii, katika mwaka huu wa fedha ni kuitaka ihakikishe inatekeleza malengo waliyojipangia, ikiwa ni pamoja na azma yake ya kufanya ukaguzi wa kumbukumbu na nyaraka katika taasisi za umma pamoja na kushauri na kuongoza mfumo wa uwekaji kumbukumbu katika taasisi hizo za umma.

Kamisheni ya Utumishi

Mhe. Mwenyekiti, kumekuwa na malalamiko ya baadhi ya taasisi za umma kuhusu mwenendo wa Kamisheni kwa kuchelewesha miundo ya utumishi ya taasisi hizo. Mfano mzuri ni muundo wa utumishi wa Baraza la Wawakilishi

ambao umechukua karibu mwaka mzima kupitishwa na hata hivyo bado taratibu nyengine hazijakamilika. Pamoja na kuwa jambo hili limezungumzwa katika mijadala mbali mbali lakini hadi sasa muafaka haujapatikana, kutokana na hali hiyo tunaitaka serikali kuharakisha suala hili la muundo wa utumishi wa Baraza la Wawakilishi na mamlaka kamili kama ilivyo katika Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984.

Mhe. Mwenyekiti, kamati hairidhishwi na hali ya kutokuwepo ushirikiano wa kuridhisha, hali inayosababishwa na baadhi ya watendaji wa juu wa Kamisheni pamoja na kutotumia lugha nzuri wakati wa majadiliano na taasisi nyengine za serikali kuhusu upitishwaji wa miundo ya utumishi.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa Kamisheni ni chombo cha serikali na taasisi inazozihudumia nazo ni za serikali ni vyema kukawa na maelewano mazuri, lugha za kiungwana na hatimaye kuafikiana na taasisi hizo bila ya kupitia mizunguko mingi ambayo ndiyo inayoleta malalamiko na kuvutana kusikokuwa na tija.

Tume ya Utumishi Serikalini

Mhe. Mwenyekiti, **c**hangamoto zinazoikabili tume hii zimeonekana kushughulikiwa katika bajeti ya mwaka huu, changamoto hizo ni kama vile uhaba wa wafanyakazi na maslahi ya wajumbe wa tume ambapo fedha zimetengwa kwa ajili hiyo. Kamati inapongeza hatua hiyo ya wizara na inaomba iendelee kwa taasisi nyengine.

Chuo cha Uwatala wa Umma

Mhe. Mwenyekiti, kamati inategemea kupata muda wa kutembelea chuo hiki hapo baadae wakati kazi za kamati zitakapoanza mwezi wa Septemba ili kuona kama ruzuku ya Tsh. 600 milioni zilizokadiriwa katika mwaka huu wa fedha zimepatikana na kutosheleza katika kutekeleza majukumu yao. Kamati inaahidi kulisimamia hilo wakati ukifika panapo majaaliwa.

Aidha kamati inaikumbusha serikali kulizingatia suala la kufanya *harmonization* ya mishahara ya walimu wa chuo hiki ambapo hadi hivi sasa walimu hawa wanalipwa mishahara ya walimu wa skuli za kawaida. Suala hili halikubaliki kutokana na walimu wa vyuo vyengine wenye sifa sawa na walimu wa Chuo cha Utawala wa Umma kulipwa mishahara mikubwa, hivyo kamati inaitaka serikali kulizingatia hilo hasa ikizingatiwa kuwa suala hili ni baya kwa mustakbali wa wafanyakazi hawa wakati wa kustaafu.

Mamlaka ya Kuzuiya na Kupambana na Rushwa

Mhe. Mwenyekiti, mamlaka hii ni mpya ambayo imeundwa kwa mujibu wa Sheria Na.1/2012. Sote tunakumbuka kuwa Sheria ya kuunda Mamlaka hii ilipitishwa kwa kishindo hapa Barazani, kukiwa na matumaini makubwa ya uwepo wake kusaidia kukabiliana na vitendo vya rushwa na uhujumu uchumi vilivyokithiri nchini mwetu.

Mhe. Mwenyekiti, kamati inaipongeza nia njema ya serikali yetu kuunda chombo hiki. Aidha, kamati inapongeza hatua za kuijenga na kuiimarisha mamlaka kwa kuanza kuipa fungu lake la bajeti mbali na kuonesha kuwa kuna dhamira ya kweli ya kuwezesha mamlaka hii kufanyakazi zake kwa uhuru.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na mwanzo mzuri wa chombo hiki, kuna changamoto zimeshaanza kujitokeza ambazo zimeanza kukizana na ile dhamira njema ya kuanzishwa chombo hiki, nayo ni viwango vidogo sana vya mishahara vilivyowekwa kulipwa watumishi wa mamlaka hii.

Mhe. Mwenyekiti, kamati yangu imetembelea mamlaka na kuonana na watendaji wake wachache waliopo, akiwemo Mkurugenzi Mkuu ambaye yupo tayari kabisa kubeba jukumu hili zito. Kamati imeona anahitaji kuungwa mkono kwa kila hatua ya kuimarisha chombo hiki ili kianze kazi zake vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, viwango vya mishahara vinavyokusudiwa kulipwa watendaji wa mamlaka hii ni kama vile wanavyolipwa watumishi wengine wa kawaida wa serikali. Kwa maumbilie ya utumishi wa vyombo kama hivi duniani huu ni mzaha unaoonekana kupingana na ile dhamira na nia njema ya serikali yetu kuunda chombo hiki. Aidha, ni kuwavunja moyo watendaji wetu waliopewa jukumu la kuihuisha mamlaka hii.

Mhe. Mwenyekiti, majukumu mazito iliyopewa Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi hayalingani na viwango hivyo vya mishahara walivyopangiwa. Mhe. Mwenyekiti, haiwezekana hata kidogo mfanyakazi wa chombo hiki alipwe mshahara sawa na watumishi wengine wa serikali halafu mtu huyu huyu anakabidhiwa jukumu la kufanya uchunguzi wa rushwa au uhujumu uchumi yenye thamani ya mamilioni ya fedha, tukitegemea mfanyakazi huyu awe muadilifu katika kutekeleza wajibu wake huo, hii ni ngumu Mhe. Mwenyekiti. Sasa itakuwa badala ya kuunda Mamlaka ya Kupambana na Rushwa itakuwa kinyume chake kuwa Mamlaka ya Kuendeleza Rushwa, maana watendaji hawa watakuwa majaribuni siku zote.

Mhe. Mwenyekiti, kamati yangu bado haijaridhishwa na hali hii na inapendekeza hatua za haraka zichukuliwe na serikali kukaa tena na uongozi

wa mamlaka kujadiliana angalau kwa hatua ya awali viwango vipya vya mishahara inayolingana na kazi hii hata kama vitaanza kulipwa kwa awamu.

HITIMISHO

Mhe. Mwenyekiti, mwisho naomba tena kuchukua nafasi hii kukushukuru tena kwa kunipa fursa hii ya kuwasilisha hotuba ya kamati ya Katiba, Sheria na Utawala. Aidha niwashukuru wajumbe wako kwa utulivu wao waliouonesha wakati nawasilisha hotuba hii.

Mhe. Mwenyekiti, nawaomba wajumbe wako waichangie bajeti hii, watoe mapendekezo yao panapohitajika na hatimaye kuipitisha baada ya kuafikiana kwa hoja mbali mbali watakazoibua wakati wa mjadala.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwasilisha, naunga mkono hoja.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe kabla hatujamwita Mwenyekiti wa *PAC* kuna maelekezo kwamba bajeti hii itachangiwa baina ya leo na kesho tutafanya majumuisho. Kwa hivyo ningeliwaomba Wajumbe mjipange vizuri na *points* zenu ili kila mmoja asirudie rudie.

Mhe. Fatma Mbarouk Said (Kny: Mwenyekiti wa Kamati ya *P.A.C*): Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa fursa hii ya kusoma hotuba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali na Mashirika *(P.A.C)* kuhusiana na bajeti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, kwa mwaka wa fedha 2013/2014.

Mhe. Mwenyekiti, nianze hotuba yangu kwa kufanya nukuu takatifu ya Suratul Ahzab, aya ya 35 ambapo Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema:-

Suratul Ahzab, aya ya 35	"Na wale wanaomtaja na kumkumbuka Mwenyezi Mungu kwa wingi, wakiwa ni (Waisilamu) wanaume na wanawake, kwa hakika, Mwenyezi Mungu amewaandalia msamaha na malipo makubwa"

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa sisi sote tunahitaji msamaha wa Mwenyezi Mungu na malipo mema ya duniani na akhera, ni vyema tukaendelea kumtaja na kumkumbuka yeye na hivyo, na mimi nachukua fursa hii kumkumbuka kwa kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia neema ya uzima wa afya na naendelea kumuomba aniwezeshe, pamoja na Wajumbe wote wa Baraza hili kutekeleza majukumu yetu kwa ikhilasi, uadilifu na usahihi.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati ya *P.A.C,* ni moja kati ya Kamati za Kudumu za Baraza la Wawakilishi. Historia ya Baraza hili tokea kuanzishwa kwake mwaka 1980, inathibitisha kwamba kamati hii imeanza kuundwa mwaka huo na tofauti na kamati nyingi za Baraza, Kamati hii haijawahi kufutwa katika historia ya Baraza hili tukufu, tokea mwaka huo wa kuanzishwa kwake na inaendelea kuitwa kwa jina hilo hilo la asili ambalo ni "Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali na Mashirika, (*Public Accounts Committee)*

Heshima hii ni kubwa mno ambayo sio tu, kamati hii inajivunia lakini pia Waheshimiwa Wajumbe wako wa Baraza hili, kupitia kamati zao mbali mbali na wasiokuwa Wajumbe wa kamati, wanaendelea kwa karibu mno kushirikiana na kamati hii, katika kuisaidia kutekeleza majukumu yake na katika uhai wake, Kamati hii imeendelea kujivunia heshima na kuaminiwa na hata wananchi wa Zanzibar kwamba inatekeleza vyema majukumu inayopangiwa.

Mhe. Mwenyekiti, pongezi zinastahiki kwa Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza hili ambao uwezo wao unazidi kuimarika siku hadi siku, wiki hata wiki, mwezi na mwezi, na hata mwaka mmoja kwa mwengine, kutokana na umakini wao wa kuchunguza fedha za umma, wakiwa katika Baraza, wakiwa katika Kamati zao mbali mbali za kudumu lakini pia umakini wao huongezeka mara dufu, pale wanapopangiwa kuitumikia Kamati hii ya *P.A.C.*

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na Kamati ya *P.A.C* kuanzishwa tokea uhai wa Baraza hili, kazi za kamati hii zinatekelezwa katika mnasaba wa kazi za Kamati za Kudumu za kusimamia serikali kwa mnasaba wa maelekezo na muongozo wa Kanuni za Baraza, na kwa muda wote kazi ya Kamati ya *P.A.C* ya kupitia bajeti ya serikali ama Wizara au Taasisi yoyote ya Umma, iliachwa kando na kutowahi kutekelezwa.

Tunapenda kwanza kuchukua fursa hii, kukushukuru wewe Mhe. Mwenyekiti, kwa kukubali kwa mara ya kwanza, kamati hii kuipitia bajeti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, ambapo, mazoea yetu ya kuiona Kamati ya *P.A.C* haina bajeti ya kuichambua na kutoa maoni yake husika, yametufanya sote kwa muda wote huo kuamini kwamba kazi za kupitia bajeti ya Afisi hii ya Mdhibiti, zifanywe na Kamati inayohusika na Wizara inayosimamia Afisi hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, hatuna budi tukiri kwamba miongoni mwa mambo magumu sana kwa mtu yeyote na zaidi kwa mkusanyiko wa watu, ikiwa ni pamoja na serikali ama hata kamati zetu za Baraza, kuacha kufanya jambo lililozoeleka. Lakini huwa gumu zaidi, pale linapotakiwa kuachwa kufanywa

kama lilivyozoeleka na likatakiwa lifanywe kama sheria inavyoelekeza. Tunapenda tulikushukuru sana Baraza la Wawakilishi pamoja na serikali, kwa kuitikia kwa vitendo kauli na wito wa Mhe. Rais wa Zanzibar, wa kuacha kufanya kazi kwa mazoea na badala yake tufanye kazi zetu kwa mujibu wa sheria.

Mhe. Mwenyekiti, shukurani hizi zimuendee Mhe. Waziri wa Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora, kwa kukubali kwake kukaa na Kamati ya *P.A.C* kwa mara ya kwanza, kwa lengo la kuipatia bajeti ya Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu na kuitikia wito wa Kamati. Lakini bila ya kusahau kumpongeza na kumshukuru Mdhibiti Mkuu wa Hesabu, kwa kukubali nae kutekeleza matakwa ya sheria na hatimae Kamati ya *P.A.C,* ikaweza kuipitia bajeti yake.

Mhe. Mwenyekiti, Sheria ya Fedha za Umma, Namba 12 ya mwaka 2005, imetoa maelekezo kupitia kifungu cha 35 kwamba:-

> "35(1) Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu, kwa kuzingatia mwaka wa fedha wa (kuanza kwa Afisi yake kwa mujibu wa Sheria hii) na kwa kila mwaka wa fedha unaofuata baadae, atatayarisha na kuwasilisha kwa Waziri (anayehusika na masuala ya Mdhibiti ambapo kwa sasa ni Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora), makisio ya mapato na matumizi ya Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu ambaye Waziri husika baada ya kukabidhiwa ataiwasilisha kwa Baraza la Wawakilishi la Zanzibar".

1) Kwa kuzingatia makisio yaliyowasilishwa kwake kwa mnasaba wa kijifungu cha (1) cha kifungu hiki, Baraza la Wawakilishi litazingatia Ushauri wa Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali na Mashirika na Ushauri wa Waziri anayehusika na masuala ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuzingatia maelekezo ya kifungu hicho cha 35 cha Sheria ya Fedha za Umma, hakuna ubishi wowote kwamba Kamati ya *P.A.C* ina dhima kubwa ya kuipitisha bajeti ya Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu, ili Wajumbe wa Kamati hii kupitia Mwenyekiti wao aweze kuwasilisha maoni ya Kamati wakati wa kuwasilishwa na kupitishwa kwa bajeti hiyo, na Baraza lako tukufu liweze kupitisha bajeti hiyo kwa kuzingatia maoni ya Kamati ya *P.A.C* na maoni ya Mhe. Waziri anayehusika na Afisi hii ya Mdhibiti.

Mhe. Mwenyekiti, ni vyema pia tukafanya rejea ya Kanuni ya 96(1) ya Kanuni za Baraza la Wawakilishi, Toleo la 2012, inayozungumzia Makadirio ya Matumizi ya Wizara kama ifuatavyo:

> "96(1) Kabla ya Kamati ya Matumizi haijashughulikia fungu lolote la Makadirio ya Matumizi, fungu hilo kwanza lipelekwa kwenye Kamati inayohusika litafakariwe na halitaletwa kwenye Kamati ya Matumizi ya Baraza zima mpaka Mwenyekiti wa Kamati iliyopewa kazi ya kufikiria fungu hilo atakapomwarifu Spika kwamba Kamati yake imemaliza kulifikiria fungu hilo".

Mhe. Mwenyekiti, kanuni hii inatukumbusha kwamba Kamati za Kudumu za Baraza la Wawakilishi, zina jukumu la awali la kuyapitia na kuyachambua mafungu ya Makadirio ya Matumizi ya kila Wizara, kabla Makadirio hayo ya makusanyo na Matumizi hayajashughulikiwa na Baraza hili, kupitia Kamati yake ya Matumizi.

Katika kulitafakari hili, kuna vitu muhimu vya kuzingatia wakati tunapofanya marejeo ya majukumu la Kamati ya *P.A.C* katika kuichambua na kutoa maoni yake juu ya bajeti ya Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu. Kwanza maana ya 'Fungu' na la pili ni Kamati gani iliyotakiwa kushughulikia fungu ama mafungu hayo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mujibu wa kifungu cha 2 cha Kanuni za Fedha za Umma ya mwaka 2005, imeeleza maana ya fungu kama ifuatavyo:

> "2 Ni mkusanyiko wa Makisio ya Matumizi ambapo makisio yake yamefanywa (yamekubaliwa) na Sheria ya Matumizi au Sheria ya Matumizi ya Nyongeza"

Mhe. Mwenyekiti, sote tunafahamu kwamba Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu inapitishwa bajeti yake kwa kuzingatia fungu la 11 linalopatikana katika vitabu vyetu vya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Kazi za Kawaida na Maendeleo kwa kila mwaka. Sasa suala linalobakia ni Kamati gani ya Kudumu ya Baraza la Wawakilishi inapaswa kuishughulikia bajeti hiyo?

Mhe. Mwenyekiti, kwa kawaida imezoeleka kuwa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala ya Baraza la Wawakilishi ndiyo inayoshughulikia bajeti ya Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa sababu Kamati hii ndiyo inayoshughulikia na kusimamia Wizara inayoisimamia Afisi hii,

ambapo kwa awamu nyingi za Serikali hapa Zanzibar pamoja na kubadilishwa kwa Wizara, lakini mara nyingi huangukia katika usimamizi wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala.

Lakini pia tufahamu kwamba Kamati ya Kuchunguza na Kudhibiti Hesabu za Serikali na Mashirika, nayo inasimamia Wizara zote za Serikali, Serikali za Mitaa na Mabaraza ya Miji na hata mashirika yote. Na ni wazi kwamba Kamati ya *P.A.C* pia inahusika na bajeti ya fungu la Afisi ya Mdhibiti kwa sababu inaisimamia Wizara inayohusika na Afisi hii, lakini pia ni Kamati hii inayoisimamia hata Afisi yenyewe ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu katika kutekeleza majukumu yake ya kila siku. Kwa maana hiyo kwa kuzingatia masharti ya Sheria ya Fedha ya mwaka 2005 na kwa makusudio ya Kanuni za Baraza, Kamati ya *P.A.C* ina nafasi zaidi ya kushughulikia makadirio ya mapato ya Afisi hii ya Mdhibiti.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kutoa uchanganuzi huo ambao ni muhimu kwa Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako, kwa kuzingatia kwamba kazi hii ni mpya kwa Kamati na haijazoeleka, na hivyo bila ya kutoa ufafanuzi huo kungeliwafanya Waheshimiwa kujiuliza masuala mengi yasiyo na majibu. Mhe. Mwenyekiti, ni vyema sasa tukafanya uchanganuzi wa bajeti ya Afisi ya Mdhibiti ambayo imegawika katika sehemu kuu mbili; Sehemu ya mapato na sehemu ya matumizi ya kazi za kawaida.

KUHUSIANA NA MAKUSANYO YA MWAKA WA FEDHA 2013/2014:

Mhe. Mwenyekiti, Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu kwa mwaka 2013/2014 imekadiriwa kukusanya Tsh. 15,000,000/= zinazotarajiwa kukusanywa kupitia ada ya ukaguzi. Mhe. Mwenyekiti, fedha hizo sio nyingi sana lakini uchache wake unatokana na kutegemea chanzo kimoja tu, nacho ni ada ya ukaguzi (*Audit Fee*).

Aidha, pamoja na kwamba kiwango hicho kimepanda ukilinganisha na cha mwaka uliopita ambapo ilikuwa ni Tsh.10,000,000/= pekee, Kamati inaitaka Afisi hii kuwa fanisi katika ukusanyaji wake, ili makusanyo hayo yaweze kuongezeka mwaka hadi mwaka. Huku Kamati ikiendelea kusisitiza haja ya kuongezwa kwa vyanzo vya makusanyo ili mapato yake yaweze, sio tu kuisaidia Serikali lakini matunda yake na manufaa, yawaenee wananchi wote wa Zanzibar, kwani wao ndio walengwa wa bajeti za Serikali.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati yetu inasisitiza kuongezwa kwa mapato kwa sababu tuna hakika kuwa inawezekana, kwani kwa mwaka wa fedha 2011/2012, Afisi iliweza kukusanya Tsh.18,200,000/-. ambapo juhudi nyingi

zikitumika, mapato hayo pamoja na uchache wake, yataweza kuongezeka mwaka hadi mwaka.

KUHUSIANA NA MATUMIZI YA KAZI ZA KAWAIDA KWA MWAKA WA FEDHA 2013/2014:

Mhe. Mwenyekiti, Kamati iliarifiwa kwamba makadirio ya fedha zitakazotumika kwa kifungu 0201 (Utawala Unguja) ni jumla ya shilingi 1,339,477,000/= kwa Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali Zanzibar. Pamoja na maelezo yaliyotolewa, Kamati ilihitaji ufafanuzi wa ziada kwa baadhi ya kasma ili ipate kujiridhisha.

Mhe. Mwenyekiti, aidha, kamati ilihitaji ufafanuzi kuhusiana na suala zima la kushuka kwa makadirio ya kasma 211101 (Mishahara ya waajiriwa wa kudumu) kutoka shilingi 410,529,000/= kwa mwaka wa fedha 2012/2013 hadi shilingi 395,058,000/= kwa mwaka 2013/2014 na kupatiwa maelezo ya kwamba fedha hizo zimepungua kutokana na kupungua kwa idadi ya watendaji katika Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu kulikotokana na kustaafu na kufariki kwa baadhi ya watendaji.

Hoja hii pamoja na uzuri wake, inatanzwa na hoja ya haja ya uajiri mpya kwa wataalamu wanaohitajika kwa fursa ya kujaza nafasi tupu zilizoachwa na hao waliostaafu ama waliofariki. Suala la kuajiri wafanyakazi wapya kwa Afisi ya Mdhibiti linahitajika na Kamati yetu imekuwa ikilielezea kwa Serikali, kila muda unaporuhusu. Hivyo, bado Kamati inachukua nafasi hii kuikumbusha Serikali juu ya haja ya Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu iweze kuajiri wafanyakazi inaowahitaji, watakaoweza kutekeleza majukumu ya kitaalamu watakayopangiwa.

Mhe. Mwenyekiti, sambamba na hilo, kamati inatoa wito kwa Serikali, kupitia Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora kuitupia jicho la huruma Ofisi ya Mdhibiti kwa kuwapatia kibali cha kuajiri hususan wataalamu wa fani mbali mbali zinazohitaji ukaguzi wa thamani halisi ya fedha (*Value for Money Audit);* Ukaguzi wa Kimazingira (*Environmental Audit*), Ukaguzi wa Kompyuta (*Computerised Audit*) na kaguzi nyenginezo, ili kufanya shughuli za ukaguzi ziwe za kitaalamu, mbali na ule ukaguzi uliozoeleka wa fedha pekee (*financial audit*).

Aidha, idadi ndogo ya wataalamu waliopo ofisini hapo inawafanya waelemewe na majukumu na hivyo iko haja ya kuongeza idadi yao kwa nia ya kukuza ufanisi wa shughuli zao za kila siku. Ni vyema Serikali ikatumia fedha zaidi katika kuajiri wataalamu kwa nia ya kuokoa mabilioni ya fedha

yanayopotea kutokana na ubadhirifu, udhaifu katika mikataba pamoja na viwango duni vya kazi hasa katika sekta ya ujenzi.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na maelezo yaliyotolewa mbele ya Kamati kuwa marekebisho ya mishahara kwa watendaji wote wa taasisi za serikali yanasimamiwa na Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, kupitia Idara ya Bajeti, Kamati ilihitaji ufafanuzi kuhusiana na suala la kukwama kwa "*scheme of services*" ya Ofisi ya Mdhibiti kwa kipindi kirefu sasa jambo ambalo linawatia unyonge watendaji wa Ofisi hii kwa kuzingatia uzito wa kazi zao na thamani ya miradi wanayoikagua. Ni dhahiri kuwa kuwajengea maslahi bora watendaji wa Ofisi hii kutasaidia katika kuongeza ari ya utendaji kwa uadilifu zaidi na kuifanya Serikali kuweza kunusuru fedha nyingi kwa matumizi mengine ya maendeleo.

Kwa kuzingatia maelekezo ya Serikali ya kufanya mapitio ya "*scheme of services*" za taasisi zake zote na kuziweka katika viwango vinavyowiana, Kamati inaitaka SMZ kufanya uwiano huo kwa uangalifu mkubwa na kuzingatia ukweli kwamba watendaji wa taasisi hizo wanafanya kazi katika mazingira yanayotofautiana.

Aidha, Kamati hii inaendelea kuitaka Serikali kuongeza maslahi ya wafanyakazi wa Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu, kwani kazi wanazozifanya ni nzito na zinahitaji kiwango kikubwa cha uaminifu. Mhe. Mwenyekiti, mahali muhimu pa kuongeza maslahi ya wafanyakazi hao, ni hapa panapohusiana na mishahara ya watendaji wa afisi hii, jambo ambalo linaendelea kuisikitisha kamati, kwa kuzingatia ukweli kwamba bajeti hiyo imekuwa ikishuka mwaka hadi mwaka.

Mhe. Mwenyekiti, kasma namba 211110 ya kifungu cha 0201 cha Utawala Unguja, imezungumzia posho maalum (*Special Allowances)*, ambalo tokea kuanza kwa Baraza hili, posho hilo limekuwa likijadiliwa sana chini ya usimamizi mahiri wa Mwakilishi msomi, Mhe. Ismail Jussa Ladhu. Tatizo kubwa alilonalo Mhe. Jussa pamoja na Wajumbe wengine, ni kukosekana kwa uchanganuzi wa wazi wa posho hilo. Si kwamba Kamati inapinga kuwepo kwake lakini hata nasi wakati tunapitia bajeti hiyo ya Mdhibiti, hakukuwa na maandishi yoyote ya kutoa uchambuzi wake. Hivyo ile haja ya Serikali kujipanga katika kutoa uchanganuzi husika na zaidi kwa kuwa sasa imeshaamuliwa na Baraza kufanywa kwake, kufuatia ahadi ya Serikali yenyewe, Kamati inahimiza kutolewa kwa ufafanuzi wa vigezo vinavyotumika na watendaji wanaohusika kwa mujibu wa nyadhifa zao kupatiwa malipo ya posho maalum na hata posho la baiskeli, ili kuwajengea uwezo Wajumbe wa Baraza hili kupata uelewa mpana zaidi juu ya maposho hayo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2013/2014, Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali imetengewa jumla ya shilingi 100,000,000 kwa ajili ya matengenezo makubwa ya jengo lake huko Pemba ambapo kutokana na hali mbaya ya jengo hilo, Kamati inashauri Serikali kufikiria uwezekano wa kujenga jengo jipya, ukizingatia fedha nyingi za matengenezo zinatolewa kwa kazi hizo. Kwa mfano, mwaka 2012/2013, zilitumika Tsh.23,200,000/- kwa matengenezo madogo na mwaka huu nao ni Tsh. 100,000,000/- ni dhahiri kwamba, gharama za matengenezo zinakuwa kubwa zaidi kuliko ama inalingana na kujenga jengo jipya la Afisi.

Kwa vile program za ujenzi wa Afisi za Serikali ya Mapinduzi Zanzibar iko chini ya Afisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo kupitia, Idara ya Uhakikimali na mitaji ya umma kama ilivyoarifiwa mbele ya Kamati hii, Kamati inaitaka SMZ kutoa kipaumbele maalum kwa ujenzi wa jengo hilo hasa kwa kutilia maanani mazingira yasiyoridhisha yanayowakabili watendaji wa Ofisi hiyo ambayo hayawiani kabisa na hali ya Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu Unguja.

Mhe. Mwenyekiti, kasma namba 263178 iliyo katika kifungu cha 0201 inahusiana na ushauri nasaha *HIV/AIDS*, ambayo imetengewa Tsh.1,500,000/- pekee kwa Afisi ya Mdhibiti Unguja na hata upande wa Pemba imetengewa jumla ya Tsh. 500,000/- pekee. Mhe. Mwenyekiti, Kamati yetu haina pingamizi na kiwango hicho kwa matumizi ya fedha za ushauri nasaha dhidi ya maradhi ya Ukimwi, lakini tunashangaa sana kwa Wizara ama Idara nyengine, kutengewa fedha nyingi zisizo ushahidi wa kudhibitika na kuchungika.

Kwa mfano, ukichukua Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais pekee, Afisi Kuu Pemba ilitengewa Tsh. 2,729,000 huku Idara ya Mipango, Sera na Utafiti ilitengewa Tsh. 52,500,000/-. Mhe. Mwenyekiti, Kamati yetu kwa muda mrefu imekuwa inafadhaishwa na matumizi mabaya ya fedha za Ukimwi katika Wizara na Taasisi mbali mbali za Serikali. Fedha za Ukimwi zimekuwa kama ‘SHAMBA LA BIBI’ kwamba kila mtu anaingia na kuvuna anavyotaka. Na kinachoishangaza Kamati ni ukweli kwamba fedha hizo zinaidhinishwa na kutolewa kwa kila mwaka, huku matumizi yake hayaonekani wazi.

Mhe. Mwenyekiti, umefika muda sasa wa kukaguliwa kwa makini fedha hizo kwa kila taasisi inayopewa. Kamati ya *P.A.C* iliyopita ya mwaka 2010-2013, iliwahi kushauriana juu ya suala hilo la haja ya ukaguzi maalum wa fedha za Ukimwi, baada ya kupata mfadhaa mkubwa wa matumizi yake, kufuatia kazi

za Kamati za ukaguzi uliofanyika Tume ya Ukimwi, Wizara ya Afya, baadhi ya vikosi vya SMZ ikiwa ni pamoja na Kikosi cha Valantia na taasisi nyengine za Serikali.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa sasa Baraza lako tukufu limemuagiza Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kufanya ukaguzi maalum wa matumizi ya fedha za Ukimwi baada ya hoja ya Mhe. Ismail Jussa Ladhu ulipoikubali na kueleza kuwa uwezo wa Baraza la Wawakilishi kumuagiza Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu kufanya ukaguzi maalum, wakati kamati ya matumizi ilipokaa na kuanza kupitisha bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais siku ya Jumatano tarehe 26/06/2013 kamati yetu imefurahishwa na maamuzi hayo inaikumbusha Ofisi ya Baraza kuchukua hatua za mapema za kumkumbusha Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu juu ya maamuzi ya Baraza kuhusiana na ukaguzi maalum wa fedha za ukimwi kwa taasisi zote za serikali.

Mhe. Mwenyekiti, Waswahili wanasema ‘Mstahamilivu hula mbivu’. Msemo huu pia unajidhihirisha katika bajeti ya Afisi ya Mdhibiti ambapo kwa mwaka wa tatu sasa wamekuwa wakiomba fedha za ununuzi wa sare, lakini fedha hizo hazijapatikana. Pamoja na Afisi kuomba Tsh. 4,500,000/- kwa mwaka huu wa fedha, bado wana matumaini ya kuingiziwa fedha hizo ambazo matumizi yake sio tu kuwafanya wafanyakazi wawe nadhifu na maridadi wakiwa afisini, lakini pia kutawajengea ushujaa na kujiamini na kuipenda kazi zao.

KUHUSIANA NA MATUMIZI YA KAZI ZA MAENDELEO KWA MWAKA 2013/2014:

Mhe. Mwenyekiti, kwa miaka miwili sasa, yaani mwaka wa fedha 2012/2013 na 2013/2014, Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu, haijatengewa fedha za maendeleo. Suala hili, linaihuzunisha sana Kamati yetu kwani tunaamini kwamba matumizi ya fedha hizi ni ya msingi sana katika kuleta maendeleo na ustawi wa nchi yetu na pia ndio kichocheo cha uwajibikaji na ustawi wa taasisi zetu.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa bado Serikali haijaona haja ya kutenga fedha za maendeleo kwa Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu, Kamati yetu inaitaka Serikali itafakari kwa kina suala hili ili mwaka ujao wa fedha, Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu iweze kutengewa fedha kwa matumizi yake ya maendeleo.

HITIMISHO:

Mhe. Mwenyekiti, jambo la mwisho ambalo ni muhimu kwa kuwepo kwake ni kuendelea kutoa shukurani zangu za dhati kwako kwa namna unavyoisaidia Kamati kutekeleza vyema majukumu yake, na kutoa mashirikiano mazuri kwa kila namna tunavyohitaji. Shukurani hizi pia ziwaendee watendaji wote wa Afisi ya Baraza lako kwa namna moja ama nyengine, wanavyoisaidia Kamati yetu kutekeleza majukumu yake.

Naishukuru tena Serikali kupitia Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora, kwa kukubali kwa mara ya kwanza katika historia ya Baraza, Kamati ya *P.A.C* kuipitia na kuishughulikia bajeti ya Afisi ya Mdhibiti kwa maana fungu Namba 11 linalohusiana na makadirio ya makusanyo na matumizi ya afisi hii kwa mwaka 2013/2014.

Mhe. Mwenyekiti, sasa sina budi kuwashukuru Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako, kwa usikivu wao na utulivu na ninaamini wataijadili ipasavyo bajeti ya Wizara hii, bila ya kusahau fungu la Afisi ya Mdhibiti. Shukurani zangu maalum ziwafikie Wajumbe wa Kamati ya *P.A.C*, kwa kutoa ushirikiano mkubwa kwangu na kuendeleza mapenzi na mshikamano wa kufanya kazi kwa pamoja na naomba sana moyo wao wauendeleze ili malengo ya kuwepo kwa Kamati hii yaweze kufikiwa.

Mhe. Mwenyekiti, naomba sasa niwatambue Wajumbe wa Kamati ya *P.A.C.* ambao ni hawa wafuatao:-

1. Mhe. Omar Ali Shehe -Mwenyekiti.
2. Mhe. Fatma Mbarouk Said -Makamo Mwenyekiti.
3. Mhe. Rufai Said Rufai -Mjumbe
4. Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi -Mjumbe
5. Mhe. Salma Mussa Bilali -Mjumbe
6. Mhe. Mbarouk Wadi Mussa -Mjumbe
7. Mhe. Salim Abdalla Hamad -Mjumbe
8. Mhe. Shamsi Vuai Nahodha -Mjumbe

Mhe. Mwenyekiti, sina budi kuwashukuru makatibu wetu wa Kamati, ambao ni:-

1. Ndg. Asma Ali Kassim; na
2. Ndg. Othman Ali Haji.

Makatibu wetu hawa ndio macho, masikio, pua na hata miguu ya Kamati. Bila ya uwepo wao, Kamati hii haiwezi kufanya kazi kwa ufanisi. Lakini kwa kuzingatia ufanyaji kazi unaohitaji taaluma na fani nyingi za kiuhasibu,

uchumi, fedha, sheria na nyingi nyenginezo, makatibu hawa hutumia elimu zao kwa kiasi cha uwezo wao katika kuisaidia Kamati.
Tunaendelea kuwaomba na kuwanasihi waendelee kuisaidia Kamati, licha ya kupata misuko suko kadhaa ambapo kwa kadri Kamati inavyoongeza wigo wa kufichua maovu, ndipo na wao wanapotizamwa kwa jicho la kuonekana 'wakorofi'.

Mhe. Mwenyekiti, mbali na Baraza lako kuwa na uwezo mkubwa wa kujadili, kuichambua na kuipitisha bajeti ya Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu, pamoja na bajeti nyengine za mawizara, ni vyema sana wanapoendelea na kazi zao nzito, kuangalia pia mambo yafuatayo:-

- Uhusiano uliopo baina ya matumizi yaliyokadiriwa na mategemeo ya kuongezeka kwa ufanisi katika utoaji huduma.
- Uwiano baina ya mishahara iliyokadiriwa na vitendea kazi vilivyopangwa kutumika.
- Namna jamii itakavyofaidika kutokana na utendaji wa Ofisi (na Wizara) kwa mwaka wa fedha 2013/2014 na vipi ilifaidika kutokana na matumizi yaliyofanywa kwa mwaka 2012/2013; na hata kuangalia
- Njia zitakazotumika na Ofisi (na Wizara) katika kufikia ufanisi wa matumizi yanayopendekezwa.

Mhe. Mwenyekiti, sina budi kumalizia hapa ingawa nina mengi ya kusema na yenye faida kwa kadri nnavyopata nafasi ya kuchangia kwa niaba ya Kamati na kwa kadri muda niliopewa unavyotarajia kumalizika, ndipo na mawazo mema, ushauri na maelekezo yanavyozidi kufukuta kichwani mwangu. Ukweli huu pia unadhihirishwa na mshauri na nguli maarufu wa Kiswahili Afrika Mashariki, Bw. Shaaban Robert ambaye hata katika kitabu chake cha mashairi ya mapenzi bora alisema:-

"Yana ajabu maisha,
Yakikaribia kwisha,
Ndipo yanapoamsha,
Fani mashazi mashazi."

Mhe. Mwenyekiti, naunga mkono juu ya upitishwaji wa bajeti ya fungu la 11 la Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, huku hesabu na mafungu mengine ya Wizara hii, nitaunga mkono baada ya kuchangia na kupewa majibu ya kina na fasaha juu ya hoja nitakavyozitoa wakati nitakapopewa tena nafasi ya kuchangia.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kuwasilisha.

Mhe. Makame Mbarouk Mshimba: Bismillahi Rahman Rahim Mhe. Mwenyekiti, nimeanza kwa jina kubwa na hasa leo nina uzito wa Wizara hii ya Utumishi ya Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora, basi nimeona kuwa nianze kwa jina kubwa la Mwenyezi Mungu ili Mwenyezi Mungu anitakabalie haya ambayo ninawaombea wanyonge walioko huko nje wafanyakazi waliokuwa mpaka sasa hivi hawajajijua haki zao zikoje. Kwa hivyo nimeanza kwa jina hilo tukufu kwa kuwa mimi nimeapa kwa kutumia jina la msahafu kwa jina la Mwenyezi Mungu mwenyewe.

Mhe. Mwenyekiti, nitajitahidi sana kusema kwa unyonge sana na kuonesha huzuni zangu kwa hawa waliotutuma huko nje ili tuwasaidie kuwatetea na waone kuwa serikali tunaiambia kwa jitihada zetu zote na wapi sasa wao watachagua kuwa lipi Waheshimiwa tunavyosema kuwa ninakwama wapi watajua leo hii katika bajeti hii.

Mhe. Mwenyekiti, nianze na ukurasa wa 12 katika Idara ya Uendeshaji na Utumishi. Mhe. Mwenyekiti, sisi wanadamu kila mtu ana lugha zake ndani ya nafsi yake na anapokuwa anapotaka kutafsiri jambo au kulizungumza jambo basi mheshimiwa naomba sana tueleweke katika kiswahili ambacho tunazungumzia yale ambayo tunaona sisi waheshimiwa wao kwa sababu sisi tunaona, lakini wengine hawaoni sawa sawa na mchezaji mpira ukiwa uwanjani unakuwa hujioni lakini wa juu ndio anayeona. Kwa hivyo nawaambia sana Waheshimiwa Mawaziri tunapoona sisi wasinune na sisi kwa sababu sisi tuna wajibu wetu na sisi tuliona *message* hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, Idara hii kwa kiswahili cha humu ndani nasema Idara hii naomba kunukuu, "Idara hii ina jukumu la kutoa huduma za utumishi na uendeshaji katika Ofisi ya Rais Utumishi wa Umma na Utawala Bora zikiwemo ajira, maendeleo na utumishi, upandishaji wa vyeo na kufanya tathmini kwa watumishi na kuhakikisha kuwepo kwa watendaji wa kutosha na wenye sifa ambazo za kueleweka". Mhe. Mwenyekiti, hapa ndio ninapoanzia kama nitakubalika na kama kanuni itanilinda, ajira kweli zimetoka nakubaliana na hilo kwenye matangazo na wametafutwa wenye sifa sidhani kama ni kweli wale wote wenye sifa wamepatiwa ni hao, hiyo siwezi kujua lakini nitajua leo.

Mhe. Mwenyekiti, niseme neno ya umu shaka kwa sababu ni kitu ambacho kikawa kina kasoro lazima ukitilie shaka, lakini usiwe na *approved* kusema kuwa hili ni uhakika. Naweza kusema Mhe. Mwenyekiti, na kama tutafanya *evaluation* hasa ya uhakika basi ajira nyingi atakayeshtuka basi na yeye kahusika na suala hilo. Ajira nyingi zimechukuliwa na mawaziri, sisi

Waheshimiwa humu ndani hakuna hata mmoja na aoneshe mmoja tu kwamba yuko Mwakilishi angalau kapeleka wananchi wake na wamefanikiwa, hamna hata mmoja wamenyamaza kimya, wengine wamefunga mikono kama wanataka kusali. Sasa hebu fikiri Mhe. Mwenyekiti, hakuna hata mmoja na kama tutafanya hiyo hesabu katika hao ambao waliotajwa humu kwa mujibu wa kitabu hiki, sidhani kama wamo hao watu ambao wenye sifa hizo waliotakiwa, wewe peleka tu unaambiwa.

Mhe. Mwenyekiti, kifungu hiki mimi sitoridhika nacho kwanza hilo

Nam.1107

IMESAHIHISHWA

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: (Anaendelea) wanavyosema utumishi kuhakikisha kuwepo kwa watendaji, sifa pamoja Idara ya kutoa huduma zote, manunuzi mambo mengine Lakini Mhe. Mwenyekiti, kifungu hichi kinaweza kikasomeka katika kifungu chengine.

Mhe. Mwenyekiti, niende sasa katika Idara ya Utumishi, anasema Idara ina jukumu la kupitia miundo na mifumo ya Wizara na Taasisi za Umma kusimamia kwa mujibu wa sera na sheria zilizopo ili kuleta ufanisi katika utoaji wa huduma, vile vile na kusimamia maslahi ya wafanyakazi na kuendeleza kusimamia mfumo wa malipo ya mishahara.

Mhe. Mwenyekiti, ukiangalia kwa utaalamu wa haraka haraka kifungu kile nilichokisema mwanzo na kuna mambo kidogo yanalingana na yanakubaliana. Mimi ningeona tu kwa usanii wangu wa kujua hili jambo na tafsiri zangu kwa kuwa siku hizi bajeti za karatasi kutumia nyingi tunatumia *cost* ya fedha, basi hili tungejaribu lugha tukaiweka katika kifungu kimoja tu, nayo ingetusaidia ili kutoa muamko mmoja au muonyesho mmoja, kuliko kufanya kutumia, tabu kubwa ambayo iliyokuwa tafsiri yake inazunguka mle mle.

Mhe. Mwenyekiti, wizara hii ndiyo yenye muundo huo wa kutengeneza mishahara. Wenzetu *Mainland* huko wameshaongezwa mishahara na sisi tunaambiwa kuwa wataongezwa wafanyakazi mishahara, lakini kitabu hiki leo nimekesha japo tumepewa dakika chache tu, kwa sababu tunasema tupewe mapema ili tuweze kuchangia vizuri lakini tunapewa buubaa, hapo kwa hapo na sisi tunakwenda hivyo hivyo tunavyoona.

Mhe. Mwenyekiti, mishahara nitathubutu kusema kuwa haijaongezwa na kama imeongezwa basi haijafikia maslahi ya wale walengwa kunufaika na ule mshahara waliopewa. Mhe. Mwenyekiti, sioni kabisa mimi, labda sijavaa

miwani hamna kuonesha hapa kwamba angalau mfanyakazi wa chini anapata mshahara kiasi kadhaa. Mimi sijaridhika kabisa kwa kweli Serikali inasimamia mfumo wa mishahara hiyo na malipo yenyewe kwa wafanyakazi kweli au tunafanya mzaha tu.

Mhe. Mwenyekiti, Mwenyezi Mungu atujaalie iwe salama na inshallah iwe Zanzibar ni njema atakaye na aje kwa jambo lenye kheri na siye, lakini iko siku watatupiga mikwaju wafanyakazi na wao wanachoka, wanajituma katika kujenga nchi yao, wanatutilia fedha hawa wafanyakazi, lakini hatujawapenda. Mimi nasema hatujawapenda kwa sababu kumpenda mfanyakazi ni kumpandishia mshahara wake wenye maslahi uwende na wakati. Mhe. Mwenyekiti, tunawapuuza tena sana tu.

Mhe. Mwenyekiti, hebu tutizame *paragraph* hii ya 29 Idara ya Utawala Bora, panasema nini hapa kwenye Utawala Bora na Mhe. Mwenyekiti, naomba kunukuu kifungu cha 64 hichi.

"Idara hii ina jukumu la kuratibu na kutathmini utekelezaji wa misingi mbali mbali ya utawala bora ikiwa pamoja na kuratibu na kusimamia sera, sheria na kanuni katika kuhakikisha haki za binadamu zinalindwa, maadili ya viongozi wanakuwepo na amani na utulivu".

Mhe. Mwenyekiti, tunatamka wenyewe tunatunga sera wenyewe, tunatekeleza sheria wenyewe, lakini hatimae hatutekelezi. Leo binadamu yumo humu lakini binadamu yule leo kwa kuwa tumevaa Uheshimiwa tunawadhililisha wale. Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli ni suala ambalo la kusikitisha sana, hiyo utawala bora wenyewe naomba Mhe. Waziri na ndio sijui tafsiri kwa sababu mimi ni mtu wa Kinduni na yeye mtu wa Tumbatu, anisaidie lugha, tafsiri hii hebu naomba aje kuniekea sawa ili tuelewane vizuri, utawala bora ukoje katika nchi kwa jamii au binadamu wenyewe.

Mhe. Mwenyekiti, niingie tena kwenye ukurasa wa 30, anasema utekelezaji wa malengo hayo katika utekelezaji wa sera ya utawala bora, Idara ilifanya mikutano mitano katika kikundi kazi cha utawala bora na kutoa mafunzo ya namna ya uandaaji wa viashiria vigezo na upimaji. Mhe. Mwenyekiti, sawa ameainisha vijiji vyenyewe hivyo kama Kiwengwa, Pwani Mchangani na kadhalika. Lakini je tujiulize hii elimu imefika na kama imefika elimu hii, manufaa yako wapi, manufaa yenyewe haya tuliyokuwa nayo. Sasa naingia huko kwenye safari yenyewe.

Mhe. Mwenyekiti, tutafika tu ukurasa wa 46, naanza kwa Mdhibiti. Hapa ndio nina masikitiko makubwa sana kwa Mdhibiti. Bajeti iliyopita nilimsema mtu ambaye alifukuzwa kazi Mhe. Waziri akatoa ufafanuzi mzuri tu wenye busara na hekma lakini bado wanafukuzwa watu kazi, ina maana ile juzi ulipiga gitaa tu wewe hapa bado utekelezaji haujatekelezwa. Tuna wananchi wetu kwenye majimbo yetu wanafukuzwa kazi ovyo. Hapa kwenye Mdhibiti pana wafanyakazi si chini ya wanne au watatu wale wamefukuzwa kazi kwa nadharia ya kuwa hawakusimamia upotevu wa shilingi bilioni moja katika Idara fulani, Wizara haina bilioni seuze hicho kitengo, hebu tufikirieni jamani.

Tunawasimamisha watu kazi kwa kuwatia mashaka hawa. Sasa ubaya wake zaidi Tume imeundwa, Mdhibiti ameunda Tume hatimae ripoti imetiwa kwenye *briefcase* mpaka leo Tume haijatoa uamuzi, sio haijatoa uamuzi imetoa uamuzi lakini kada mwenyewe hajasema. Mimi naanza kuzuia hapa mie, nipate maelezo ya kutosha hawa watu waliozuiliwa na ripoti ya Tume inasemaje, tusiwadhalilishe tu, Idara leo ina uwezo wa kuwa na bilioni moja, wakati Wizara haina hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, tusitumie vyeo kwa kudhalilisha watu, hichi kitu ambacho nasema kwamba tusikifanye kitu hicho ni jambo kubwa sana kwa Mwenyezi Mungu. Nasema hivyo kwa Mwenyezi Mungu wakati leo hawa maskini ya Mungu wanapata nusu mshahara, wana jukumu, wana watoto, wana watu wa kuwasaidia, wana maskini, wana wagonjwa, leo tunakwenda kuwafanyisha kitu kama hichi haileti taswira nzuri naanza kuzuia shilingi hapa. Mhe. Mwenyekiti, mfuko wangu ulikuwa hauna pesa, sasa naanza kuchukua pesa zangu hapa.

Mhe. Mwenyekiti, kama inawezekana kwa nini tusitunge sheria. Unajua kuna kitu ambacho Mhe. Mwenyekiti, kwa nini na wewe usichunguliwe, wewe unachungua na wewe uchunguliwe, kama kuna sheria tuleteeni Mhe. Waziri, ulete sheria hapa tuweze kuchungulia na sisi, *I am very serious* msifanye kitu masihara bwana, hichi kitu bwana si kitu cha mchezo kwa sababu hawa watu ambao tunawatumia, isiwe kwa maslahi ya mtu tu. Mhe. Waziri ameweka utandawazi hapa juzi tu amepandisha watu vizuri tu lakini leo wanafukuzwa, kila anayefukuzwa kazi sasa njooni Baraza la Wawakilishi tutakuteteeni sisi hakuna masihara. Haiwezekani Mhe. Mwenyekiti, kila siku watu hawa tu wafukuzwe, waliokuwa wizi hawafukuzwi. Kuna mtu ambaye anajulikana wakati ule Wizara ya Mawasiliano, kuna mtu alisimamishwa kazi kwa ubadhirifu na kamati ile ilitoa uamuzi, leo mtu yule amesharudishwa kazini na ameonekana ana kosa, yupo hatiani kabisa, yuko Kibele sijui anafanya kazi huko, karudishwa kazini wakati mtu mwizi karudishwa kazini, hawa waliokuwa wanatiliwa mashaka tena hawakusimamia vizuri wanapewa nusu mshahara kwa nini, tupo watetezi wao.

Mhe. Mwenyekiti, nasema hapa mimi kifungu hichi sitokipitisha kama sikupewa ripoti kamili kuambiwa tena niambiwe hawa watu hakuna tena Tume imeamua warudishwe kazini na mshahara wapewe, mimi nitakubaliana naye.

Mhe. Mwenyekiti, niende katika Kamisheni ya Utumishi wa Umma, majukumu makuu ya Taasisi hii ni kushauriwa Rais na masuala hayo. Lakini Mhe. Mwenyekiti, nisema tunaanzia na tatizo hapa. Sisi hapa Mheshimiwa wangu Mwanasheria siku zote husema kuwa tuangalie sana kwenye Katiba zetu ili kwa kuweza kusaidia tusiweze kukiuka Katiba ili kwa kuleta ufanisi uliokuwa na mstakbali mwema. Hapa naomba sana katika Kamisheni hii tunapokuwa tunataka kumshauri Rais katika masuala ya utumishi na Mhe. Rais anakuwa anatoa matamshi mazuri, lakini Mhe. Rais, si mtu ambaye ana

matatizo, tunakuwa na matatizo sisi kwa kuweza kuyatekeleza halafu tunamsingizia Rais, Rais hawezi kukataa kitu kwenye maslahi ya umma.

Mhe. Mwenyekiti, Baraza la Wawakilishi linakuwa na muundo wake na wao na Tume hiyo tumeipeleka muda mwingi sana kwenye Kamisheni hiyo na tukasema, mpaka leo inafika si chini ya miaka miwili kama hivi, hakuna jibu lolote ambalo limejibiwa. Sisi tunasema Baraza hili linakwenda na wakati tumepewa fedha na *UNDP* kwa kupata elimu na kututoa nje na kwenda kuangalia Mabaraza ya wenzetu au Mabunge ya wenzetu jinsi gani wanavyoendesha katika muundo wao au katika muhimili wao. Lakini sisi sijui tunakuwa tunaonekana tunafanya viroja. Mimi naamini Mhe. Mwenyekiti, hatufanyi viroja isipokuwa tunafanya lile jambo, unajua kila jambo sasa hivi linakwenda kwa wakati. Baraza la Wawakilishi lina muundo wake, utumishi wake, lakini la kusikitisha kabisa wataalamu hawa....

UTARATIBU

Mhe. Mwanasheria Mkuu:Mhe. Mwenyekiti, nadhani siku zote huwa tunasema kwamba nguvu ya Baraza hili ni kanuni zake na ndio maana Mhe. Mwenyekiti, Baraza hili unakaa hapo juu na joho sasa hivi, ungeweza kuteremka na joho lako lakini ukiteremka hapa chini rungu linafichwa na wewe unavua joho na mengine kama hayo, yote ni kwa sababu ya kulinda utaratibu wetu, si kwa sababu usingeweza kukaa hapa chini na joho, lakini ndio utaratibu wetu.

Mhe. Mwenyekiti, sasa kanuni zetu moja katika jambo ambalo linasisitizwa sana ni kutorudia rudia, ukiangalia kanuni ya 48 (7) inatuelekeza ifuatavyo. Inatuambia kwamba Mjumbe yeyote hatoruhusiwa kuchukua jambo lolote ambalo Baraza lilikwisha kuliamua ama katika mkutano uliopita, uliopo au ule uliotangulia isipokuwa kwa kufuata kanuni ya 49. Mhe. Mwenyekiti, naamini unakumbuka na wajumbe wanakumbuka kwamba suala la miundo ya Baraza la Wawakilishi na Utumishi wao limezungumzwa wakati tunazungumza bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais.

Mhe. Mwenyekiti, wakati ule yalitoka maelekezo nakumbuka alikuwa analizungumza Mhe. Hamza, hoja za msingi kabisa na akalizungumza katika Ofisi ya Uratibu na Mwenyekiti akamuomba kwa nini tusisubiri wakati wa Baraza la Wawakilishi, akatoa hoja zake kwa nini anataka kuzizungumza pale, lakini tukaendelea likazungumzwa, yeye alitaka Serikali ichukue dhima juu ya kulimaliza suala hili na Mnadhimu wa Serikali, Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, akachukua dhima hiyo na siku ya Jumapili wakati tuko Uroa, nakumbuka Mhe. Mwenyekiti, mimi mwenyewe, Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Mhe. Waziri wa Ofisi ya Rais Utumishi, Waziri wa Nchi Afisi ya Rais Makamu wa Pili, wakati wenzetu mmetangulia sisi tumebaki zaidi ya saa moja kuzungumza suala hili kwa yale ambayo yalishaamuliwa na Baraza hili wakati tunazungumza fungu la Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais. Sasa leo tunapolirudia hili Kanuni inatuelekeza hivyo na utekelezaji wenyewe umeanza kutekelezwa kwa kufuata yale

ambayo Baraza hili limekwishaamua. Sasa nadhani ni kinyume kabisa na kanuni yetu ya 48 (7) na pia inakwenda kinyume kabisa, nafikiri ya kanuni 59(1) ambayo inataka kwamba Baraza hili lizungumze hoja, lifanye maamuzi na maamuzi yale yatekelezwe, maamuzi yale yamo kwenye kutekelezwa, sasa leo tunaporudia nadhani ni kinyume na kanuni zetu.

Mhe. Mwenyekiti: Kwa vile Mjumbe alikuwa ni miongoni mwa Wajumbe kwenye kikao hicho tunaomba tuendelee na utaratibu mwengine wa suala jengine ambalo anataka kuchangia ndani ya dakika zake tatu zilizobakia, naomba tuendelee.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Usinibene, niachie na mimi nipumue. Kikao ulichosema ulichosema kilikuwa nje sio ndani ya Baraza, tulichozungumza hicho kikao anasema nilikuwepo mjumbe mwenyewe kule Marumbi tofauti na hapa, hapa ndipo penye sheria yenyewe tuzungumze hilo la kwanza. Lakini Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Hamza alipotoa hoja katoa Wizara ambayo ni ya Makamu wa Pili, mimi nasema katika Wizara yenyewe kuhusika, ndio hii kama mimi nitaizungumzia wapi, futa kifungu hichi Mheshimiwa basi nisikieleze, sina kanuni. Namuomba sana radhi Mhe. Mwanasheria, ameniambia kanuni hizo lakini mimi nimekwenda katika kifungu chenyewe husika, hapa ndio kuhusika na natarajia kupata maelezo ya yule muhusika mwenyewe.

Mhe. Mwenyekiti, la pili ingekuwa kama ni hivyo basi leo mapema tungetegemea kupata ripoti kwa huyo Mnadhimu wa Serikali kutoa *briefing* ambayo kauli ya mjumbe lakini leo unambie iko *briefing* hiyo, na ndio maana mimi nikaungumzia suala hili, kama nina makosa basi mimi nitamwambia Mhe. wangu Mwanasheria kwa hilo ninamuomba radhi, kwa sababu sioni tatizo leo nilikusudia hivyo

UTARATIBU

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Nasema tena kwamba nguvu ya Baraza hili, uwezo wa Baraza hili kusema kweli ni kanuni zake, kanuni zetu Mhe. Mwenyekiti, umeshaamua itatoka hoja imeamuliwa nilitegemea Mhe. Mshimba, ama atahoji kabla hujatoa uamuzi ili uzingatie hayo katika kutoa uamuzi, lakini tunachozungumza kanuni iko *very clear* kwamba mtu haruhusiwi kufukua jambo lolote. Tulipozitunga kanuni hizi tulikuwa tunajua Wizara zipo, mafungu yapo lakini kanuni zimeeleza *very clear*, siye tunachosema kwamba kama ni hoja hii au kama ni jambo hilo limezungumzwa, kanuni inavyotuelekeza kwenye mkutano huu halijazungumzwa. Sasa nasema kwamba kama ni hili limezungumzwa na hicho anachosema yeye kikao kwa kawaida yakishatoka maamuzi hapa, vikao vya kufuatilia hatufanyi humu Barazani, tunafanya nje ya Baraza, ndio utaratibu. Sasa hilo ndio nasema kwamba hicho kikao cha kufuatilia kimeshakwisha na hili jambo linafuatiliwa na Serikali ilichukua ahadi ya jambo hili.

Mhe. Mwenyekiti, sasa mimi nadhani sababu ya kanuni ya kuweka tusirudie rudie ni kwa sababu tunataka huu muda tuutumie vizuri kwa mambo ambayo hatuyazungumza yapo.

Mhe. Mwenyekiti: Nafikiri Mhe. Mwanasheria Mkuu hili suala limeisha tunamuomba Mhe. Mjumbe kama analo la kuchangia ndani ya dakika 3, jengine la ziada afanye, laa hana naomba aheshimu maamuzi ambayo yalikuwa yamepatikana kule tulipokuwa sote katika kikao muhimu.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Sasa nasema Mhe. Mwenyekiti, sitaki niwe mkaidi lakini na mimi najua njia ya kupitia mimi sikubaliani nacho kifungu hichi. Kifungu hichi na mimi sikubaliani nacho kabisa na nitakitolea shilingi mapema nakwambia kabisa, amenipa tahadhari namshukuru sana Mhe. Mwanasheria kwamba nizungumze mapema kabla ya kuja kuchangia suala lenyewe, basi nasema na mimi mapema kifungu hiki nakistopisha nakiondolea shilingi.

Mhe. Mwenyekiti, niende katika ukurasa wa 55. Nasema Tume ina jukumu la kuajiri na kusimamia utaratibu wa ajira Serikalini. Mhe. Mwenyekiti, ndio yale yale na mimi nasema siku zote ukenda kifungu hichi kinajirudia kinakwenda kifungu hichi ndio muundo wetu na ndio taratibu ulivyo. Mhe. Mwenyekiti, hapa tuna masikitiko makubwa sana hasa upande wa Wawakilishi wa *back benchers* hatutendewi haki na sisi kama tunaongoza wananchi kwenye majimbo. Sifa za wananchi wetu tunazo lakini hatupewi na sisi katika sifa hiyo wanasikia tu tayari watu wameshaajiriwa na ile kutangazwa inakuwa *abortion* tu ile kwa sababu unasikia leo kuna ajira tano, kumbe watu zamani wameshachukuliwa. Sasa na sisi kama ni watumishi wa watu tupewe nafasi ya kuweza kuwaajiri kuwaleta waajiriwe, kwa hizo sifa walizokuwa wanazitaka wao sisi wananchi wetu tunao, tatizo hilo tunalo lakini ufafanuzi wake mpaka leo na hili nimeshalisema mara nyingi sana, ajira zetu wanachukua Mawaziri, yaumu shaka msinipigie buti nasema Mawaziri hatuwajui nani lakini ni yaumu shaka na kama tutakwenda kufanya *research* tutakuta hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kumalizia nimebenwa benwa hapa nasema sitounga mkono abadan na wananchi wameniambia nisiunge mkono lakini nikipata maelezo mazuri nasaha nzuri nitakuja kuunga mkono baadae. Ahsante sana.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Mhe. Mwenyekiti, naanza kwa jina la Mwenyezi Mungu kumshukuru mwenyewe Subhana Wataalla kutuamsha tukiwa hai na wazima, kuturudhuku uhai tukaendelea na shughuli zetu mbali mbali katika ulimwengu huu na hasa katika kipindi hichi katika Baraza hili la Wawakilishi tukijadili masuala yanayohusu nchi na watu wake.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile naomba kukushukuru na wewe na kunipa nafasi hii ya kuwa mtu wa pili leo kuchangia bajeti hii ya Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Tatu Mhe. Mwenyekiti, naomba nimpongeze na Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora na yeye kwa kuja

kuwasilisha hotuba yake vizuri, katuletea kitabu kizito lakini pia kimeambatana na kitabu cha maelezo ya bajeti inayotumia *program*.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya shukurani na pongezi hizo kuna suala limejitokeza naomba nilizungumze hapa kabla sijaingia katika mchango wangu kwa sababu linahusu maslahi ya nchi yetu, nilikuwa na utaratibu wa kutumia ile kanuni ya kujadili jambo la dharura lakini nikaona si jambo kubwa la hivyo la kuweza kutumia utaratibu ule, lakini kwa sababu ninapojadili hapa najadili masuala ya nchi yetu, kuna suala limejitokeza limenikirihisha na bahati nzuri kwa wanaofuatilia katika mambo ya mitandao huko limewakirihisha Wazanzibari wengi sana, yaani ni suala zima taswira ya nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, kama tunavyofahamu hivi sasa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ina ugeni mzito wa Rais wa Marekani Mhe. Barack Obama. Mhe. Mwenyekiti, kwa bahati mbaya sana kuna baadhi ya vyombo vya habari vimeamua kutumia nafasi hii kuipaka matope na kuichafua Zanzibar. Bahati mbaya sana mimi ninahidi kuna ajenda ya kisiasa nyuma ya hili kwa sababu waandishi wenyewe wa vyombo vya kimataifa, lakini angalau muandishi mmoja katika vyombo hivi viwili ni mwandishi anatokea upande wa Tanganyika. Naomba Serikali ifuatilie na akitaka naweza baadae kuwapa. Kuna taarifa ambayo imechapishwa katika mtandao wa *Aljazeera* ni chombo kikubwa kinachoheshimika duniani, ikizungumzia ujio wa Rais Obama, lakini mwandishi anaitwa Erick Kabendera kaandika makala akihusisha Zanzibar na ugaidi na kujaribu kupotosha mjadala mzima wa suala la Katiba linaloendelea hivi sasa akihusisha na taswira chafu kwa nchi yetu, hilo halikubaliki hata siku moja Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti, tumechoka kudhalilishwa Zanzibar lakini ingelikuwa moja mimi ningelisema kwamba labda ni suala la bahati mbaya, lakini na jana usiku kuna kijana wetu wa Kizanzibari akanitelea *link* ya mtandao mwengine ambapo huko kuna Shirika la Habari linaitwa *CBN*, nina wasi wasi kwamba lina madhehebu fulani ya kidini, linazungumzia ziara hii lakini tunajua sote habari ikianzaa mara nyingi kuna utaratibu wa kuandika ile *profile*, imeandikwa Zanzibar lakini panazungumzwa ukosefu wa uvumilifu wa kidini ikihusishwa Zanzibar. Sasa Mhe. Mwenyekiti, kwanza haya masuala yaliyozungumziwa yote kama ni uvumilivu wa kidini yako Mahakamani na bado haijatoka hukumu kuweza kujua kwamba yanahusika na uvumilivu wa kidini au kutokuwepo kwake na yana dhamira nyengine. Mhe. Mwenyekiti, hili ni baya.

Mhe. Mwenyekiti, juzi tulipambana vya kutosha kusafisha taswira ile, naiomba Serikali hili isiliachie itoe kauli rasmi na bahati nzuri Baraza hili liko katika mkutano unaendelea, litoe kauli rasmi kuviambia vyombo hivi na kuiambia dunia kwamba Zanzibar hakuna ugaidi na jitihada zote za kupotosha na kuchafua taswira ya Zanzibar tunazikataa kwa nguvu zetu zote. Mhe. Mwenyekiti, sisi ni Wawakilishi wa wananchi na viongozi tuliopewa

dhamana naomba sana katika hili baadae nitazichapa niwape Serikali hizo nakala mbili ambazo nimezizungumzia.
Mhe. Mwenyekiti, tumechoka Zanzibar kufanywa ndio jaa la hawa kwao kumetokezea matukio makubwa katika Mji wa Arusha kwa muda wa kipindi kifupi mabomu mawili yameripuka hatujasikia yakihusishwa na mambo haya, lakini Zanzibar ndio kila wakati imekuwa ndio pahala pao kutupia uchafu wao, tumechoka.
Mhe. Mwenyekiti, baada ya kutumia fursa hii kulizungumza hili naomba sasa niende katika bajeti hii ya Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora.
Mhe. Mwenyekiti, mimi kwanza nianze kwa kupongeza nampongeza Mhe. Rais, katika dhana yake nzima ya kuanzisha ofisi hii, lengo ilikuwa ni kufanya utawala bora na hasa utumishi wa umma uwe una mipango na mipangilio, maana unaweza ukawa na mipango usiwe na mpangilio, uwe na mipango na mipangilio, kama tujue kuna nidhamu zinazoongoza au taratibu zinazoongoza masuala mazima ya utumishi wa umma. Kwa hivyo nadhani itakuwa hatutendi haki ikiwa hatukuipongeza Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais Utumishi wa Umma Utawala Bora

Nam408

IMESAHIHISHWA

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: (anaendelea) tukaipongeza Wizara hii ya Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa kazi ambayo wameanza kuifanya.

Mimi napata taaluma zaidi kwa sababu nilikuja kujua kwa vile kipindi kilichopita nilikuwa Mjumbe wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala. Moja katika wizara mbili tulizokuwa tukisimamia ni wizara hii, nikajua kwamba moja katika watu walioshiriki kiasi kikubwa kuandaa rasimu ya sheria ile mpya ya Utumishi wa Umma alikuwa ni Mwanasheria Mkuu wetu Mhe. Othman Masoud Othman. Tunamjua sote weledi wake, kwa hivyo hata tulipopewa semina sisi Wajumbe wa Kamati wakati ule tuliona kwamba kuna nia nzuri na sheria imejipanga vizuri. Hitilafu za hapa na pale haziachi kujitokeza kwa sababu sisi ni binadamu, na mwenyewe Mhe. Mwanasheria Mkuu katika sisi ndio tuliomaliza karibuni tu alitwambia kwamba mara nyingi sheria unaweza kuiona mapungufu yake unapoanza kuitekeleza.

Kwa hivyo, napongeza mheshimiwa najua unapokuwa na vichwa kama cha Mhe. Mwanasheria Mkuu mimi mwanasheria kama hizi au mageuzi kama

haya una kila sababu ya kuamini kwamba lengo ni zuri na tutafika pahala pazuri.

Lakini baada ya pongezi hizo Mhe. Mwenyekiti, niseme kwamba bado tunayo kazi kubwa ya kusimamia mambo haya. Kamati ya Katiba, Sheria na UItawala chini ya mwenyekiti wake kijana ambaye tunamtegemea huko siku za mbele atazidi kung'ara Mhe. Ussi Jecha Simai. Inafurahisha Mhe. Mwenyekiti, kuona vijana wanashika nafasi za uongozi katika kamati zetu za Baraza hili kwa sababu inaonesha kwamba lile lengo la kujenga uwezo kwa watoto wapya linaendelea vizuri.

Katika hotuba yake aliyoisoma hapa kazungumzia kwamba bado katika Utumishi wa Umma uajiri bado unaelekezwa zaidi katika kuwa unamjua nani kuliko kuwa unajua nini. Alisema Mwenyekiti wa Kamati, yaani bado tatizo la kuajiri kwa kutegemea *know how* badala ya *no how* ni elimu maarifa yako, lakini *know how* mimi namjua Mhe. Ismail Jussa ana ukubwa pahala fulani basi yeye ataniunganishia nipate ajira hii. Hili bado liko Mheshimiwa.

Hivi karibuni alilizungumza Mhe. Omar Ali Shehe humu ndani akataja kadhia kwamba hizi ajira zilizokuwa zimetangazwa mbona kunaonekana kwamba taratibu hazikufuatwa. Lakini na mimi Mhe. Mwenyekiti, juzi katika jimbo langu mwenyewe kuna kijana kanifuata, kwa sababu anaendelea kutafuta kazi sitaki kumtaja jina nisije nikamharibia zaidi akawa asipate. Lakini kumetangazwa nafasi za kazi katika wizara fulani wamekwenda wamefanyiwa mahojiano, wote wamemthibitishia kwamba wewe umefanya vizuri kuliko wote, ulipokuja uajiri kawekwa upande.

Sasa napata tabu Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu moja ya msingi mkubwa wa sheria ile ilipokuja tuliambiwa ni kuzingatia uwezo kwamba ndio msingi wa sheria ile na mabadiliko au mageuzi itakayoyafanya. Kasema Mwenyekiti wa Kamati, Mhe. Ussi kwamba utendaji kazi bado haujabadilika kwa sababu miaka mingi tuliajiri watu kwa kuzingatia unamjua nani badala ya kuwa unajua nini. Sasa katika kipindi hiki cha kusimamia mageuzi chini ya sheria hii ambayo tuliisifu sana hapa na ile misingi sita tuliyokuwa tumeitaja pale mwanzo katika sheria hii. Ikiwa katika utekelezaji bado kunatumika hoja nyengine ziwe za kisiasa, ziwe za kumjua nani, ziwe za kuwa umetoka wapi, bado tutakuwa na kazi refu sana katika kujenga utumishi wa umma uliokuwa unaweza kumsaidia mwananchi wa Zanzibar na kubadilisha maisha yetu.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, naomba hili waziri na uongozi wake wa wizara ulitazame tena, tunakwenda bado bajeti ziko mbili kabla Baraza hili halijafikia mwisho, tusifikishane mahali tukaja tukataja na majina na mifano. Kama ninavyosema ingelikuwa si kuchelea kwamba huyu kijana nitamharibia

zaidi maana ndio unajua kazi zetu zinavyokwenda ningetaja mimi, lakini bado kuna matatizo katika mawizara yetu na katika usimamizi wa suala hili la uwezo.

Mhe. Mwenyekiti, hatupigi hatua hata moja ya maendeleo ikiwa hili hatujalifanyia kazi. Upendeleo Waingereza wanaita *nepotism* katika masuala ya uajiri na katika suala la kutoa huduma unauwa maendeleo ya nchi yoyote duniani, seuze yetu sisi ambayo bado inajikongoja.

Mhe. Mwenyekiti, jengine ambalo nataka nilizungumzie nimesikitishwa kidogo, alipokuja Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo alitwambia kwamba serikali imekusudia kunyanyua na kuongeza maslahi ya watumishi wa umma. Akatwambia maelezo tutakuja kupewa na waziri mhusika lakini nakipitia kitabu cha bajeti katika ukurasa wa 68 mpaka 71 ndio kumezungumziwa maendeleo na maslahi ya wafanyakazi.

Mhe. Mwenyekiti, hakuna maelezo ya kutukinaisha sisi kwamba kimeongezwa kiasi gani na utaratibu wake, baadae hiyo nyongeza kwengine itakwenda vipi. Mwaka juzi tulioongeza angalau tuliambiwa kwamba kima cha chini kimeongezwa kwa asilimia 25 halafu tukaambiwa yaliyobakia waongezewa kulingana na uwiano huo na wale ambao wana taasisi ama wana fani maalum utaratibu utakuwa tofauti. Mara hii hata ule msingi hatuujui, Waziri wa Nchi (OR) Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo katwambia tusubiri Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora kaja hotuba yake hapa iko *vague***.**

Sasa sisi kama wapitishaji wa bajeti tunapitisha msingi wa hiyo nyongeza bila shaka itakuwa na fungu lake lile, lakini tushachoka Mhe. Mwenyekiti, kupitisha ile *lump sum,* fungu tunaambiwa kwamba hili ni la marekebisho ya mishahara lakini sisi wapitishaji hatujui msingi wake upi. Hili mimi binafsi siwezi kulikubali kama sijapewa maelezo hasa, msingi wake wa nyongeza unaanzia wapi kama kuna kima cha chini kinaongezwa kiasi gani. Hayo marekebisho mengine au haya maelezo ya jumla jumla mimi Mhe. Mwenyekiti, siwezi nikayakubali.

Mhe. Mwenyekiti, jengine hapo hapo tunazungumzia kuhusu kuongeza maslahi ili kulinda watu wetu wasiondoke wale wenye fani maalum. Sasa hili ni tatizo Mhe. Mwenyekiti, na mimi naogopa dhana inayojengeka katika wizara hii na kamisheni yake kujiona kwamba wao wafalme waliobakia wote ni kama vile manokoa wako mashambani huko.

Mhe. Mwenyekiti, tunazo taarifa kwamba Wizara ya Afya imependekeza marekebisho ya mishahara ya madaktari, lakini lishamalizika huko wafalme walioko katika Kamisheni ya wizara yao wamekwamisha mpaka leo, mpaka imefika pahali tunaambiwa Waziri wa Afya kasema iko siku wakigoma madaktari mimi nitaungana nao kugoma nao pamoja. Sasa Mhe. Mwenyekiti, kama kuna fani inaenziwa duniani ni fani ya udaktari, ukienda katika nchi za watu kama Uingereza na nchi nyingi za Magharibi ukishasoma unaambiwa uondoke pale ukatafute kazi kwenu, lakini ukiwa katika fani ya udaktari au uuguzi kwa sababu inajulikana ni fani muhimu inayotakikana unabembelezwa ubakie na kupewa mshahara mzuri katika nchi iliyokuwa si yako. Tunawajua vijana wengi tu wa Kizanzibari hapa madaktari wamepata kazi katika katika nchi za huko Ulaya, mimi nawajua wengine tumesoma nao na wengine wako katika nchi jirani hapo kama vile Botswana, Msumbiji wanafanya kazi kwa sababu sisi tumeshindwa kuwatunzia maslahi yao.

Mimi najiuliza katika Zanzibar hii madaktari hao ni wangapi na wana tofauti ya kiasi gani ambapo wizara inaona tabu kuwaidhinishia mpaka ifike pahala waziri anasema atagoma na madaktari wake. Ndio maana juzi nilionekana kama mtu wa ajabu, nakataa Mhe. Mwenyekiti, hii dhana kwamba watawala tu juu ndio tunaoangalia maslahi yao iwe waziri, katibu mkuu, mwakilishi lakini hawa wanaotufanyia kazi na kufanya kazi kubwa sana ya kutunza maisha yetu na watu wetu hatuwatizami.

Walimu Mhe. Mwenyekiti, sisi sote tulifika hapa kwa sababu tulianzia darasani na jamii ambayo haiheshimu walimu basi haiwezi kumheshimu mtu yeyote. Najua kwa walimu kuna mtihani kwa sababu ni wengi sana, lakini nasema wakati tunafanya marekebisho ya mishahara tunazitizama fani kama hizo? Leo tunapata matokeo mabovu ya mitihani sababu ziko nyingi, lakini moja mimi naamini ni maslahi ya walimu na maslahi ya walimu hayawavutii wale waliokuwa na uwezo mzuri kubakia katika fani hii. Kwa hivyo, tunawapata watu ambao uwezo wao mdogo wanakuwa hawana pa kwenda ndio kimbilio lao imekuwa ualimu. Katika hali kama hiyo tunategemea watoto watapasi vipi Mhe. Mwenyekiti.

Kwa hivyo, mimi nasema suala hili la maslahi Mhe. Mwenyekiti, walitizame tena, nimelitaja la madaktari kwa sababu hili nalijua kwamba wizara imekamilisha madaktari wanakuja kutulilia hali sisi. Sasa kama ninavyosema madaktari hawa Zanzibar wako wangapi. Tunajua hali yetu ilivyo hapa kwa nini tushindwe kuwapa maslahi bora.

Mhe. Mwenyekiti, pamezungumzwa hapa najua Mhe. Mwanasheria Mkuu katoa hoja ya suala hili kwamba tusilijadili kwa sababu limeshatolewa maamuzi. Lile la maslahi kwa kuheshimu kauli ya Mwanasheria Mkuu kwa

hapa naliacha, lakini moja siwezi kuliacha Mhe. Mwenyekiti. Nalo palikuwa na suala la maslahi na ni mategemeo yangu kwamba kwa vile tumeambiwa linashughulikiwa kwamba mapendekezo tuliyonayo Baraza la Wawakilishi yataheshimiwa.

Kuna la pili ambalo hili lilinishitua sana Mhe. Mwenyekiti, na ni dharau ya mwisho kwa chombo hiki cha Baraza la Wawakilishi, chombo ambacho tumesema wenyewe hapa heshima yake ni kubwa, hili si suala la maslahi ni suala la kuamua hata idara zake.

Mhe. Mwenyekiti, Katiba ya Zanzibar ibara ya 77(1), inasema kwamba:

> "77(1) Kutakuwa na Afrisi ya Baraza la Wawakilishi itayoongozwa na Katibu wa Baraza la Wawakilishi na itakuwa na nafasi za madaraka kama itavyoidhinishwa na Tume ya Utumishi ya Baraza la Wawakilishi".

Lakini siku ile ya semina ya Baraza la Wawakilishi *Zanzibar Beach Resort*, mimi nilipata *shock* kumsikia Katibu wa Kamisheni ya Utumishi anasema kwamba idara za Baraza la Wawakilishi mpaka zikaidhinishwe na Rais, hii ni mihimili tofauti. Lakini najiuliza kama hoja yake ilikuwa ni kwamba wenye mamlaka ya kuanzisha Ofisi ni Rais, mbona wakuu wa Idara hizi katika Baraza la Wawakilishi hawatangazwi na Rais, hivi ni vitu tofauti. Ilikuwa ni kauli ya dharau na kebehi ya mwisho kabisa kwa chombo hiki Mhe. Mwenyekiti, kwamba Baraza hili haliwezi kuamua idara zake na taasisi ati zikaidhinishwe kwa Rais tumeona wapi duniani?

Mimi sijasikia Bunge la Uingereza hivyo mpaka Waziri Mkuu aidhinishe au hata hapo Bara, hivyo anataka kutwambia kwamba Idara za Bunge mpaka zikaidhinishwe na Rais wa Jamhuri ya Muungano au nchi yoyote nyengine. Mimi sijawahi kusikia hii kwamba chombo cha Kutunga Sheria muhimili mmoja wa dola idara zake zikaidhinishwe na Rais, sijapata kusikia. Lakini ndio ule usemi niliosema kuvaa joho na kudhani kwamba wafalme wengine wote manokoa tu. Mhe. Mwenyekiti, sisi hatuwezi kukubali kudharauliwa chombo hiki. Nasema nataka maelezo kuhusu hili. Nataka maelezo vile vile kwa Mhe. Waziri sizungumzii tena miundo ya utumishi hiyo tumeambiwa tuiwache naiacha. Mimi nazungumzia sasa utekelezaji wa maamuzi.

Mhe. Mwenyekiti, ninavyoambiwa kwamba Tume ya Bajeti ya Baraza ambayo imeanzishwa na Kanuni ya 147 ya kanuni zetu ilisharidhia marekebisho na hoja iliyotolewa sizungumzi miundo, nazungumza sasa hoja ya uwezo wa kifedha ya serikali kuhudumia, tuliambiwa kwamba

haiwezekani. Lakini naambiwa katika kikao cha Tume ya Bajeti ambapo Waziri wa Fedha ni mjumbe ilikwishaelimisha kwamba tofauti yenyewe wala si kubwa kiasi hicho inayozungumzwa ya maslahi ya wafanyakazi, ni bajeti ambayo tofauti yake kwa mwezi ni kama shilingi 8,749,000/-, kwa mwaka mzima sijui hata kama zitatimia labda shilimgi milioni mia moja na ushei.

Sasa mimi nataka kumuuliza waziri anambie kwamba wenye fedha walisema inawezekana na Tume ya Bajeti ndio ikapitisha, na mwaka jana ilikuwemo katika bajeti na mwaka huu imo. Sasa hawa wizara inapokwamisha msingi wake nini aje nisaidie Mhe. Waziri ili tuone kama bajeti hii inafaa kwa hilo.

Mhe Mwenyekiti, niondoke hapo niende katika Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe una dakika tano za ziada.

Mhe. Ismail Jussa Ladhu: Aah!, si ya ziada Mhe. Mwenyekit, kwa mujibu wa kanuni sijafikia nusu saa bado ambayo ninaruhusiwa.

Mhe. Mwenyekiti, Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali imeanzishwa na Katiba yetu na ni chombo huru. Sasa hapa naomba nisaidiwe kwa sababu ya muda nisitoe maelezo marefu. Lakini Mhe. Mwenyekiti, tuna taarifa kwamba kuna kuingiliwa ingiliwa kwa ofisi hii.*(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, Katiba ya Zanzibar ibara ya 112(7) inasema kwamba:

> "112 (7) Katika kutekeleza madaraka yake kwa mujibu wa masharti ya kijifungu cha (3), (4) na (5) ya kifungu hiki, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali hatalazimika kufuata amri au maagizo ya mtu mwengine yeyote au Idara yoyote ya Serikali, lakini maelezo haya ya kifungu hiki hayataizuia Mahkama nayo kutumia madaraka yake kwa ajili ya kuchunguza kama Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ametekeleza madaraka yake kwa mujibu wa masharti ya Katiba hii au siyo"

Mhe. Mwenyekiti, ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya Zanzibar kwa kipindi cha mwaka 2010/2011 katika ukurasa wa 97 na 98 ilitajwa orodha ya wastaafu wa KMKM ambao wameshastaafu mwezi wa Disemba 2011, lakini mishahara yao hadi Machi inaendelea kupelekwa vikosini. Tunaambiwa kwamba sio hawa tu lakini katika *sample* iliyofanywa ya ukaguzi imegundua kuna uoza mkubwa zaidi kuliko huu. Hizi ni fedha za

wananchi maskini wa Zanzibar ambao tunawaambia wachangie katika matibabu, elimu, maji, wahangaike wakatafute mchele wa mapembe wale na familia zao lakini huku fedha zao tunaziachia zinatafunwa namna kama hii Mhe. Mwenyekiti. Sasa Mhe. Mwenyekiti, sijui kumekwama nini katika kufanya ukaguzi yakinifu na unaotosheleza wa suala hili. Sasa mimi hili sitaki kuingia katika maeneo mengi Mhe. Mwenyekiti.

Juzi Mhe. Mwenyekiti, nilitoa hoja hapa kwamba kwa mujibu wa Sheria ya Fedha za Umma ya mwaka 2005 kifungu cha 26(6) kinatoa mamlaka kwa Baraza au kamati zake kuagiza kama inaona pahala popote pana matatizo ya kimahesabu mkaguzi akafanye mahesabu. Mhe. Mwenyekiti, nawaomba wenzangu waridhie na katika hili kila anayekuja aniunge mkono, Baraza hili liagize Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ikapitie *pay roll* yote ya serikali ijiridhishe, kwamba kweli fedha inayoambiwa ya mishahara wafanyakazi hao kweli wapo au kuna watumishi hewa? Kuna wakubwa wanashirikiana wanakula fedha hizi kwa ajili ya mishahara hewa. Kama ilivyotajwa katika ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu kwa mwaka 2010/2011 mimi nataka ikafanywe *proper auditing* ya ukaguzi yakinifu wa *pay roll* yote ya serikali. Mhe. Mkaguzi akatufanyie tujiridhishe na hilo Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti, nimalizie na suala la e-*Government*. Katika hotuba ya waziri ukurasa wa 9 mpaka 11 kazungumzia suala la e-*Government*. Katika ukurasa wa 11 naomba nimnukuu Mhe. Mwenyekiti, anasema kwamba, "Hadi kufikia mwezi wa Machi 2013 Idara imetumia jumla ya shilingi 98,737,130/= kwa kazi za kawaida na shilingi 57,249,900/= kwa utekelezaji wa kazi za maendeleo. Kutokana na kuchelewa kuanza kwa matumizi ya huduma za mkonga wa mawasiliano ya *ICT* hakuna makusanyo yaliyopatikana na kwa sasa ukusanyaji wa mapato hayo umehamishiwa Ofisi ya Rais, Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo Zanzibar".

Mhe. Mwenyekiti, pana harufu ya uvundo hasa sio ya kawaida. Mwaka jana tulikuja kuambiwa kwa mapozi humu ndani na kila aina ya majigambo kwamba mradi umekamilika. Sasa serikali badala ya kupoteza fedha nyingi katika suala la mradi itaingiza fedha kutokana na mradi huu wa mkonga wa taifa unaoambatana na kutoa huduma katika *e-Government*.

Mhe. Mwenyekiti, mimi sasa nina kila sababu ya kuliambia Baraza lako kwamba hapa pana wizi umefanyika, kwa nini niseme hivyo, nimesimama ndani ya Baraza hili si mara moja, mbili wala tatu katika mradi huu, nimezungumza na ile iliyokuwa kamati yangu ya zamani ya Katiba, Sheria na Utawala kudai hesabu za mradi huu, tukaagizwa tuombe Wizara ya Fedha

tumeandika barua katika kamati iliyopita mpaka tumemaliza mwaka hatukupewa hesabu za mradi huo, kuna nini kinafichwa.

Mhe. Mwenyekiti, nilipokuwa nikichangia mwaka 2011 bajeti hapa nilisema kwamba bajeti ya milioni 19 Dola za Kimarekani kwa mradi huu zimekuzwa sana, na nikasema wataalamu walikuwa wanasema kwamba kuwa nguvu yake na masafa yake basi ilipaswa isizidi US$ milioni tano. Mimi si mtaalamu wa fedha lakini nikasema hebu turidhishwe hatukuridhishwa. Leo tulipoomba uchanganuzi wa mahesabu hatupewi lakini maelezo tunayoyapata sasa hivi tuko katika Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi na wewe Mhe. Mwenyekiti ni Mwenyekiti wa Kamati hiyo, wewe mwenyewe shahidi, tukienda katika kazi tunaambiwa kwamba hata namna ya uzikaji wa ile *fiber optic* umefanywa chini ya viwango, watu wameripua ripua tu, matokeo yake ndio maana mradi huu unashindwa kufanya kazi.

Mimi nina kila sababu ya kuamini kama hapa fedha za wananchi maskini tunatumia *Exim Bank* ya China kwenda kutafuta mikopo mikubwa mikubwa ikaning'inia katika shingo za wananchi wa Zanzibar wataendelea kulipa madeni miaka mia inayokuja huku watu wanakula fedha hizi. Mhe. Mwenyekiti, katika hili mimi nimefika pahala na nitakuja katika vifungu nitasimama sio tu niondoshe shilingi, lakini nitataka Kamati Teule iundwe ikachunguze mradi huu wote tena ikifika hapo nitaomba kwamba isiwe tu Wajumbe wa Baraza kwa sababu hapa pana masuala ya kitaalamu, lakini Baraza liidhinishe tupate wataalamu wanaoaminika waliokuwa hawajaegemea upande wowote tufuatane nao na watakaoteuliwa; wala sisemi labda niwe mimi, yeyote, wakafanye kazi ya kupitia kwa kituo mradi huu tujue uhalisia wa mradi huu Mhe. Mwenyekiti. Tumechoka kila siku kuja hapa tukishuhudia fedha za walipa kodi zinatumika ovyo. Maana yake ikiwa ni deni ni fedha za walipa kodi hizo wanazilipa wananchi wa Zanzibar huku sisi tukiendelea kuwaambia wachangie elimu, afya, maji wachangie kila kitu. Sio tatizo kuchangia lakini basi tija ionekane.

Baada ya hayo Mhe. Mwenyekiti, bajeti hii siipitishi mpaka nipate maelezo ya mafungu yangu niliyoyasema.xxxxxxxxxxxxxxxxxxxxxxxxxxxxxxxxxxxxxxxx

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutukutanisha hapa sisi sote tukiwa wazima kujadili hotuba hii ya Waziri wa Nchi, (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka fedha 2013/14.

Mhe. Mwenyekiti, pili nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii ya kutoa maoni mawili matatu kuhusu bajeti hii. Lakini pia Mhe. Mwenyekiti, nimpongeze Mhe. Mwenyekiti wa Kamati na watendaji wake kwa ujumla

kwa kutuleta hotuba yao lakini pia nimpongeze Mhe. Waziri kwa uwasilishaji wa hotuba hii.

Mhe. Mwenyekiti, mimi kama Mjumbe wa Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala sitokuwa na mengi mno ya kusema kwa sababu naamini maoni ambayo Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ameyasoma mbele ya Baraza hili ni maoni ambayo ametoa ushauri, maelekezo na ufafanuzi ambao ameuomba ni kwa niaba ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala.

Mhe. Mwenyekiti, mimi kwa kuanzia nianze na Idara ya Nyaraka na Kumbukumbu na katika idara hii pamoja na maeneo mengine nitagusia yale maeneo ambayo kwa muda mrefu sasa yamekuwa ni kilio tangu tumeanza Kamati ya Katiba ya kipindi kilichopita hadi hivi sasa. Kuna baadhi ya mambo ambayo hayajapatiwa ufumbuzi na hivyo nitagusia maeneo hayo na baadae nitawaachia wajumbe wengine kuzungumzia katika yale mambo ambayo wanahisi wanataka kuishauri serikali.

Mhe. Mwenyekiti, naipongeza kazi nzuri inayofanywa na Idara ya Nyaraka na Kumbukumbu za Kitaifa kwa kutunza kumbukumbu zetu muhimu za kihistoria na kutoa huduma za utafiti. Katika utunzaji wa nyaraka lazima kuwe na uangalifu mzuri sana na nashukuru idara ilikuja na wazo zuri sana la kutafuta *CCTV Camera* ili kuona kwamba kunakuwa na ulinzi mzuri wa nyaraka hizi. Lakini la kusikitisha tangu tumeanza kazi Kamati ya Katiba na Sheria ya kipindi kilichopita na hadi hivi sasa idara hii imekuwa na lengo hili la kununua *CCTV Camera* mpaka hivi sasa halijakamilika. Hebu mara hii nimuombe Mhe. Waziri kwamba lengo hili lifikiwe sasa ni muda mrefu sana tangu wamekuwa na hilo wazo na kila siku watanunua, hivyo naomba mara hii lengo hili angalau tuone utekelezaji wake halisi unafanyika.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, tukiachia mbali na suala la *CCTV Camera*, idara hii pia hutoa nafasi kwa watu mbali mbali wa nje na wa ndani kwenda kufanya utafiti katika idara hii nyaraka. Kwa kuthibitisha hayo kiambatanisho Nam. 5 ambacho kimo katika hotuba ya Mhe. Waziri imeonesha idadi ya watafiti waliofika Idara ya Nyaraka na Kumbukumbu za Taifa.

Mhe. Mwenyekiti, pia hapa tumekuwa tukiishauri serikali tangu tumeanza kazi kama Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kwamba yale malipo ambayo yanalipiwa kwa utafiti huu yanalipiwa katika Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais na tukashauri kwamba yale malipo ni vizuri yangefanyika pale pale Idara ya Nyaraka ambapo hao watu huenda wakafanya huo utafiti.

Katika hotuba ya Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais nilijaribu kuangalia katika mapato kama kuna sehemu yoyote ambayo haya

malipo yanaambatanishwa lakini kwa bahati mbaya sikuona. Kwa hivyo, naomba kwamba kila siku tumekuwa tukiishauri wizara kuwa wazungumze na Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais ili malipo haya yawe yanafanyika katika Idara ya Nyaraka na Kumbukumbu, lakini mpaka hivi leo suala hili halijafanyika. Kwa hivyo, naomba kuuliza sijui kuna ugumu gani labda Mhe. Waziri atueleze kwamba kuna ugumu huu na huu wa malipo haya kufanyiwa *transfer* kulipwa katika Idara ya Nyaraka.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo niingie ukurasa wa 59 katika Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi Zanzibar. Mhe. Mwenyekiti, mamlaka hii ni mpya na ndio kwanza mara hii imepata bajeti yake. Naitakia kila la kheri mamlaka hii katika kutekeleza majukumu yake, lakini pia hapa tunaishauri mamlaka kuwa sisi Wajumbe wa Kamati wa Katiba, Sheria na Utawala kipindi kilichopita tulipata nafasi ya kutembelea taasisi kama hii Tanzania Bara inayojulikana kama TAKUKURU. Wakati tulipofanya mazungumzo nao walitushauri kwamba tukitaka ufanisi mzuri katika taasisi hii basi tusikosee pale taasisi hii inapoanzishwa.

Katika kipindi hiki cha Kamati ya Katiba chini ya Mwenyekiti wangu Mhe. Ussi Jecha Simai tulishauri kwamba maslahi ya wafanyakazi wa mamlaka hii yaangaliwe sana. Kwa sababu tukikosea na tukiwapa maslahi madogo na hawa wafanyakazi wanakwenda kuchunguza kesi za mabilioni ya pesa kutakuwa na vishawishi. Nafikiri Mhe. Mwenyekiti wa Kamati katika hotuba yake pia ameligusia, amesema tuhakikishe kwamba wafanyakazi wa mamlaka hii na Mhe. Waziri tumemwambia na tunamuomba kwamba hili alitilie maanani aangalie sana maslahi ya wafanyakazi hawa. Hata wenzetu wa TAKUKURU wanafanya hivyo kila baada ya muda wanapohisi kwamba wana uwezo wa kuwa-*bust* hawa wafanyakazi wao wanafanya hivyo.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Mjumbe nitaomba uendelee tena jioni nafasi ilibakia.

Waheshimiwa Wajumbe baada ya hatua hii tuliyofika naomba kuahirisha Baraza hadi saa 11:00 jioni.

(Saa 7:00 mchana Baraza liliahirishwa hadi saa 11:00 jioni)

(Saa 11:00 kamili Baraza lilirudia)
(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe kuendelea na mchango wake kuna taarifa ambayo imekuja. Jana tulipokuwa katika kikao chetu hapa kuna mambo ambayo Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais aliahidi kwamba atakuja kuwasilisha katika Baraza hili.
Sasa nyaraka zile tayari zimewasilishwa kwa vile tumechelewa kufika nimeomba bora tuziache kwanza tusubiri muongozo wa Spika ili tuweze kupata maelekezo ya ziada.
Baada ya taarifa hiyo sasa naomba Mhe. Wanu Hafidh Ameir naomba uendelee.

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: Mhe. Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia nafasi tena kumalizia yale machache ambayo nakusudia kuchangia katika hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Mhe. Mwenyekiti wakati nilipokuwa nachangia mchana niliishia katika Mamlaka ya Kuzuia rushwa na Uhujumu uchumi na nikamuomba Mhe. Waziri kwamba na Serikali kwa ujumla walifikirie kwa kina suala la maslahi ya wafanyakazi wa mamlaka ile ili wawajengee mazingira mazuri waondokane na vishawishi na vichocheo vyengine vya nje.

Mhe. Mwenyekiti, sambamba na hilo nizungumzie kuhusu suala la maadili ya watumishi na hasa sisi viongozi. Mhe. Mwenyekiti, tumekuwa tukipiga kelele sana maslahi ya watumishi wa umma kunyanyuliwa. Lakini sambamba na hilo Mhe. Mwenyekiti, wasitake kupatiwa maslahi makubwa tu na ile *output* yao ionekane pia. Ndio mana tukasema hivi sasa kuna malalamiko mengi kuhusu uporomokaji wa maadili katika Taasisi zetu za Serikali. Lakini niwaase kwamba watumishi wajitahidi sana wasiwe wanalalamika sana kuhusu maslahi lakini pia ile *output* yao ionekane.
Lakini vile vile hata sisi viongozi kama hotuba ya Mhe. Mwenyekiti wangu alivyosema hapa kwamba tunasubiri kwa hamu ule Mswada wa Maadili ya Viongozi kwa sababu hivi sasa inaonekana kama wengine kama tunatoka nje ya njia tunatukanana wakati mahala pa kusemana pako. Kwa hiyo Mhe. Mwenyekiti, kwa ujumla niseme kwamba Watumishi pamoja na Viongozi tuwe na maadili ya kazi.

Mhe. Mwenyekiti, chengine ambacho nilichokuwa nataka kuchangia ni Chuo cha Utawala wa Umma. Niipongeze kazi nzuri inayofanywa na Chuo ya kutoa mafunzo kiutawala na kiutendaji katika sekta za umma na binafsi ili kuwajengea uwezo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa hili naomba nitoe wito kwa ndugu zangu wa kike, dada zangu na hata mama zangu kujitokeza kwa wingi hasa wale waliomo katika utumishi kutumia fursa hii inayotolewa na Chuo cha Utawala wa Umma kuendelea kujifunza na kuendelea katika chuo hiki ili tusiachwe

nyuma. Mhe. Mwenyekiti sababu ya kusema hayo nilikuwa naangalia viambatanisho mbali mbali ambavyo vinaonesha watumishi waliopata mafunzo mbali mbali kwa mwaka 2012/2013, na muhtasari mzima umesema kwamba watumishi 243 wamepatiwa mafunzo wanawake 104 na wanaume ni 117.

Mhe. Mwenyekiti, sio hatua mbaya ambayo tumepiga lakini *still* nilikuwa naomba bado wanawake wajitokeze sana na waombe nafasi katika chuo ili waweze kujienedeleza.

Mhe. Mwenyekiti, katika chuo hiki pia kulikuwa na kilio cha muda mrefu sana kama nilivyosema kwamba mimi nitagusia yale maeneo ambayo yanaonekana hayajafanyiwa kazi kwa muda mrefu na kilio hichi kilikuwa ni cha mishahara ya walimu wa chuo hichi. Na katika hotuba zetu mbali mbali za kamati ya Katiba na Sheria iliyopita na ya sasa hata hii iliyosomwa leo na Mhe. Mwenyekiti. Ilisema Serikali itafanya marekebisho ya mishahara ya walimu wa chuo ili wawe sambamba na wale wenzao wa vyuo vyengine vya Serikali kama Chuo cha Habari na vyuo vyengine.

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na malalamiko hayo naipongeza Serikali kwa hatua ya muda mfupi ambayo imechukua ya kuongeza maposho ya walimu wale. Lakini Mhe. Mwenyekiti, mishahara ndiyo inayowasaidia watumishi wale. Kwa hiyo, nimuombe sana Mhe. Waziri alifanyie kazi suala hili ili tuone kwamba wale walimu wanaosomesha pale wawe na mishahara sambamba na ile walimu wa vyuo vyengine vya Serikali.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kumalizia hili la jumla na naiomba Serikali kwamba ilifikirie suala zima la kuanza ujenzi wa jengo la Wizara hii. Mhe. Mwenyekiti, wizara hii kwa kweli ina ufinyu wa nafasi, lakini mbali ya ufinyu wa nafasi hiyo nafasi ambayo inapatikana kuna baadhi ya ofisi zinavuja. Lakini hasa niongelee hili la ufinyu wa nafasi, ni aibu Mkurugenzi mzima ana- *share* ofisi ya sekretari wake. Kwa kweli ni aibu kwa taasisi ya Serikali nzima.

Kwa hiyo, nilikuwa naomba sana, najua sasa hivi kuna ujenzi wa majengo mengine ya Wizara za Serikali ambayo yanaendelea. Lakini niiombe sana Serikali ilifikirie hilo kwani haileti picha nzuri wala kazi haziendi kwa ufanishi kwamba Mkurugenzi mzima ana-*share* ofisi na sekretari wake, kwa hiyo *at least* apatiwe pahala faragha ambapo anaweza kufanya kazi zake. Lakini mbali ya kazi Mhe. Mwenyekiti, hata aseme kuwa atake kupumua pia hawezi maana ndio yuko chumba kimoja na sekretari wake.

Kwa hiyo, Mhe. Mwenyekiti, naomba sana Serikali ilifikirie hilo wizara hii jengo lake halitoshi lakini pamoja na kuwa halitoshi linavuja, kwa hiyo lifikirie suala hili *at least* waanze taratibu za kuanza ujenzi wa jengo la wizara hii.
Mhe. Mwenyekiti, baada ya kusema machache kama nilivyosema mwanzo mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Katiba na Sheria sitokuwa na mengi, mengi yamesemwa na Mwenyekiti katika hotuba ya kamati ile.

Kwa hiyo, baada ya kusema hayo naunga mkono hoja na naomba Wajumbe wenzangu wajadili bajeti hii lakini pia waunge mkono bajeti hii ahsante.

Mhe. Asha Abdu Haji: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kwa kunipa nafasi hii.
Kwanza kabisa napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa afya njema jioni hii.

Pili napenda kumpongeza Mhe. Waziri na watendaji wake wote kwa kutuandikia bajeti hii kutuletea hapa ili tuweze kuijadili.
Mhe. Mwenyekiti, ukurasa wa 58 kuna wafanyakazi 13 ambao wamefukuzwa kazi kutokana na ukosefu wa nidhamu. Je, Mhe. Waziri namuuliza watu hawa kwanza aliwaonya na ikiwa amewaonya na ikiwa amewaonya basi amewaonya mara ngapi watu hawa na ikiwa amewafukuza kazi, je mafao yao atawalipa na watu hawa wako katika fani gani, na ni wa aina gani wanawake wangapi na wanaume wangapi.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa wizara zote ajira zao lazima zipitie kwenye Utumishi wa Umma ni sababu zipi zinazopelekea kutosikiliza maelekezo kutoka wizara husika? Mfano wizara ya Elimu, Afya na kadhalika. Wizara hizi zitapeleka watu wao ikiwa Wizara ya Afya itapeleka watu wao hawa tayari kwa ajira ikiwa watu 10 wataruhusiwa 3 ikiwa Wizara ya Elimu ikiwa watu 20 watachukuliwa watu 5. Je, hii ni haki? Na watu hawa wenyewe wameshaona kwamba hawa wana sifa tayari kwa ajira wakipelekwa kule hawawachukui wanawachukua wanaowataka.
Mhe. Mwenyekiti, tulipotembelea katika kamati Wizara ya Fedha ilisikitika sana, Mhasibu Mkuu wa Serikali alisikitika sana amepeleka watu 100 na hayo tayari kwa ajira wahasibu na hepu hepu yao wamepelekewa watu 4 sio 25 sio 20 wamepelekewa watu 4. Je, hili si tatizo? Ikiwa ni tatizo hulioni kwamba ni tatizo kubwa. Ikiwa watu wao wameshapeleka 100 wana ukosefu wa wahasibu wanapelekewa watu 4 hili hulioni kwamba ni tatizo.

Mhe. Mwenyekiti, kuna taasisi za Serikali ambazo zina uhaba wa wafanyakazi, lakini Utumishi wa Umma bado nafasi hizi hazijazwi katika

nafasi sawa na Halmashauri za Wilaya hazina wanasheria lakini haziajiriwi kwa sababu zipi ambazo haziajiri wanasheria.

Mhe. Mwenyekiti, huoni kuna Halmashauri inafanya kazi zao bila ya kupata wanasheria. Huoni kwamba Halmashauri zinafanya kazi zao kwa kubahatisha kwa kukosa wanasheria.
Mhe. Mwenyekiti, kwa machache naunga mkono asilimia mia moja.

Mhe. Mohammed Mbwana Hamad: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nachukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu *subhana Wataala* kutujaalia jioni hii kuwepo hapa kutekeleza majukumu yetu ya kitaifa. Pia tukiwa katika hali ya afya njema.

Lakini la pili nachukua nafasi ya kumpongeza Mhe. Waziri wa Utumishi wa Umma na Utawala Bora jisni alivyowasilisha hotuba yake kwa ufasaha na kwa umakini wa hali ya juu. Lakini pia nitakuwa mchache wa fadhila sana kama sikumpongeza Mhe. Fatma Mbarouk Said kwa niaba ya Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwasilisha hotuba ya Mwenyekiti wa *PAC* kwa uchangamfu na ufasaha wa hali ya juu kabisa.

Baada ya pongezi hizo nianze mchango wangu katika ukurasa wa 33 wa kitabu hichi kiliopo mbele yetu.
Mhe. Mwenyekiti, ukurasa wa 33 Idara ya Nyaraka na Kumbukumbu za Taifa. Naomba kunukuu: Idara hii ina majukumu ya Kuhifadhi Nyaraka muhimu za historia na kutoa huduma za utafiti na kadhalika.
Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli idara hii ni muhimu sana kwa sababu kumbukumbu za taifa ndio roho ya taifa. Taifa linapokosa kumbukumbu kwa kweli linakuwa linafanya mambo yake kwa kubahatisha tunajua kama pale kuna mambo ya historia karne kwa karne zilizopita kutotunzwa kwa ufanisi kwa kweli kunaweza kupelekea kukosa hata uelewa wa kujua vitu vyetu muhimu na mambo yetu muhimu yaliopo katika nchi yetu ya Zanzibar.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa pale ni pahali ambapo panatunzwa vitu muhimu. Sasa kitu muhimu zaidi cha kuwepo pale nakuomba Mhe. Waziri kuwepo na kifaa cha kuzuia unyevu kwa sababu baridi ya *air condition* inaweza kusababisha kuharibika kwa nyaraka zile. Kwa hivyo, kama kifaa hicho kipo *fahuwal-murad* lakini kama kifaa hiki kama hakipo kiwepo ili kumbukumbu zetu ziweze kudumu vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hapo niende moja kwa moja mpaka Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu Serikali. Mhe. Mwenyekiti, ofisi hii ni muhimu sana kwa sababu ndio inayoidhinisha matumuzi ya Serikali baada ya kupitisha Bajeti na Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza naipongeza Ofisi kwa kuwaendeleza watendaji wake nafikiri hapa sehemu ya 107 inaeleza kwamba:
"Ofisi imeendelea kuwawekea mazingira mazuri watumishi wake ambapo ada ya masomo pamoja na gharama nyengine zimelipwa kwa wafanyakazi 13 waliojiunga na vyuo 2012/2013 na wafanyakazi 17 wanaendelea na masomo yao ya muda mrefu katika vyuo mbali mbali".

Naipongeza sana Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu kwa ajili ya kuwaendeleza wafanyakazi wake ili upatikane ufanisi wa hali ya juu. Lakini Mhe. Mwenyekiti, niseme kwamba ofisi hii miongoni mwa majukumu iliyopewa ni kuzikagua Taasisi za Serikali na kuangalia muenendo mzima wa matumizi kwa fedha walizoingiziwa.

Lakini masikitiko yangu makubwa kuna ripoti nyingi za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ambazo zinawasilishwa katika Baraza la Wawakilishi katika vitabu mbali mbali vya miaka mbali mbali lakini ripoti ile inamalizia katika vitabu tu. Nimuulize Mhe. Waziri wa Utumishi wa Umma na Utawala Bora ni lini watendaji wa Serikali ambao wanakwenda kinyume na taratibu na sheria za fedha wanachukuliwa hatua za kinidhamu.

Mhe. Mwenyekiti, nikiangalia ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya mwaka 2010/2011 humu mna maelezo kadhaa kuna maelezo mengi. Kuna mambo mengi ambayo yamekwenda kinyume na taratibu lakini hatua yoyote Serikali inayochukua juu ya watumishi hawa ambao wanaharibu mali za serikali.

Mhe. Mwenyekiti, nataka nitoe tu baadhi ya *sample* ya matatizo ambayo yanajitokeza katika ubadhirifu ndani ya vitabu hivi ambavyo kila mwaka Mdhibiti na Mkaguzi anavitolea taarifa. Nikichukua kitabu hichi cha 2010/2011 cha Mdhibiti ukurasa wa 51 kuna Shirika la Bima la Zanzibar ufungaji wa hesabu za mwisho wa mwaka 2010/2011 Shirika la Bima la Zanzibar halikuwasilisha hesabu zake za mwisho wa mwaka kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu kwa ajili ya kufanyiwa ukaguzi, kwa vile ukaguzi wa hesabu hizo haukufanyika itakuwa vigumu kuweza kutoa maoni kuhusu hesabu pamoja na hali halisi ya fedha za Shirika.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, nikienda katika Shirika la huduma za Maktaba halikuwasilisha hesabu zake za mwisho wa mwaka kwa Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali, na tatizo hilo hilo liko Shirika la Umeme. Shirika la Umeme Zanzibar halikuwakilisha hesabu zake za mwisho wa mwaka, nikienda Shirika la Utalii halikuwasilisha hesabu zake za mwisho wa mwaka,

na Shirika la Meli na Uwakala pia halikuwasilisha hesabu zake za mwaka hili ni tatizo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu tunazungumzia suala la Utawala Bora na Utumishi wa Umma malengo ni kwamba watumishi wetu waweze kufuata taratibu za kiserikali zilizowekwa. Sasa basi kwa kuwa kuna mwaka wa hesabu sijui kuna watu wanaanza sijui tarehe ngapi na ngapi na wengine wanakwenda mwezi gani mpaka mwezi gani. Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri atakapotoa majumuisho anieleze kwa kina wizara ngapi au taasisi gani zina mpango huu wa kuwasilisha mahesabu yake na taasisi gani na gani zina mpango mwengine wa kuwasikilisha mahesabu yake.

Lakini tukienda katika Mabaraza ya Mji huku ndiko kunako uoza. Mhe. Mwenyekiti, tunaomba katika Mabaraza ya Mji na Halmashauri wapelekwe waajiriwe vijana wenye sifa za kuweza kutunza mahesabu na kuweza kukamilisha matakwa ya kisheria katika taasisi wanazozifanyia kazi.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli nasema kwamba Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anajitahidi kufanya kazi yake lakini kazi hiyo inagonga mwamba kwa sababu ya kukosa meno. Baada ya ripoti ya Mkaguzi au ripoti hizi za mkaguzi yeye kazi yake imemaliza. Kwa hivyo, nafikiri wizara inayohusika itwambie ni nani wa kulaumiwa katika ubadhirifu wa fedha hizi za Serikali na fedha za Mashirika ya Umma.

Nikiondoka hapo niende hapo hapo katika Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wanasema kwamba katika nukta ya 109. Vile vile kufanya matengenezo makubwa ya jengo la Ofisi lilioko Pemba. Mhe. Mwenyekiti, kila siku tutakuwa tunatumia pesa kwa kutengeneza majengo ambayo labda hayakidhi haja.

Kwa sababu Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali wana kiwanja pale Pemba Tibirinzi kwa nini Serikali kwa kupitia Wizara hii haijaamua kwa makusudi kujenga Ofisi ambayo itakidhi haja kuliko kila siku kutoa mapesa mengi kwa kutengeneza matengenezo makubwa. Mhe. Mwenyekiti, niiombe Ofisi ya Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais suala la kujenga jengo la Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali pale Pemba lipewe nafasi kubwa.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya hapo niende katika ukurasa wa 69 unahusiana na masuala ya maendeleo na maslahi ya wafanyakazi, niende katika nukta ya 159 Mhe. Mwenyekiti, nanukuu:

"Baada ya kukamilika zoezi la kuwapanga watumishi kwa madaraja yao kwa mujibu wa miundo ya Utumishi, Serikali kwa mwaka wa 2013/2014

imepanga kufanya marekebisho ya maslahi ya watumishi wa umma ambapo itazingatia vigezo mbali mbali ikiwemo uzoefu wa utumishi.

Mhe. Mwenyekiti, mara nyingi katika Bajeti ya Serikali Waziri hueleza ni asilimia ngapi kwa watu wa kiwango fulani cha mshahara wataengezewa hapa Mhe. Waziri ametueleza kifumbo fumbo. Kwa hivyo, tunamuomba Mhe. Waziri atueleze ni asilimia ngapi ya wafanyakazi mwaka huu wakajisikia.

Mhe. Mwenyekiti, katika maelezo ya maslahi ya wafanyakazi namuomba Mhe. Waziri awaangalie wafanyakazi ambao wanafanya kazi katika mazingira magumu kuwapatia posho maalum kwa ajili ya mazingira magumu.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka nikwambie kitu kwamba jana tuliondoka hapa karibu saa tano za usiku, kwa kweli ni tatizo Waheshimiwa wengi wana magari yao, lakini wafanyakazi wa Ofisi ya Baraza la Wawakilishi wengi wao hawana usafiri, na jana usiku kuna mfanyakazi mmoja wa Baraza la Wawakilishi wamemshambulia jamaa. Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, nakuomba uweke posho maalum kwa mazingia magumu.

Lakini la pili kwa sababu tuko katika Utawala wa Umma na Utumishi Bora kuongeza wakati zaidi ya saa tatu ni tatizo. Kwa hiyo, Mhe. Mwenyekiti, nakuomba ikiwa mazingira yetu yatakuwa yanaweza yakahatarisha mwenendo wa wafanyakazi wetu kutoka hapa zaidi ya saa tatu basi tutafute mbinu yoyote ya mbadala tumalize shughuli zetu katika usiku wa mapema na baada yake isizidi mpaka saa tano za usiku kwa kweli hili ni tatizo. Mhe. Mwenyekiti, tuzingatie kwa kina kwa sababu wenzetu wanakaa katika mazingira magumu.

Mhe. Mwenyekiti, naona unaniwashia taa, kwa hiyo pamoja na mtaa yako naiheshimu nasema kwamba nashukuru kwa kunisikiliza kwa makini nasema ahsante sana kwa kunipa nafasi hii. (*Makofi*).

Mhe. Asha Bakari Makame: Mhe. Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa na mimi kuchangia wizara nyeti ambayo ndio uti wa mgongo wa wafanyakazi na wakulima.

Lakini pia Mhe. Mwenyekiti, nichukue nafasi hii nimpongeze sana Mhe. Waziri ambaye kitabu chake kimepangika vizuri na namna ya utekelezaji wake. Lakini niseme tu hakuna kizuri kisicho na ila. Itabidi lazima tutoe yale mambo ambayo kwa kumsaidia yeye mwenyewe binafsi akiondoka hapa na kwenda kuyatekeleza.

Kwanza Mhe. Mwenyekiti, kwanza mimi kama mwanamke nimpongeze sana mwanamke ambaye ni Ofisa katika Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ni tabu sana kuweza kuwapata kinamama kama hawa. Kwa hivyo, nichukue nafasi hii binafsi kumpongeza kwa kazi zake nzuri ambazo anazifanya na jitihada zote anazozifanya. Kwa hivyo, niseme kwamba nimuombe Mhe. Waziri ampe mashirikiano ya hali ya juu ili kuweza kufanikisha malengo ambayo Serikali yetu imemtuma.

Mhe. Mwenyekiti, niwaombe na wafanyakazi wa ofisi hii pia wampe mashirikiano na nahakikisha mashirikiano wanampa maana asingeweza kuzimudu kazi zake vizuri. Kwa hivyo, nimuombe Mhe. Waziri tena nimuombe sana huyu mama naye ashirikiane naye kwa mambo yote ambayo yanamtatiza hii yote ni kumsaidia Waziri wake kazi azikamilishe kikamilifu.

Nikieondoka hapo Mhe. Mwenyekiti, nije katika maslahi ya walimu. Mhe. Mwenyekiti, sisi sote humu tuliomo humu huu Uheshimiwa tusingekuwa nao kama si taaluma walizotupa walimu wetu huko tunakotoka. Ualimu Mhe. Mwenyekiti, ni kazi ngumu sana, ni kazi ambayo uwe na stahamala uwe na ukweli na uhakikishe kwamba unapata dhima kwa Mwenyezi Mungu kama hukuwafundisha watu ambao wakaweza kufanikisha shughuli zao.

Kwa heshima kubwa nimuombe Mhe. Waziri kama kuna mategemeo ya kuongezwa au hakuna basi awape kipaumbele walimu. Hawa kila mwaka tunawaombea kwa sababu wana kazi ngumu.

Lakini jengine zaidi nimuombe Mhe. Waziri hebu aje anifahamishe kabla Wizara ya Elimu haijaingia kueleza, kuna vijana wetu ambao wanajenga taifa anaona hana kazi lakini ajenge taifa kusaidia pale mtu anapoishi, lakini wanajenga taifa mtu anakwenda halipwi na anasomesha kwa mwaka mmoja, matokeo yake akiomba kazi Mhe. Mwenyekiti, haajiriwi ushahidi mimi ninao kamili. Kwa hivyo, ninamuomba Mhe. Waziri hebu atufafanulie haya kulikoni kuna nini huko.

Mhe. Mwenyekiti, nikiondoka hapo niende kwa madaktari na wauguzi. Daktari kama hakupata msaidizi basi udaktari wake haukamiliki. Mhe. Mwenyekiti, namuomba sana Mhe. Waziri kama kuna ongezeko la kuhakikisha kumuongeza daktari, basi asimuongeze daktari tu peke yake, hapa nasema amuongeze daktari pamoja na wale wafuasi ambao wanamsaidia daktari. Kwa kweli hawa wenzetu ukienda hospitali kazi ipo, utamuona mtu anakaa tokea asubuhi ndio huyo huyo hana *shift* wala hana chochote, anasema siwezi kuondoka. Kwa hivyo, naomba sana Mhe. Waziri kuna watu wa vipaumbele maalum, pamoja na hao walimu, madaktari na wauguzi basi na wao wapewe kipaumbele kwa sababu wana kazi kubwa.

Nikiondoka hapo Mhe. Mwenyekiti, nimpongeze Mhe. Waziri, *'maana mtu lake mpe'* nimpongeze kwa kuhangaika na kutafuta pesa kwa ajili ya kupata semina ya Muundo wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa, kwa sababu kila nikisimama hapa nilikuwa nazungumzia suala la kupatiwa semina kujua maana ya Serikali ya Umoja wa Kitaifa ni kitu gani, maana yake naona sasa kuna mchafukoge.

Namuomba sana Mhe. Waziri hizo fedha zikipatikana tu utuhakikishie kwamba unatuletea semina hizo mpaka akili zetu zifunuke zaidi, tujue Serikali ya Umoja wa Kitaifa ni nini na nini, ili tusije tukarudi tulikotoka. Maana yake naona sasa hivi kidogo damu inachemka. Kwa hivyo, kabla haijachemka ikafurika damu ya mwilini ikapasuka ikamwagika huko basi tuweze kudhibiti.

Mhe. Mwenyekiti, nikiondoka hapo nimpongeze Mhe. Waziri katika ukurasa wa 25 kifungu cha 52 kwamba kuna watumishi zaidi ya mia nne walitarajiwa kustaafu katika kipindi cha mwaka unaokuja, lakini akaona ni vyema watumishi hawa awapangie mipango ya kuweza kuwasaidia wakati wanapostaafu ili tuondokane na ile dhima ya kwamba mtu akishastaafu basi siku mbili au ya tatu utamuona yuko hoi bin taaban. Kwa hivyo, hapa nimpongeze kwa dhati kabisa kwa watu hawa 449 na isiwe ni hawa tu, kwa kila kipindi kinachopita wanaostaafu basi wapangiwe mipango kama hii ili kuhakikisha watu wetu wanaendelea na kujinasua wao wenyewe kiuchumi.

Mhe. Mwenyekiti, nadhani nililizungumzia sana suala la kujengwa ofisi za wizara mbali mbali. Mhe. Waziri katueleza humu kwamba kuna ujenzi wa nyumba za serikali. Mimi ninamuomba Mhe. Waziri. Narudia tena kuwa tuige wito wa Marehemu Karume, Mwenyezi Mungu amrehemu aliko. Tukianzisha kitu Unguja basi na Pemba kianzishwe, tukianzisha chochote kile ambacho kina manufaa kwa wananchi basi na Pemba tuanzishe, kwa sababu huko nyuma Marehemu Mzee Abeid Aman Karume alituzoesha vibaya. Alikuwa akijenga majumba ya Michenzani basi na Pemba anatia jiwe anamaliza na Unguja inamaliza, nyumba za vijijini zinajengwa na kule zinajengwa, viwanja vya watoto kimejengwa Unguja na Pemba kimejengwa. Yale yote ni mambo ya maendeleo ambayo alikuwa akiyafanya Marehemu Karume hapa Unguja basi na Pemba alikuwa anafanya.

Kwa hivyo, naiomba serikali kwa kupitia hili Baraza la Wawakilishi naomba sana jambo tukianzisha Unguja basi na Pemba tuanzishe, tuwape raha na wao kisiwa cha pili, wajione kwamba Pemba na wao wana haki ya kila aina kinachofanywa Unguja. Sisemi haya kwa sababu mimi ni Mpemba, lakini nayasema haya kwa sababu ni maendeleo ya wananchi wa Zanzibar.

Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, namuomba sana Mhe. Waziri na sio waziri huyu tu, kama walivyoshirikiana hapa wizara tatu kujenga nyumba moja, basi na kule washirikiane, kwa sababu tunapoteza fedha nyingi sana kwa kukodi nyumba za watu binafsi. Ukizifanyia hesabu Mhe. Mwenyekiti, fedha tunazokodi nyumba basi ni mamilioni ya fedha. Kwa nini hatuchukui mradi na sisi tukajenga nyumba. Pemba zikijengwa nyumba tatu tu basi ofisi zote zitaenea, hebu fanyeni ari mjenge nyumba tatu tu za ofisi kama mawizara mengine. Hebu fanyeni ari, tubadilike, tujenge nyumba kule za ofisi ili na wao wajisikie. Majengo tunayokaa Mhe. Mwenyekiti, ni mabovu mengine.

Mfano jengo la majenzi wewe mwenyewe ukipanda pale unaona wasi wasi. Kwa hivyo, naomba sana Mhe. Waziri, muambizane kwenye *cabinet* kwamba umefika wakati sasa wa kubadilika, turudi lile jema liigwe turudi kwenye mfumo wa Marehemu Karume ili tuwape wananchi raha kama nyinyi. Baada ya kusema hayo Mhe. Mwenyekiti, nichukue nafasi hii kusema kwamba ujenzi huu wa nyumba Mhe. Waziri utakuja kuniambia kuwa utaanza lini Pemba kabla hapajamalizika hapa. Maana hapa naona tayari mambo basi kabla hamjahamia hapa na ujenzi wa Pemba uanze, si hivyo bajeti hii uje uniambie ni lini itaanza, hii nitakuachia lakini inayokuja nitakunyang'anya mshahara. Nachukua mshahara wako, basi utajiju! *(Makofi).*

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kusema hayo nikushukuru tena wewe binafsi kwa kunipatia nafasi hii na nasema pamoja na ukali wote niliosema hapa naunga mkono hoja. Lakini aje anipe maelezo mazuri katika uchangiaji wangu ambao nimeuchangia hapa. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mohamed Haji Khalid: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kupata nafasi kutoa machache juu ya wizara hii muhimu kwa watumishi na watendaji wa serikali. Kwanza nikupongeze wewe binafsi. Pili nimpongeze Waziri kwa umahiri wake na usomaji wake mwema na niwapongeze wale wote alioshirikiana nao katika kutengeneza taarifa hii ya bajeti ya wizara yake kwa mwaka huu wa 2013/2014.

Mhe. Mwenyekiti, kabla sijatoa mchango wangu naomba niseme jambo moja. Kwa kweli tumekuwa na mtindo ambao umeshakuwa ni wa kudumu wa kuongeza muda bila ya mpaka, kiasi bajeti mbili zilizopita tunafanya kazi ya siku mbili kwa siku moja, na muda tunaoongeza ni zaidi ya ule muda wa kawaida. Ningeomba suala hili tulitizame kidogo, kuna taarifa ambayo sijaithibitisha kuwa jana yuko mfanyakazi wetu mmoja alipata matatizo kidogo kwa kuondoka usiku mkubwa kama tunatoka katika vilabu kulichangia suala hilo. Kwa hivyo, tunaomba tunapoongeza muda basi ule muda tunaoongeza uwe una mpaka, usiendelee tu kuwa lazima bajeti

imalizike kwa nguvu, lakini na muda tuujali ili tuwajali watendaji wetu kule tunakokwenda.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya utangulizi huo mimi mchango wangu ni mdogo sana, nitaanza kwenye idara ya uendeshaji na utumishi lakini kifungu kidogo kinachoanza na utoaji wa ajira. Mhe. Mwenyekiti, wizara hii na idara hii ni kama moyo kwa hii serikali, kwa sababu watumishi wote wa umma hiki ndio kioo chao na hapa ndio kwenye mtazamo wao. Jinsi wizara hii itakavyokuwa na ufanisi katika utendaji wake na ndivyo watendaji na watumishi wa umma watakavyokuwa na ufanisi na wao katika utendaji wao wa kazi.

Mhe. Mwenyekiti, ajira ya serikali katika nchi yetu inaonekana kuwa ni ngumu kidogo na zile za sekta binafsi nazo pia bado hazijajengewa uwezo wa kuweza kuwaajiri vijana kwa wingi. Lakini pale ambapo nafasi zinatokea kuwaajiri vijana wetu katika sekta zetu za serikali, tunaomba waajiriwe vijana wenye sifa zinazotakiwa zote za kielimu na vipimo vyengine, ili kuondoa matatizo baina ya watu na watu na baina ya vijana na vijana.

Mhe. Mwenyekiti, Zanzibar hali ya maisha ni magumu, na ugumu huu wa maisha ndio unaowafanya vijana wetu watafute ajira kwa hali yoyote ile. Mhe. Mwenyekiti, wakati wangu mimi ajira haikuwa na tabu sana kama hivi leo, ingawaje haikuwa na tija kiasi hicho lakini haikuwa ngumu kama ilivyo leo. Na kwa kipindi hicho watu wenye elimu ndogo kama yangu walikuwa wakijiona kuwa ndio waliosoma na walikuwa wana nafasi kubwa ya kupata ajira. Leo mtu mwenye elimu kama yangu nafasi yake ya kuajiriwa ni finyu mno. Kwa hivyo, hapa nitoe wito kwa vijana kuwa wajitahidi kusoma ili wafikie kiwango cha elimu ambayo ikitokezea ajira iwe kwao haina matatizo makubwa.

Mhe. Mwenyekiti, hapa kuna kijifungu au kuna sentensi inayozungumzia kupandisha vyeo watumishi. Mhe. Mwenyekiti, sehemu nyingi za utumishi wetu hakuna utaratibu maalum unaowekwa wa mtu kupanda vyeo, ukiacha vyeo ambavyo ni vya Mhe. Rais ambavyo anateua mwenyewe, lakini hivi vya ndani vya ofisini ni lazima kuzingatiwe mtu elimu yake, uzoefu wake na pengine umri wake wa kazini, ili kama kupandishwa cheo kuna maslahi basi haitokuwa vyema kuwe kuna mtu ambaye ni mzoefu kwa muda mrefu; elimu anayo, ujuzi anao halafu akawekwa mbele mtu ambaye amekuja jana kwa sababu tu pengine kuna mtendaji katika ofisi ile ni jamaa yake, upandishaji huu uende kulingana na taratibu za kisheria.

Mhe. Mwenyekiti, nizungumzie kwenye uwekaji wa kumbukumbu za watumishi, hili ni jambo muhimu sana. Mimi nimetoka serikalini muda mrefu, lakini wakati huo ambapo mimi nilikuwa ni mfanyakazi wa serikali, basi

kulikuwa kuna utaratibu mzuri sana wa kuwekwa kumbukumbu za kila mfanyakazi. Sijui leo ambapo tumeendelea kiasi hicho na mpaka leo ikiwa kuna watu wanazungumziwa kuwa kuna wafanyakazi hewa. Kama kumbukumbu zipo za utumishi hii hewa inatokea wapi. Anajulikana Mohamed Haji Khalid yupo na kila siku ofisi hii inafanya utafiti wa wafanyakazi wake na kila siku haimalizi na kila siku wafanyakazi hawako, je utafiti huu unafanywaje? Mbona kila siku utasikia kuna wafanyakazi hewa. Nchi iliyokuwa hewani ni ya kusadikika tu, lakini Zanzibar sio ya kusadikika ni nchi ambayo iko ardhini.

Kwa hivyo, wizara hii ijitahidi kuweka kumbukumbu za wafanyakazi wake, ili mfanyakazi yeyote atakapokwenda au anapohitajiwa iwe kumbukumbu zake ni za kuvuta tu na akaelezwa. Kwa mfumo wenu wa kisasa ni kufungua kompyuta akaonekana tu. Kwa zamani ilikuwa faili lake liko hapa linachukuliwa bila ya kutafutwa. Lakini leo inaonekana kumbukumbu ya mtu pengine hata mikataba ya kuajiriwa haijulikani ilipo, hili ni tatizo na lazima twende katika ufanisi. Kwa hivyo, hili ni jambo muhimu la kuweka kumbukumbu za watumishi katika hali iliyo bora zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, wizara hii imezungumzia kuwajengea uwezo na kuwapatia mafunzo wafanyakazi kwa mujibu wa kada zao. Hili ni sawa sawa, kwa sababu Mhe. Mwenyekiti, nimeshuhudia sehemu mbali mbali mtu kasomea kitu chengine, anawekwa kusimamia au kufanya kazi katika *sector* ambayo sio aliyoisomea, hili ni tatizo. Mtu kasomea udaktari anakwenda kuajiriwa pengine Wizara ya Kilimo na Maliasili. Ni lazima ajira zetu twende na zile elimu zetu tulivyozisomea.

Mhe. Mwenyekiti, naona umeniwashia taa haraka sana. Nije katika maslahi ya watumishi. Mhe. Mwenyekiti, haya hayana matatizo. Mimi wakati wangu nilipoajiriwa ule mkataba wangu yaani ulikuwa unanionesha maslahi yangu yatakuwa hapa na hapa, na anayekuja nyuma yangu anafuata hivyo. Wakati ule sisi mkataba wetu ulikuwa unatuonesha sisi walimu wa *primary school* mshahara wako kwa mwezi utakuwa ni shilingi 360, unapata nyongeza ya mwaka ya shilingi 20 halafu shilingi 20 mpaka unafikia shilingi 1,500 hapo unafika kwenye *bar*. Sasa aliyekuja nyuma yako hakukutii. Lakini leo una

Mhe. Mwenyekiti: Una dakika tano za ziada.

Mhe. Mohamed Haji Khalid: Leo mwalimu ambaye kafanyakazi kwa miaka 20 nyuma, tuchukulie ana elimu ndogo ya *form four*, mwalimu *training*, halafu akaajiriwa mwengine mwaka huu basi *rank* ya mapitano yao ni ndogo mno, kwa sababu hakuna *scheme of services* iliyopangwa kuwatofautisha watu hawa wawili. Kwa kweli tunawavunja moyo sana walimu. Kila mtu

aliyepita skuli basi kapita kwa mwalimu, lakini tukishakuwa huku tunawasahau walimu.

Mhe. Mwenyekiti, tuwachukulie walimu ndio walimu wetu, kwa hivyo na wao tujali maslahi yao na wala sio walimu tu, lakini ni watumishi wote ni lazima walipwe kulingana na elimu zao, uzoefu wao na maslahi yao yapangwe wa mbele awe mbele na wa nyuma awe nyuma. Mtu aliyekuwa na elimu ya aina moja na aliyeingia kazini kwa wakati tofauti basi msilingane kabisa katika maslahi yenu ya kila mwezi, hii ni kumvunja moyo aliyetangulia.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya kusema hayo machache, niseme namalizia hapo ahsante sana.

Mhe. Marina Joel Thomas: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, na mimi kwa kunipa nafasi ya kuchangia hotuba hii. Pili nampongeza waziri kwa kazi kubwa na nzuri ambayo ameifanya ya kuandaa hotuba hii ya bajeti na pia nawapongeza watendaji wake wote.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nitachangia katika sehemu tatu. Kwanza Mamlaka ya Kuzuia Rushwa, Idara ya Miundo ya Taasisi Utumishi na Maslahi ya Watumishi, Idara ya Mipango Sera na Utafiti na Sheria ya Maadili ya Viongozi.

Mhe. Mwenyekiti, ninaanza kuchangia katika Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi Zanzibar. Hii ipo katika ukurasa wa 59 katika kifungu cha 34. Mhe. Mwenyekiti, mamlaka ina jukumu la kufanya uchunguzi dhidi ya vitendo vya rushwa na uhujumu wa uchumi hapa Zanzibar. Mhe. Mwenyekiti, tatizo la rushwa kwa hapa Zanzibar limekuwa ni tatizo kubwa. Rushwa imetawala kila sehemu, kuna rushwa ya siri na kuna rushwa ya dhahiri na kuna rushwa ya maneno, kwa hivyo imetanda kila sehemu.

Hapa nilikuwa nataka kumuuliza Mhe. Waziri amejiandaa vipi dhidi ya mamlaka hii kutenda kazi zake ipasavyo. Mamlaka hii itakuwa na majukumu makubwa sana na itapatwa na changamoto nyingi sana, ikiwemo vishawishi ambavyo vitawapelekea na wao wenyewe wakaingia katika kundi la rushwa.

Kwa hivyo, hapa Mhe. Mwenyekiti, nina ushauri kwa Mhe. Waziri mamlaka hii aiangalie kwa kina kabisa kuhusu maslahi yao, mazingira yao ya kazi na tukitaka wafanye kazi zao vizuri, kwa uadilifu, kwa uaminifu na kwa umakini, basi nahisi tungewaweka katika mazingira mazuri kabisa.

Mhe. Mwenyekiti, niende sasa katika Idara ya Miundo ya Taasisi Utumishi na Maslahi ya Watumishi, hii iko katika ukurasa wa 25 kifungu cha 55. Mhe. Mwenyekiti, moja kati ya majukumu ya idara hii ni kusimamia maslahi ya wafanyakazi, kuendeleza na kusimamia mfumo wa malipo ya mishahara ya wafanyakazi.

Mhe. Mwenyekiti, kila mfanyakazi ana umuhimu wake katika kazi kwenye taasisi au wizara. Hata yule muhudumu anayefagia na yeye ana umuhimu wake. Siku moja tu mfano asije yule muhudumu ofisi isisafishwe basi ni tatizo. Kwa hivyo, kila mfanyakazi ana umuhimu wake katika kitengo chake. Hapa nitazungumzia suala la watumishi au wafanyakazi wale wa muda mrefu ambao kimaslahi yao yanakuwa ni madogo, hawana elimu au elimu yao ni ndogo, lakini wamefanya kazi kwa muda wa miaka 20 au 30, lakini ana umuhimu katika *sector* husika na analeta tija katika taasisi husika. Kwa hivyo, wafanyakazi hawa Mhe. Waziri nakuomba uwatizame kwa jicho la huruma kabisa ni watu ambao ni wa umuhimu katika *sector* mbali mbali.

Mhe. Mwenyekiti, nikiangalia katika *sector* ya afya, maslahi ya *sector* ya afya nayo uyaangalie Mhe. Waziri ambayo ni muhimu, kwa sababu *sector* hii ndio inayotuletea wafanyakazi waliokuwa na afya njema na siha safi kabisa. Bila ya afya, bila ya siha basi utakuwa huwezi kufanya kazi vizuri. Kwa hivyo, waangaliwe na hawa na hasa wale wa ngazi za chini kabisa wauguzi, wahudumu. Hao wengine wenye elimu zao tunajua wana ziada zao za mishahara, lakini na wao pia waangaliwe. Kwa sababu kuna miaka mitatu au minne nyuma kulitokea wimbi kubwa la wafanyakazi wa Wizara ya Afya walikuwa wanaondoka na kuhamia sehemu nyengine ambazo zilikuwa na maslahi zaidi. Pengine nchi za nje au Tanzania Bara, hii imetokana na maslahi yao madogo na hii nayo tuiangalie katika *sector* hii Mhe. Waziri.

Mhe. Mwenyekiti, pia niende kwenye *sector* ya elimu ambayo ni muhimu, kwa sababu *sector* hii ndio inayowajenga vijana bora ambao ndio watakuja kuwa wataalamu, watakujakuwa madaktari bingwa na watakujakuwa walimu wa vyuo mbali mbali. Kwa hivyo, tuwaangalie walimu nao katika *sector* hii, kwa sababu walimu wana kazi nzito katika jamii. Walimu wana kazi ya kujituma na ni kazi ya kujitolea, kuna walimu ambao mishahara yao ni midogo kabisa, kuna walimu wengine pengine maposho yao ni madogo kabisa. Mhe. Waziri nakuomba kwa dhati kabisa uwaangalie walimu hasa walimu wa skuli za kawaida na hata kwenye vyuo.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, nitakwenda katika Idara ya Mipango Sera na Utafiti. Idara hii ina jukumu la kutayarisha na kuzifanyia mapitio sera na kufanya tafiti. Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri wizara yake inashughulikia watumishi wote wa umma, watumishi wa kutoka wizara tofauti, lakini sasa

kuna watumishi ambao wamekwenda kusoma katika vyuo mbali mbali vya nje na ndani ya nchi. Watumishi hao wanaposoma kuna sehemu ambazo wanafanya utafiti. Kwa hivyo, naomba nimuulize Mhe. Waziri wale wanafunzi wote ambao wamesoma na baadae wakafanya utafiti je, wizara yako ina kitengo maalum cha kuzihifadhi zile tafiti zote za wanafunzi hao waliosoma ndani na nje ya nchi. Nasema hivyo kwa sababu utafiti ni kumbukumbu nzuri ambayo itasaidia serikali na hata wanafunzi wengine watapata kumbukumbu za kufanya katika masomo yao.

Kwa hivyo, kama huna kitengo hicho, labda nikushauri kwa kushirikiana na Mhe. Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali, pale maktaba kuu muzichukue kopi zote za tafiti za wanafunzi mbali mbali waliofanya utafiti ndani na nje ya nchi, iwe kama ni kitengo mukiweke pale ili kiweze kuwasaidia hata na wanafunzi wetu wapya ambao ni chipukizi wanaotarajia kusoma hapo baadae.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo ninakwenda kwenye Sheria ya Maadili ya Viongozi. Kwanza napenda kuipongeza wizara kwa
kuandaa sheria hii, ambayo itasaidia kudhibiti viongozi mbali mbali ambao pengine si waadilifu katika kutekeleza majukumu yao.

Kwa kweli uzoefu ni kwamba kuna baadhi ya wafanyakazi au viongozi wanafanya kazi kwa uzoefu, lakini pengine wanafanya kazi nje ya taratibu na sheria zilizowekwa, akijua kwamba hakuna sheria yoyote ambayo itakayonifunga. Kwa hivyo, kuwepo kwa sheria hii itasaidia kuwadhibiti hata viongozi ambao wanaovunja taratibu za nchi, wanakula rushwa na hii ndiyo itakuwa sheria itakayowadhibiti hao.

Baada ya kusema hayo, Mhe. Mwenyekiti naunga mkono hoja. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, ahsante. Sasa ni zamu ya Mhe. Salmin Awadh Salmin na baadaye ni Mhe. Hija Hassan Hija.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Mhe. Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii, ili na mimi niweze kuchangia Hotuba ya Mhe. Waziri wa Nchi, (OR), Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Kwanza naanza mchango wangu kwa kusema kwamba siungi mkono hoja hii. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kwa kutumia Kanuni ya 98(6) (e) naomba kunukuu kidogo.

Kanuni ya Baraza la Wawakilishi kifungu cha 98(6) (e) kinaeleza hivi:-

> “Nakusudia kupunguza shilingi mia moja ikiwa ni ishara ya kutoridhika na sera ya jambo maalum lilioko chini ya usimamizi wa wizara au idara inayohusika”.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kutumia kifungu cha 6(c) cha Kanuni ya Baraza la Wawakilishi, Mhe. Mwenyekiti naomba kunukuu kidogo.

Kanuni ya Baraza la Wawakilishi kifungu cha 6(c) kinaeleza hivi:-

> “Nakusudia kutoa fungu hilo kutokana na kutoridhishwa na utekelezaji wa Kamisheni ya Utumishi wa Umma”.

Kwa maana hiyo, nitazuia fungu 47 mpaka hapo Mhe. Waziri atakaponipa maelezo ya kutosha, kwamba ni sababu zipi zilizopelekea kushindwa Kamisheni ya Utumishi kuthibitisha muundo uliopelekwa na Tume ya Utumishi ya Baraza la Wawakilishi hadi kufikia miaka miwili sasa. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nataka ninukuu sehemu ya Hotuba ya Mhe. Rais wa Zanzibar na wakati alipokuja kulizindua Baraza hili. Kwa hivyo, sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi hotuba ile tuliichukulia kama ni dira na miongozo ya Mhe. Rais katika kutekeleza majukumu yake katika kipindi chote cha miaka mitano atakayokuwepo madarakani. Mhe. Mwenyekiti, sehemu ya hotuba hiyo ya Mhe. Rais naomba kuinukuu.

Sehemu ya Hotuba ya Mhe. Rais (*Hansard*) inaeleza hivi:-

> “Kila wizara itawajibika kuwa na mpango wake wa mafunzo kwa wafayakazi na mafunzo ya mpango unaofahamika, ambao unapaswa utekelezwe kwa ajili ya mafunzo ya muda mrefu, mfupi na muda wa kati, ili kuwapa nyenzo na uwezo wafanyakazi kuyafahamu maeneo yao ya kazi na kutumika ipasavyo.
>
> Maslahi bora ya wafanyakazi popote pale ni ajenda yetu na tunaimarisha mashirikiano na chombo chao na vyombo huru vya wafanyakazi, ili kukuza mahusiano yaliopo.
>
> Katika kuendeleza wafanyakazi serikali yangu itaimarisha mazingira bora ya kazi na maslahi ya wafanyakazi kwa kadri hali ya uchumi wetu na kadri ya uchumi unavyoimarika.

> Suala la miundo ya utumishi (*scheme of service*) itashughulikiwa kwa kadri ya kada za utumishi zilizopo. Tunayo nia katika serikali yangu ya kuanzisha Wizara ya Utumishi wa Umma, ambayo pamoja na mambo mengine itahusika na mambo yafuatayo, ameyataja haya mambo ambayo Wizara ya Utumishi wa Umma itahusika". *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kwa kutumia dira hii ya Mhe. Rais, Ofisi ya Baraza la Wawakilishi ilipeleka mapendekezo kwa Tume ya Utumishi ya Baraza la Wawakilishi juu ya muundo wa chombo hichi cha Baraza la Wawakilishi.

Kwa mujibu wa sheria na Katiba Tume ya Utumishi ya Baraza la Wawakilishi imeridhia na imekubaliana na muundo ule na hatimaye kuiwasilisha Kamisheni ya Utumishi wa Umma kwa kuuthibitisha na hilo ndilo jukumu la Tume ya Utumishi katika maeneo haya. Mhe. Mwenyekiti, watakaounda muundo wa Tume ni Tume ya Utumishi ya Baraza, lakini muidhinishaji ni Kamisheni ya Utumishi wa Umma. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kwa masikitiko makubwa Kamisheni ya Utumishi wa Umma imeshindwa kuidhinisha muundo ule. Lakini wapo wanaosema kwamba Baraza hili lisigeuzwe kama ni Mahakama. *(Makofi)*

Sasa Mhe. Mwenyekiti, kama taasisi za serikali na taasisi za umma zitashindwa kutimiza matakwa ya wananchi, basi Baraza la Wawakilishi ndio itakuwa kimbilio lao. Vile vile watakapofika pahala kukosa imani na vyombo vya serikali au hata mahakama basi chombo hiki itakuwa ndio kimbilio chao. Kwa hivyo, hii sio mahakama wala sio Mahakama ya Rufaa kama wengine wanavyodhani. Kwa kweli hali hii inatokana na kwamba wananchi wamekosa sana imani na vyombo vyao, na ndio maana wanakimbilia huku na hata kwa mambo madogo madogo tu. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, Kamisheni ya Utumishi wa Umma imeshindwa kuwajibika katika hili, kuidhinisha muundo wa chombo hichi cha wafanyakazi, ambacho chombo hichi ndicho kitakachoweza kupanga namna ya maslahi yao na Mhe. Rais amesema hapa.

Sasa leo Mhe. Mwenyekiti, haiwezekani hata kidogo sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi ikawa shughuli zetu zinakwenda vizuri mipango yetu tunayoipanga inakwenda vizuri, lakini watumishi wanaotutumikia sisi, ambao ndio wanaotusaidia katika kushughulikia suala hili wakawa wanaendelea kuwa na manung'uniko haifai hata kidogo. *(Makofi)*

Kwa kweli haiwezekani watumishi wetu wawe wanadhalilishwa na hii ilikuwepo ndio haki yao na wajibu wao, kwa sababu wanachokidai ni haki yao. Kwa maana hiyo, muundo wa taasisi hii ni haki yao, ambapo wataweza kupata maslahi yao. Kwa hivyo, hili haliwezekani hata kidogo kwamba taasisi iliyopewa dhamana juu ya jambo hili kulitekeleza likae zaidi ya miaka miwili bila ya sababu yoyote, bila ya kujibu sababu yao na hilo haliwezekani. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nakusudia kuondosha shilingi mia moja katika Fungu la 47 la Kamisheni ya Utumishi wa Umma hadi hapo Mhe. Waziri atakaponieleza na niridhike, sababu iliyopelekea hadi leo taasisi au chombo hichi kushindwa kuidhinisha Muundo wa Utumishi wa Baraza la Wawakilishi. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa nikiangalia hotuba ya Mhe. Waziri namna Kamisheni inavyotekeleza majukumu yake na kwenye ukurasa wa 52, naomba kunukuu.

Ukurasa wa 52 wa hotuba ya Mhe. Waziri unaeleza hivi:-

> "Utekelezaji wa malengo ya mwaka 2012/2013 Kamisheni imefanya vikao 20 kwa lengo la kuwaelimisha watendaji Wakuu wa Wizara, Idara Maalum, Bodi za Mashirika ya Umma, Wakala wa Serikali, Mikoa, Wilaya na Manispaa na Mabaraza ya Miji na Halmashauri zote za Unguja na Pemba kuhusu majukumu ya Kamisheni na Tume za Utumishi.
>
> Pia Kamisheni imetayarisha rasimu za awali za miongozo kuhusu uchunguzi na ukaguzi wa rasilimali watu, utayarishaji wa uwasilishaji wa taarifa za rasilimali watu na ripoti ya mwaka, hali halisi ya utumishi wa umma.
>
> Vile vile iliidhinisha miundo ya utumishi ya Wizara 16 za SMZ, ilipokea na kuzingatia mapendekezo ya miundo ya utumishi kutoka Tume ya Utumishi ya Baraza la Wawakilishi, Tume ya Utumishi wa Mahakama na Tume ya Utumishi ya Idara Maalum".

Mhe. Mwenyekiti, maelezo haya tafsiri yake nini kwamba kamisheni inazingatia zaidi miundo ya utumishi serikalini kuliko miundo ya tume hizi. Kwa kweli haiwezekani hata kidogo kamisheni imeweza kuidhinisha miundo 16 lakini katika miundo iliyopendekezwa na tume hizi za utumishi ishindwe hadi leo, haiwezekani.

Hali hii ni kuonesha dhahiri kwamba kamisheni hii bado haijawa na usawa katika vyombo hivi au katika mihimili hii ama kwenye tume hizi ni jambo la kusikitisha. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, pia nimeangalia majukumu ya Tume ya Utumishi Serikalini, naomba kunukuu kidogo.

Majukumu ya Tume ya Utumishi Serikalini ni haya yafuatayo:-

> "Tume ina jukumu la kuajiri na kusimamia utaratibu wa ajira serikalini. Kupitia na kuthibitisha miundo ya utumishi serikalini".

Kwa maana hiyo, tume hii imepewa dhamana ya kuthibitisha miundo ya utumishi na ndio maana unakuta kwamba tayari SMZ imeshathibitisha katika taasisi zake, yaani miundo ya SMZ karibu taasisi 16 na hili ni jambo la kusikitisha na haiwezekani tukalinyamazia kimya ni lazima tuliseme kwamba hakuna *fair* katika taasisi hii. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nakusudia kuondoa shilingi mia moja katika fungu hili la 47 la Kamisheni ya Utumishi wa Umma hadi hapo atakaponipa sababu za kuridhisha tena za kunitosheleza kwa nini hadi leo Kamisheni ya Utumishi wa Umma imeshindwa kuthibitisha Tume ya Utumishi ya Baraza. *(Makofi)*

Nikiendelea na mchango wangu sasa naomba nizungumzie kuhusu Ofis ya *CAG*. Mhe. Mwenyekiti, Ofisi ya *CAG* inafanya kazi vizuri na tunampongeza sana mama yule wa *CAG* anafanya kazi vizuri sana. Kwa kweli Mhe. Mwenyekiti tulikuwa tukimlaumu juu ya ripoti zake anazotuletea hapa, ambazo yale mambo mazito ya msingi alikuwa hayawasilishi hapa na kulikuwa kunakuja taarifa ndogo ndogo tu au *query* ndogo ndogo. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, ukweli usiofichika wanawake wanapopewa majukumu wanatekeleza majukumu yao vizuri sana. Mimi nilikuwa nikijiuliza mama huyu kapatwa na nini mpaka leo ashindwe kutekeleza wajibu wake kumbe kulikuwa na mambo yakimtanza. *(Makofi)*

Kwa mfano, ripoti inapotayarishwa kutaka kuwasilishwa, kumbe wale *directors* wale walikuwa wanakwenda kuifanyia *editing*, yaani wanapunguza mambo na hili sio jambo zuri, sisi tunamlaumu kumbe wakurugenzi wake watatu wakikaa wanakwenda wanaipunguza mambo, yaani yale mambo mazito hawataki yaende kwa Mhe. Rais na Baraza hili, na hilo ni jambo baya sana Mhe. Mwenyekiti. *(Makofi)*

Kutokana na hali hiyo, na baada ya kuona *CAG* analaumiwa basi akaamua sasa ripoti ile wakae kwa pamoja na waiangalie pamoja na wakurugenzi wake, jambo ambalo halikuwafurahisha hata kidogo wakurugenzi na wakaamua kuchukua likizo. Yaani wakurugenzi wawili wamechukua likizo na mmoja akabakia kwa sababu hawakufurahishwa na jambo hilo. Kwa kweli hili ni jambo la kusikitisha, mtumishi wa umma ambaye unatakiwa utekeleze wajibu wako kwa umma kulinda fedha za walipa kodi unafanya vitendo kama hivyo. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, hawa hawako peke yao hawa kuna watu ambao wanawalinda na tunajua hilo na kwa sababu wasingeweza kuzungumza maelezo hayo au wasingeweza kufanya vitendo hivyo. Leo Mhe. Mwenyekiti, *CAG* tayari ameshatayarisha ripoti ambayo anataka kuiwasilisha kwa Mhe. Rais, yaani kila anapotaka kuiwasilisha kwa Mhe. Rais anaambiwa hapana subiri mpaka ipitie hapa. jamani Katiba ipo mamlaka aliyopewa *CAG* anapoandaa ripoti maana yake yeye ndiye anayetakiwa aikabidhi kwa Mhe. Rais na wala hakuna mtu mwengine, kwa sababu yeye ndiye mwenye wajibu wa kuiwasilisha ripoti ile kwa Mhe. Rais na sio kupitia maeneo mengine. Sasa tunaposema kwamba ripoti hii kwanza ije huku, maana yake ipite huku.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, mukigonga sana hizi meza kule ndani watu wa mitambo wanapata matatizo. Kwa hivyo, jitahidi kidogo mufanye aste aste Mhe. Mjumbe unazo dakika tano za ziada.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli tumuachie yule mama afanye kazi, yaani afanye kazi za kulinda mali za umma, atusaidie kwa mujibu wa majukumu yake na wala musimtishe mukamwambia mutamfukuza kazi. Kwa hivyo, hapa hafukuzwi mtu kazi, mtu yeyote mwenyewe anayetimiza wajibu wake hafukuzwi kazi na mama tunakwambia endelea na shughuli zako, endelea kutafuta uoza, endelea kutoa madudu na muwasilishie Mhe. Rais na tuletee katika chombo hichi. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, nakubaliana na wazo la kwa mujibu wa sheria kumtaka Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, kwamba Baraza hili likubali limuidhinishie aende sasa akakague *pay roll* katika serikali, yaani afanye kazi ya kukagua *pay roll* zote, kwa sababu tuna wasi wasi juu ya watumishi hewa. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, ripoti iliyopita inaeleza karibu ya wafanyakazi 70 wameshastaafu, lakini mishahara yao bado inaendelea kuchukuliwa na wajanja na wala hii haiwezekani na hiyo pengine ni sehemu tu ya watumishi wa umma. Kwa hivyo, lazima Baraza hili likubali kumpa idhini *CAG* akague

pay roll zote za watumishi wa umma na baadaye ripoti hiyo aiwasilishe katika chombo hichi. *(Makofi)*

Sasa naomba nizungumzie suala la mradi wa *E-Government*, ambapo Mhe. Waziri ametueleza inaonekana bado lina utata. Kwa kweli mradi huu ni wa muda mrefu, ambao hivi sasa tungetegemea uanze kazi, lakini inaonekana kuna matatizo katika eneo hili. Kwa hivyo, mimi nikubaliane na hoja ya kuunda Kamati Teule japo kuwa tumeambizana kwamba tusiunde, kuunda Kamati Teule kwa ajili ya kuchunguza mradi huu. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, mradi huu ulivyokuwa ukitekelezwa na ndugu zetu wa Jamhuri ya China na sisi tuliokuwa wala sio wataalamu tulikuwa tunajiuliza na sisi sio wataalamu wa mambo ya *ICT*. Lakini tulikuwa tunajiuliza jinsi ya utekelezaji wa mradi ule na mitaro iliyokuwa ikichimbwa karibu na kwenye mabega ya barabara, hivi kweli unaweza kuzika *pipe* au waya katika *road reserve*, maeneo ya barabara ambayo wakati wowote unaweza kutanua barabara, kitu ambacho si cha *temporary* ni cha kudumu, inaonekana kuna matatizo, si hayo tu inaonekana kuna matatizo mengi. *(Makofi)*

Kwa hivyo, lazima Baraza lako Mhe. Mwenyekiti lijiridhishe, kwa sababu dola milioni 19 si mchezo na fedha hizi zingeweza kufanya mambo mangapi? Kwa hiyo Baraza hili lazima lijiridhishe pamoja na Kamati Teule itakayoundwa basi ndani yake wawemo wataalamu wa masuala haya. Mhe. Mwenyekiti, tuchunguze mradi huu na tujue matatizo yake na tujiridhishe kama unakwenda vizuri na wala haiwezekani Mhe. Mwenyekiti na fedha hizi ni nyingi zingeweza kufanya mambo mengi.

Mhe. Mwenyekiti, leo sina mchango mkubwa isipokuwa maelezo yangu ni hayo. Kwa hiyo, kama utangulizi wangu nilivyosema kwamba namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti wakati atakapokuja kufanya majumuisho basi anieleze hoja ya msingi, ili niridhike na nitakaporidhika na maelezo yake, basi hakuna tatizo tutamuidhinishia fungu lake la 47 la Kamisheni ya Utumishi wa Umma waende huko wakafanye shughuli zao.

Mhe. Mwenyekiti, siungi mkono hoja narudia mpaka nipate maelezo ya kutosha, ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Hija Hassan Hija: Mhe. Mwenyekiti, nachukua nafasi hii kwanza kabisa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uhai, uzima na furaha leo hii kwa ajili ya kujadili hotuba ya Mhe. Waziri, ambayo ni hotuba ya ofisi muhimu sana kwa maslahi ya wazanzibari ambao ni wanyonge.

Mhe. Mwenyekiti, nitangulize kabisa kumpongeza Mhe. Waziri ambaye ameleta hotuba yake nzuri tena kwa madaha makubwa. kwa kweli hotuba imeandikika yenye takwimu nzuri, ambazo zinaashiria umakini katika wizara yake.

Mhe. Mwenyekiti, na mimi kwanza nitangulie kumpa pole kwa yule mfanyakazi wa Baraza la Wawakilishi ambaye jana hapa alituhudumia mpaka saa 5 usiku hatimaye akakumbana na watu ambao hawana maadili mema na wakakusudia kumdhuru na hatimaye kuokoa, lakini akanyang'anywa vitu vyake. Mimi mwenyewe binafsi na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kiwani nampa pole na hizo ndio changamoto za kazi na Mwenyezi Mungu amjaalie aende vizuri katika majukumu yake.

Kwanza kabisa naunga mkono zile hoja zote ambazo zimeanzwa na Mhe. Ismail Jussa Ladhu, ambapo hoja ya kwanza ya kufanya uchunguzi wa kina wa dola bilioni 19 za Mradi wa *E-Government*, ambao ni mradi wa zaidi ya miaka minne nyuma. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, naomba niwatahadharishe Waheshimiwa Wawakilishi wenzangu, kwamba si fahari, si uungwana wala si uadilifu kulinda watu pasi na sababu ya msingi. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, tunaelekea katika mwezi Mtukufu wa Ramadhani, basi tuanze uadilifu katika wiki hii ya mwanzo ya kuingia kwenye mwezi Mtukufu wa Ramadhani. Kwa hivyo, uadilifu pekee Mhe. Mwenyekiti ni kuchunguza fedha za wananchi ambazo zimetumika bila ya kuwa na uwazi.

Mhe. Mwenyekiti, kuna mdudu anaitwa Mwanamize, yule ni mdudu dhaifu sana, lakini anaweza kujenga nyumba kwa usiku mmoja seuze serikali iliyopewa dola bilioni 19 kwa ajili ya kujenga mtambo au utaratibu (*system*) wa *E-Government* umeshindwa kutupa majibu.

Mhe. Mwenyekiti, naunga mkono hoja hiyo na mimi nitashangaa sana kama kuna Waziri au Mwakilishi atakayeona hoja hii ya kuchunguza fedha hizi si ya msingi nitamshangaa na mimi nitaamini kwamba yeye ni sehemu ya tatizo. *(Makofi)*

Kwa kweli lazima tuwe wawazi, wakweli na tuwahurumie wanyonge, ambao ndio lengo la serikali yetu. Mhe. Mwenyekiti, naomba kwa heshima kubwa kuanzia Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, ambaye mimi namuamini mtu mzima mwenye busara mpaka Mwakilishi wa kawaida, basi tuunge mkono hoja hii ya kupata ukweli juu ya matumizi ya dola bilioni 19 ambazo zimetumika kwa

Mradi wa *E-Government*. Mhe. Mwenyekiti, hiyo ni hoja ya kwanza naunga mkono.

Hoja ya pili Mhe. Mwenyekiti, naunga mkono hoja ya wenzangu ya kumuomba kwa mujibu wa kanuni na sheria Ofisi ya *CAG* kutufanyia ukaguzi maalum wa *pay roll* ya serikali. Mhe. Mwenyekiti, nimekuwa nikisema humu ndani lakini kuna watu humu wakisema huonekana ni vichaa au wana hasira ama chuki. Kwa mfano, akisema Mhe. Hamza Hassan Juma huonekana amekosa uwaziri, na akisema Mhe. Hija Hassan Hija huonekana ni mpinzani na wala hatuko kwenye lengo hilo. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, tumekuwa tukisema kwamba fedha za serikali zinaliwa na wanaokula fedha wanajulikana, lakini wamekuwa wakilindwa kwa njia moja au nyengine. Sasa ili kuthibitisha ushahidi huo basi tumuombe *CAG* atuchunguzie *pay roll* ya serikali. Mhe. Mwenyekiti, juzi nilichangia na niliyataja majina wakati niliposoma barua za matumizi ya fedha za kiinua mgongo ambazo sikupewa na *CAG* wala na serikali kwa uwazi, isipokuwa nimefanya utafiti.

Kutokana na hali hiyo, mimi naamini kwamba fedha za serikali zinaliwa na lazima *CAG* tumuombe atufanyie uchunguzi maalum wa fungu hili la *pay roll* ya mishahara, ili tuweze kujiridhisha. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Fedha na hii naomba nitoe siri, kwamba ziara yetu ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo mara hii ilipokwenda Wizara ya Nchi, (OR), Fedha, Uchumi na Mipango ya Maendeleo, basi Idara ya Bajeti yenyewe baadhi yao walituambia kuna wizi mkubwa wa mishahara kwenye *pay roll* na sio *CAG*.

Kwa hivyo, kamati yangu chini ya Mwenyekiti wangu Mhe. Salmin Awadh Salmin walituambia watendaji wa fedha wale na hatusemi kwa sababu ni hofu, lakini kuna wizi mkubwa wa mishahara ya serikali katika *pay roll* ya serikali.

Pay roll hii Mhe. Mwenyekiti, hivi sasa iko chini ya usimamizi wa Ofisi ya Rais na Utumishi wa Umma. Mhe. Mwenyekiti, naomba *pay roll* hii itolewe na *CAG* aifanyie uchunguzi, ili tujiridhishe kama kweli serikali ina mzigo mkubwa huu wa wafanyakazi kwa ajili ya Zanzibar. Mhe. Mwenyekiti, pia nawaomba Wawakilishi wenzangu hiyo waikamate.

Mhe. Mwenyekiti, tulipochangia bajeti kuu ya serikali nilisema na leo narejea, kwamba bajeti lazima iwe na uwazi iwe na *data*, serikali wao walitwambia walitenga bilioni 17.5 kwa ajili ya nyongeza ya mshahara, lakini bila ya

kuwataja nani wanaoongezwa, walisema tu kwamba watawaongezewa Wawakilishi. Lakini Wawakilishi hawafiki hata milioni 500. Kama serikali ipo makini wangetwambia bilioni 17 nani kaongezwa, hadi hii leo hakuna majibu. Naomba Wawakilishi wenzangu na hili tumwambie *CAG* atuchunguzie fedha hizi wanapewa nani.

Mimi imani yangu kuna watu wanakula fedha kwa mgongo wa ajira. Mhe. Mwenyekiti, siamini kama bilioni 17 zitaongezewa watu kwa sababu hakuna uwazi, mngetwambia ni asilimia ngapi wafanyakazi wetu wa chini wataongezwa mshahara, hakuna majibu. Kwa hiyo mimi naamini kwamba fedha hizo zimetengwa kwa ajili ya watu kujinufaisha na lazima *CAG* atupe majibu achunguze fedha hizi.

Mhe. Mwenyekiti, mimi naunga mkono kwa heshima kubwa hoja ya Mwenyekiti wangu wa Fedha, Mhe. Salmin Awadh namuunga mkono kwa baraka zote kwamba azuie fungu 47 na atoe shilingi mia na mimi niko pamoja naye.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya utangulizi huo niseme kwa ufupi kwamba siungi mkono hotuba hii na sina sababu ya kuunga mkono. Mimi kazi yangu sio kuunga mkono tu, kazi yangu kuangalia uadilifu wa serikali mbele ya wananchi.

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli mimi ni miongoni mwa watu niliyekuwa namfikiria vibaya sana *CAG* mimi ni miongoni mwao. Nilikuwa nikifikiria *CAG* ni ofisi inayoficha maovu kumbe kwa muda mrefu Wawakilishi wamefanya makosa sio sahihi. Tulikuwa Wawakilishi tunamuonea *CAG* na ofisi yake. Mimi kwa niaba ya Wawakilishi wenzangu nimuombe radhi *CAG* na ofisi yake kwamba tulikuwa tunapotoshwa. Walikuwepo watu maalumu walikuwa wakitwambia kwamba *CAG* ni hivi na hivi na hivi. Ah! Maana yake amekaa sana, ni upumbavu mtu, kwani kukaa sana ndio uharibifu. Unaweza ukakaa miaka mia ukawa makini kuliko mwaka mmoja ukawa mpumbavu.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nawaomba radhi kwa niaba ya Wawakilishi wenzangu *CAG* tulikuwa tunamuelewa vibaya kwamba ni ofisi ambayo inaficha maovu kumbe kuna watu waliokuwa wanamfanyia hujuma.

Mhe. Mwenyekiti, juzi nimesoma barua tatu za Ofisi ya *CAG* jinsi watu walivyotia saini viinua mgongo feki. Nataka niwathibitishie Wawakilishi wenzangu barua zile zote tatu hakuna saini ya Bi Fatma, kuna saini za wale wakurugenzi wale watatu ambao kuwa wameondoshwa. Nitumie nafasi hii kwa niaba ya wananchi wa jimbo la Kiwani nimshukuru sana *CAG* na mimi

niseme tu kwamba kuna vita vya chini kwa chini vya taasisi tano na naomba leo nizitaje hapa hizo taasisi tano niwe shahidi nimezitaja.

1. Baraza la Wawakilishi, inaonekana *PAC* na Wawakilishi wanahoji mambo ya watu wanasahau kwamba haya mambo ni ya Wazanzibari sio ya watu.

2. Ofisi ya *DPP*, kwa sababu Baraza la Wawakilishi wakisha kuchunguza wakigundua itabidi DPP ashtaki.

3. Ofisi ya *CAG*,

4. Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali,
5. Ofisi ya Mamlaka ya Kuchunguza Rushwa na Wahujumu Uchumi.

Nakuthibitishieni Waheshimiwa Wajumbe, kuna watu wanapiga vita Ofisi hizi ili watu wafanye mambo yao na hizi ofisi zife. Ogomvi wote huu maslahi kwa Baraza la Wawakilishi wasiongezewe, *CAG* asiongezewe, kwamba kuna watu wanahujumu kwa chini ili wananchi washindwe kuhoji haki yao.

Mhe. Mwenyekiti, niwaombe Wawakilishi wenzangu pamoja na athari kubwa ya kisiasa tuliyonayo lakini tuwe makini, tutetee vyombo hivi vitano kwa maslahi ya Wazanzibari. Wazanzibari ni wanyonge sana lakini nchi hii haina umasikini kiasi hicho, kuna watu wamezowea kula ndani ya damu za wenzao, kuna watu wamekaa huko lakini wamechomeka mbinde ndani ya mgongo wa mwenzake anamnyonya damu. Bado makabaila Zanzibar tunao wa chini kwa chini.

Mhe. Mwenyekiti, ninachosisitiza kwamba haiwezekani, kwamba *CAG* tumpite vita. Juzi nimeona gazeti kwamba Ofisi ya Mhe. Waziri wametangaza kazi ya Mkaguzi wa nje aje amkague *CAG*. Si hatua mbaya lakini hivi sasa *CAG* anakaguliwa na chombo cha TCA. Mimi nilidhani kwanza serikali ingevunja mkataba kwa TCA baadaye ndio wakaomba ajira mpya, lakini hamjavunja mkataba mnatangaza ajira mpya maana yake nini? Maana yake yule mpya akija mkongwe atadai fidia kwa sababu mmevunja mkataba, mnafanya nini serikali.

Mimi nashauri ikiwa kuna lengo la kumleta mtu mpya kufanya ukaguzi basi bora vunjeni mkataba mwanzo ili wasije wakatutia hasara. Yule TCA ukivunja mkataba atatudai mamilioni ya fedha kwa jambo ambalo kuwa halina msingi wowote ni utashi tu aah! Yule amekaa sana, yule anaringa. Sasa kama yeye anaringa na wewe ringa, lakini afanye wajibu wake kwa maslahi

ya watu. Mhe. Mwenyekiti, mimi naiomba serikali Mhe. Waziri tuache mashara.

Mhe. Mwenyekiti, najua unataka kuniwashia lakini dakika 15 sijafika.

Mhe. Mwenyekiti: Nakuongeza na dakika 5 za ziada.

Mhe. Hija Hassan Hija: Na mimi niseme tu kwamba jana kuna wenzangu walilalamika kwamba tulifika saa 5. Tulifika saa tano kwa sababu mnalazimisha mambo yamalizike siku moja. Mnapoamua tumalize leo leo hasara yake ndio hiyo. Tuachiwe tuseme, mimi ni Mjumbe wa Bajeti wa Baraza hili na tumetenga siku za kutosha za kujadili bajeti hii. Msitiburure dakika 5 mara wengine 12 mara 20, tuachieni tuseme. Tupo hapa kwa ajili ya watu na ndio wao waliotuchagua. Mhe. Mwenyekiti ukiniwashia taa utanitisha naomba usiniwashie taa, ikifika nusu saa mimi nitakaa kitako kwa hiari yangu.

Mhe. Mwenyekiti, nisisitize tena kwamba Ofisi ya *CAG* tuilinde na wale wote waliohusika na ubadhirifu wa fedha za viinua mgongo pamoja na *CAG* kuwahamisha katika ofisi yake naomba asibughudhiwe aachwe. Na kwa kweli kama serikali ni waungwana wa kiasi hicho wangempongeza *CAG*. Yeye kwanza ni mtendaji ambaye ofisi yake ina kila katiba, unapombughudhi *CAG* maana yake unavunja katiba. Hii kumbughudhi maana yake inathibitisha kauli yangu kwamba serikali hii haina uchungu na wizi wa fedha, kwamba hapa ukiiba ndio unakuwa bwana na ukiibiwa unakuwa mtumwa. Yule anayeibiwa anakuwa mpumbavu na anayeiba ndio bwana.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kwa nasaa kubwa *CAG* asibughudhiwe, ifuatwe katiba na aachiwe afanye kazi kwa mujibu wa sheria. Niombe tu serikali kwamba muachieni *CAG* apumue msimbughudhi, msimkere.

Mhe. Mwenyekiti, na mimi kuanzia leo naamini kwamba kila unaposikia kesi ya wizi basi ni wanaume tu, mwanamke ni mmoja mmoja anayetuharibia nchi hii, lakini wizi wote wanaume. Mimi nashawishika kuiambia serikali nafasi za wanawake muwape wengi, wanaume wamekuwa na tatizo kila anayepewa jukumu ni prado, meli, ndege, wizi tu. Sasa mimi kuanzia leo naamini kwamba wanawake wanaweza na hata wasipowezeshwa wanaweza kufanya kazi.

Mhe. Mwenyekiti, niseme kwamba siungi mkono hotuba hii kwa sababu sina sababu ya kuunga mkono. Na nimalizie kwa kusema kwamba Kamisheni ya Utumishi wa Umma imejisahau. Nimetafuta sheria ambayo tuliipitisha Nam 2 ya 2011 nikajiuliza sisi labda tulisahau wapi. Kamisheni ya Utumishi wa

Umma imetwambia kwamba wanapitisha maombi 16 ya wizara ya muundo wa utumishi wa wizara. Jukumu lake ni kupitisha maombi ya tume nne, Afisa wa Utumishi wa Umma na wao wamesahau jukumu lao la msingi la kwamba Baraza la Wawakilishi, Mahakama, Vikosi na Serikali ndio Tume ya Utumishi wa Serikali.

Mhe. Mwenyekiti, mimi sina sababu ya kuwaidhinishia milioni mia nane na hatimaye wao wakapata nguvu ya kuwaumiza wafanyakazi wetu kwa msingi wa utashi. Mhe. Mwenyekiti, nawashauri wenzangu fedha hizi zisiidhinishwe, zizuiliwe mpaka watwambie sababu ni nini? Kuna wengine wanatwambia basi mwende Mahakamani, mkitaka twende Mahakamani na nyinyi hotuba yenu iondosheni mpaka twende Mahakamani. Najua majibu ya Waziri yatakuwa basi twende Mahakamani, kama twende Mahakamani hii iondosheni kwanza twende Mahakamani baadaye tafsiri ikitoka ndio tufanye bajeti.

Msituburuze, maana yake akizungumza Mhe. Salmin Awadh anaambiwa yeye kwa kuwa hapa Barazani kuna ndugu yake. Mimi sina ndugu yangu hapa, sina mjomba, sina ndugu wala sina shangazi, niko peke yangu. Lakini lazima tuwalinde wafanyakazi wetu msituburuze serikali. Iweje, afisa wa *CAG* ambaye anakagua zaidi ya *vote 15* apewe laki nne, lakini mhasibu wa wizara apewe milioni moja na nusu, kwa nini? Mhasibu wa wizara ana *vote* 1 anapewa 1.3 milion, *CAG* mkaguzi wa nje tena mtaalamu anapewa laki nne, kwa nini? Kama sio uuwaji wa makusudi. Kuna njama ya kuuwa ofisi hizi kwa maslahi ya watu.

Mimi naamini kwamba mafisadi inawezekana wapo wanatumia udhaifu wetu kutuangamiza Mhe. Mwenyekiti, kwa heshima kubwa lazima niwafanyie kazi wananchi wa Jimbo la Kiwani. Mimi ni Mtumbatu, kaka yangu nampenda sana lakini kwa hili naomba anisamehe siungi mkono, sikubali, sikubali, sikubali, mpaka akubali kwamba Tume hizi nne ziachiwe zipumue, tupewe haki yetu, tusiburuzwe. Na kama atajibu kama twende Mahakamani basi nashauri kwamba hotuba hii izuiliwe twende Mahakamani, tafsiri ikitoka ndio uje tena utupe hotuba yake.

Mhe. Mwenyekiti, siungi mkono hoja.

Mhe. Hamza Hassan Juma: Mhe. Mwenyekiti, kwanza nakushukuru kunipa nafasi hii na mimi nikazungumza machache sana kuhusu hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Nchi, Afisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Mhe. Mwenyekiti, kwa niaba ya wananchi wa jimbo la Kwamtipura nimesimama hapa kutetea maslahi ya watumishi wote wa umma miongoni

mwao wakiwemo wananchi wa jimbo la Kwamtipura. Na leo hii ndio bajeti yao kwa hivyo nitajitahidi na nitamuomba Mwenyezi Mungu anisaidie.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka nianze moja kwa moja, kwanza hotuba hii ya Mhe. Waziri siiungi mkono. Siiungi mkono ninazo sababu zangu, Mhe. Mwenyekiti, sitaki kurejea rejea, lakini na mimi kwa sababu hili buku ingelikuwa kapewa mmoja tungeambiwa tunarejea rejea, lakini kila mtu kapewa lake. Sasa nilitafuta katika kitabu hichi kidogo ambayo nikaomba Wizara ya Utumishi wa Umma, nikatafuta eee sijaona, nilipoangalia buku dogo nikaona Kamisheni ya Utumishi wa Umma.

Mhe. Mwenyekiti, nataka kusema Kamisheni ya Utumishi wa Umma fungu lake sitoliunga mkono kwa sababu wameshindwa kazi. Nikizungumza nitakuwa narejearejea ambapo kanuni zetu haziruhusu, lakini leo unapopewa kazi unakaa nayo juu ya meza miaka miwili ni sawa sawa kushindwa kazi.

Mhe. Mwenyekiti, kwa bahati nzuri mimi nilikwenda China, watu wananuna sana kila nikisema nilikwenda China lakini nilikwenda China. Moja katika kitu walichotueleza Wachina na kwa bahati nzuri Mhe. Ali Salum Haji hayupo hapa lakini tulisomeshwa na maprofesa watupu, mkitaka vitabu vyote ninavyo nitakuonesheni. Tuliwauliza kwa nini China ikawa inapiga hatua za haraka. Kitu alichotueleza:

1. Uwajibikaji

2. Kuwa na mipango bora inayozingatia muda

3. Unapopewa majukumu unapewa na muda, muda ukishafika kama umeshindwa kazi mzee unawajibika.

Hayo ndiyo mambo ambayo yaliyokuwa yanawafanya waendelee kwa haraka sana. Kitu cha kusikitisha, leo tume hii ya Utumishi kumbe tumeipa nguvu kubwa na nguvu ile wanaitumia vibaya.Tume ile ilipoundwa mimi naamini iliundwa kwa nia njema sana. Lakini leo imekuwa ni kikwazo cha maendeleo na halafu kuwatia tafrani watumishi wa umma hasa katika maslahi yao.

Mhe. Mwenyekiti, nazuia fungu hili mpaka nipate maelezo. Na maelezo yenyewe zishatumika busara nyingi, kama busara zimeshamalizika kitu kilichobakia ni ukaidi. Wizara tutaiachia ikafanye kazi lakini Kamisheni kama wanavyowakwamisha wenzao washindwe kufanya kazi zao kwa vizuri basi na wao tutalizuia fungu lao mpaka pale watakapotekeleza majukumu waliyopewa kikatiba na kikanuni. Kanuni sote tunazo na Katiba sote tunazo.

Mhe. Mwenyekiti, naondoka hapo nakuja kwa *CAG*. Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Salmin Awadh alikaribia anifilisi, lakini kwa bahati kama nilivyosema kila mtu kapewa kitabu chake. Mimi nilisoma ninayoyajua miye na yeye kasoma anayoyajua yeye. Naunga mkono na wenzangu waliotangulia, kaanza Mhe. Ismail Jussa Iadhu, akaja Mhe. Salmin Awadh akaja tunamtaka, sio tunamuomba, tunamtaka *CAG* aende akakague *pay roll* yote ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Sio hapo tu na hii tumemwambia kwa nini, tumegundua.

Mimi mwaka juzi niliwahi kumwambia Mhe. Waziri lilipokuja lile fungu la bilioni 19 la ongezeko la mishahara. Nikamwambia Mheshimiwa mbona hujatuletea *break down*, kwamba wizara gani watapandishwa kiasi gani, tena nikamchokoza maana miye Mhe. Haji Omar Kheri, rafiki yangu, mwalimu wangu kabisa wala sikatai, yeye ndiye aliyenifundisha kufungua mabuku haya vifungu na mambo mengine. Hata maendeleo katika Jimbo la Tumbatu mimi nimeiga maendeleo katika jimbo la Kwamtipura nimeanza kuiga kutoka Tumbatu, kajitahidi sana.

Sasa Mhe. Mwenyekiti, CAG kwa nini tukasema akakague *pay roll* ya serikali, tumepiga kelele suala la mishahara hewa, lakini sio hivyo kumbe na viinua mgongo hewa. Hii ni aibu kwa nchi ambayo imeunda maalum Wizara ya Utawala Bora, mambo ya kufumbiana macho hii nchi haiendi. Leo wafanyakazi wetu wanalalamika maslahi madogo, askari wetu wa vikosi vya SMZ ni aibu, sisi tunalala wao wanatulinda, maslahi yao hatuyashughulikii. Sasa hivi tayari yapo katika Kamisheni ya Utumishi wa Umma nenda rudi, nenda rudi, kikubwa unaambiwa fedha hakuna.

Mheshimiwa na hii kazi ya ukaguzi *CAG* tunampa mwaka mmoja atakuja kutwambia mabilioni mangapi yanayoibiwa kila mwezi na kila mwaka. Sasa kama kuna mabilioni yanaibiwa kila mwezi na kila mwaka leo useme serikali haina uwezo wa kuwalipa wafanyakazi wake vizuri. Mheshimiwa katika Rais miongoni mwa Rais ambao tunawapongeza sana kwa imani ya watumishi wa umma ni Mhe. Dokta Ali Mohammed Shein hili hatufichi kikiwepo anatoa, tena katoa uhuru wala hapangi yeye. Anawambia hebu kakaeni, angalieni kapu yetu iko vipi, wapeni. Tunashukuru hivo hivo kidogo kidogo kitachopatikana.

Lakini hicho anachosema wapeni kama kinavuja watu watapata lini kinachotosheleza. Kwa bahati nzuri Mhe. Makamu wa Pili wa Rais yupo mimi namshukuru sana siku iliyokuwa ya Wizara yake alizungumza au kabla ya Wizara yake nafikiri alitakiwa atoe kauli ya serikali na Mhe. Ismail Jussa Ladhu. Akasema jamani mimi katika kitu ninachokichukia ni ubadhirifu, rushwa, tena akasema kuna Waziri mmoja alikuja mwenyewe akaja

akanambia ofisini kwangu kuna nuka unuko. Unuko kwa lugha ya kwetu kule Kaskazini Chaani. Maana yake mambo machafu, wizi. Sasa kwa nini wengine wanashindwa.

Sasa Mhe. Makamu wa Pili wa Rais tunakwambia miongoni kwa watu waadilifu hapa Zanzibar na wewe, na ndio maana Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi akakupa nafasi ya kuisimamia serikali. Tunataka sasa uwasimamie watu wote waliotafuna pesa za viinua mgongo. Watu wameshakufa pesa zinatafunwa.

Mhe. Mwenyekiti, CAG mwenzangu kazungumza iundwe Kamati Teule Mhe. Salmin Awadh, na mimi nasema iundwe Kamati Teule kwanza ya Baraza kuna kazi ya *E- Government*. Aibu mimi unajua ni Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa. Miongoni mwa majukumu niliyopewa ni kusimamia idara inayohusiana na masuala ya *Diaspora*. Wazanzibari waliokuwepo nje wanaitafuta *website* ya SMZ hawaioni, imefungwa, aibu. Wizara tatu zinasimamia *E-Government*, *website* ya serikali hamna, tunakwenda wapi? Tena kwa bahati nzuri siku hizi mitandao wanaranda nayo mikononi, hebu itafute hapa SMZ *ww* nini sijui, hupati kitu hamna, aibu.

Mhe. Mwenyekiti, mradi huu kuna Mheshimiwa mmoja alianza kuzungumza tokea siku ya mwanzo mradi huu, sijui mara upo Miundombinu, mara Utumishi wa Umma, mara Wizara ya Fedha watu wananyang'anyiana tu, hakuna kinachokwenda ukakaguliwe. Lakini sio hapo tu *CAG* tunakupa kazi uende Dubai ukakague ZMA *Zanzibar Maritime Authority*, Mheshimiwa katika usajili wa meli kuna madudu. Wanzanzibari nchi inatafunwa hii, meli zinazosajiliwa siku zote tunasema jamani pesa zije katika utaratibu wa kawaida, kuna vyombo vingapi vya fedha. Fedha kwenye mkoba, meli zinazosajiliwa hapa ukiuliza hapa hazijulikani, kawaida inatakiwa kila meli inayosajiliwa kwa jina la Zanzibar ipatikane ajira si chini ya wafanyakazi watano.

Mhe. Spika, mimi katika Jimbo langu pale Saateni ukienda kijiweni vijana wananisikia, kuna vijana wameshasoma ubaharia kazi hakuna. Leo hizi meli zinazosajiliwa meli za nje kwa jina
la Zanzibar zinatakiwa lazima zitoe ajira kutoka kwa watu wa Zanzibar, leo kuna meli zaidi ya mia moja na ngapi. Safari ile tukaambiwa kuna meli za Iran zinapeperusha bendera ya Zanzibar tukavungwa vungwa hapa hakuna kinachotambulikana. Leo mfano ziwe meli 50 tu zilizosajiliwa kwa jina la Zanzibar, kama kila meli moja imeajiri vijana wa 5x5 = 25 vijana 250 mabaharia, ukienda pale jumba jeupe pale Majestic kila siku vijana wanakwenda kupiga chabo na mavyeti, sijui mie nimeshasomea meli,

nimeshasomea sijui kukwaruza meli, kupaka rangi. Huku tunapiga kelele sijui ajira kumbe ajira zipo, watu wanachakachua. Mheshimiwa hawa vijana waliokuwa wameshasoma wanakosa kazi watakuja kutupandia hapa migongoni kwa sababu kazi zipo, serikali imetoa fursa, huku Mheshimiwa *CAG* kama hajawahi kupanda ndege safari hii tunampandisha ndege. Fungu la *CAG* liongezwe aende Dubai akakague ZMA.

Mhe. Mwenyekiti, naondoka hapo Kamati Teule mbali *CAG* mbali, kila mtu na kazi yake. Msije mkatwambia kazi keshapewa *CAG*, Kamati Teule haipo. Kamati Teule ipo tukafanye kazi. Mhe. Mwenyekiti, sasa nije kwenye mambo madogo madogo.

Katika mambo madogo madogo kuna watumishi. Mimi nashukuru sana serikali yetu, safari hii wameangaliwa mpaka na wale wasaidizi wa Waheshimiwa Mawaziri. Mimi nilikuwa naomba, mimi nawaombea zaidi madereva, sasa hivi kutokana na uchungu wa Rais wetu katika maendeleo anafanya vikao vya Baraza la Mapinduzi mpaka saa 6 za usiku saa 7 za usiku. Siku hizi Baraza la Wawakilishi na sisi tulivyokuwa hatutaki kuchakachuliwa tunataka kila shilingi tuijue imetumika vipi. Jana tumeondoka saa 5:45 za usiku. Kwa bahati sisi sote hasa Mawaziri wana madereva wa serikali.

Mhe. Mwenyekiti, madereva wetu mishahara yao na hizo posho zao hali kama tunavyoijua, keki yenyewe ndogo. Tunaomba sana madereva hawa wa Mawaziri angalau wapatiwe vespa. Leo mtu keshamuweka Waziri na Mawaziri kutokana na woga wao anaogopa kumuachia gari dereva akarudi nayo, dereva na kibaskeli, akikabwa siku ya pili waziri ataendeshwa na nani, tuwasaidieni wenzetu hawa. Hili nilikuwa naomba sana kwa sababu wizara hii ndiyo inashughulikia maslahi ya watumishi wa umma basi angalau wapatiwe vyombo vya usafiri hasa vespa. Maana vespa hata mwizi akikufukuza akikupata mzee tena huo unakuwa uzembe wako.

Mhe. Mwenyekiti, hivi karibuni tulipitisha sheria na tulipitisha sheria Ofisi ya Mwanasheria Mkuu kusimamia maslahi ya wanasheria wote serikalini, isipokuwa wa Baraza la Wawakilishi. Tunamshukuru sana Mhe. Mwanasheria Mkuu ni msikivu na kwa sababu yeye ni Mwanasheria. Alitusikia lakini bado nilikuwa naomba ajaribu kuangalia maslahi hasa ya watumishi wa *DPP* ambaye na yeye mwenyewe ile ofisi ndiye aliyeianzisha, lakini vile vile na hawa wanasheria wengine mfano kama Mahakimu maslahi yao hayalingani.

Kwa hivyo namuomba Mhe. Mwanasheria Mkuu najua kwa kuwa ile sheria ndio kwanza tumeipitisha anajaribu kuanza kuangalia. Suala la maslahi ya hawa wanasheria wetu mimi naona liangaliwe. Kwa sababu ukiangalia hata zile sifa, kwa sababu Mhe. Mwanasheria Mkuu walipokuwa *DPP* alijitahidi,

kasomesha sana pale. Mimi kipindi hicho niliwahi kuwa Waziri miye siku mbili tatu pale, pamoja na ukubwa wangu niliokuwa nao nilikuwa nakwenda, ana matabu pale nilikuwa najiuliza sijui anasoma saa ngapi matabu yote yale. Lakini kumbe akisikia nini na nini *volume* ngapi anavuta pale. Aliwasomesha sana vijana na sasa hivi kile kitengo kipo vizuri. Sasa namuomba awatengezee na maslahi ambayo wafanye kazi vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, haya yote tunayopiga kelele baadaye yanakwenda kwenye sheria, leo umeshamkamata haya huyu katafuna pesa za umma hapa mnampiga pingu wapi, Spika hana pingu hapa, lazima Ofisi ya *DPP* iwaburuze Mahakamani. Sasa kama hawa maafisa wa Ofisi ya *DPP* hawajatengenezewa vizuri maslahi yao. Ukisema utamburuza mtu Mahakamani, utaburuzwa weye mtu hafiki Mahakamani. Hili pia nilikuwa naliomba sana lishughulikiwe.

Mhe. Mwenyekiti, jengine la kumaliziamalizia nilikuwa nataka nimalizie na kuhusu Ofisi ya Nyaraka. Kama nilivyosema kwamba kimoja ambacho nilichojifunza China kama huna kumbukumbu za nyuma au za ulikotoka si rahisi kujua unapokwenda na utaendelea vipi.

Naomba sana kuna kumbukumbu nyingi za Serikali ya Mapinduzi Zanzibar zimepotea potea, tunaomba mjitahidi kuzitafuta. Lakini miongoni mwa kumbukumbu hizo Mhe. Mwenyekiti, ni jengo lile ambalo tunaambiwa kabla ya sisi Baraza ya sisi Baraza la Wawakilishi huko nyuma kulikuwa kuna *legico* pale *Victoria Garden* ambayo ofisi ile ndio wamepewa Mamlaka ya Kupambana na Rushwa kutokana na uhaba wa nafasi au ufinyu wa nafasi. Lakini tunaomba ule ukumbi uliokuwa ukitumika wa *legico* kama Baraza la Wawakilishi na ile ndio kielelezo kwamba Zanzibar Sheria zilianza mapema. Ukumbi ule ubakie na uhifadhiwe na Baraza la Wawakilishi na zile kumbukumbu zake zote ziendelee kubakia. Ile ndio inaonesha kwamba Zanzibar utawala haukuanza jana na leo.

Kwa hivyo naomba sana Mhe. Waziri namjua msikivu, naona sasa hivi mnajenga majengo mengi tu mazuri na ya kisasa basi na huyu mwenzetu Mkurugenzi wa ZAKUKURU. Mwisho kabisa kabisa naomba *CAG* apatiwe ulinzi. Ndio maana *CAG* huyu akalindwa na Katiba, Mhe. Rais hawezi akaamka asubuhi akasema anamuondoa *CAG* lazima kuna utaratibu wa kisheria kalindwa kisheria. Mheshimiwa tumekwenda Uganda *CAG* ana ma-*body guard* watatu, ana majeshi, ana mapolisi ana wale wenye marungu na kwa sababu gani Mheshimiwa Kamati ya *PAC* bila ya *CAG* hawana kazi, wale ndio wanaoangalia madudu. Sasa leo anapokwenda kufanya ukaguzi, akagundua madudu ya watu, watu wanaweza wakamfanyia mbinu kuanzia leo, kwa sababu sasa hivi tumeshampa Ludovick Uttoh *CAG* wa Dar es

Salaam ripoti yake tena nimeangalia kifungu cha Katiba naomba nikisome ili nipate kukaa kitako.

Katiba ya Zanzibar kifungu cha 112 kilichoanzisha sheria ya *CAG* (5) kinasemaje, Mhe. Mwenyekiti nikisoma Katiba ukinikatisha kitako utakuwa umevunja Katiba. Kifungu hiki kinasemaje,

"Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali atawasilisha kwa Rais kila taarifa atakayoitoa kwa mujibu wa masharti ya kifungu kidogo cha 3(c) na kifungu hiki baada ya kupokea taarifa hiyo Rais atawatangazia watu wanaohusika wawasilishe taarifa hiyo kwenye kikao cha kwanza cha Baraza la Wawakilishi kitakachofanyika baada ya Rais kupokea taarifa hiyo na itabidi iwasilishwe katika kikao hicho kabla ya kupita siku 7 tangu siku ile ilipoanza kikao hicho iwapo Rais hatachukua hatua za kuwasilisha taarifa hiyo kwenye Baraza la Wawakilishi, basi Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali atawasilisha taarifa hiyo kwa Spika wa Baraza la Wawakilishi au Naibu Spika, ambaye atawasilisha taarifa hiyo kwenye Baraza la Wawakilishi".

Kwa nini nikasema hivyo kwa sababu wakati mwengine Mhe. Rais samahani ninapozungumza Mhe. Rais sio Dr. Shein Mhe. Rais yoyote atakayechaguliwa na wananchi wa Zanzibar kwa katiba hii. Kwa sababu inawezekana pengine katika madudu yale pengine na ofisi yake ilihusika au pengine yeye mwenyewe alihusika.

Sasa *CAG* anatakiwa ripoti ile asimuoneshe mtu yoyote anampelekea Mhe. Rais, kama Mhe. Rais kama kuna rafiki zake ndugu zake wamehusika maana yake hatoiwasilisha Baraza la Wawakilishi. Kwa hivyo *CAG* Katiba inamtaka ailete moja kwa moja kwa Spika, Spika ndio anowawakilisho wote kwa wananchi. Ndio maana nikasema ripoti ya *CAG* hatakiwi tena hata amuulize mtu niipeleke lini anatakiwa mwenyewe mguu kwa mguu Ikulu Mhe. Rais haya ndio mambo ya watu wako bajeti uliyopitisha matumizi haya, haya yametumika vizuri, haya yametumika vibaya.

Wenzetu Bara *CAG* anasemaje kule asilimia 20 ya zile fedha za manunuzi zimekwenda matumboni kwa watu, sasa huyu *CAG* wetu hajatwambia tunataka tumpe hii kazi aje atwambie ni shilingi ngapi zimekwenda matumboni kwa watu na wazicheuke.

Baada hayo machache Mhe. Mwenyekiti kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kwamtipura siiungi mkono hotuba hii mpaka nitakapopata maelezo ya kutosha kabisa.

Mhe. Bikame Yussuf Hamad: Ahsante Mhe. Mwenyekiti kwa kunipa na mimi fursa hii ya kutoa mchango wangu mchache kwa hotuba hii ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Mhe. Mwenyekiti kwanza nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia uzima na uhai wa kuweza kusimama hapa katika Baraza hili. Lakini pia napenda nimpongeze Mhe. Waziri kwa kitabu chake hiki na nimpongeze na watendaji wake kwa kazi kubwa anayoifanya ikiwa ina malengo ya ufanisi wa kisiwa chetu cha Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, mimi sina mengi kwa sababu mimi ni miongoni mwa Mjumbe wa Kamati lakini kwanza niseme kuwa naunga mkono hotuba hii asilimia mia kwa mia. Lakini kulikuwa kuna mambo nilikuwa nataka niyachangie kidogo ili kupata ufanisi zaidi.

La kwanza Mheshimiwa kuhusu ripoti yetu hii tuliyoieleza katika kifungu hiki hapa nitakachokisoma, kamati imekuta taasisi moja ya umma ambayo imekimbiwa na wataalamu wake hadi kufikia kubaki bosi na taasisi hiyo peke yake. Mhe. Mwenyekiti hili niseme kuwa serikali sasa kwa vile inapoteza pesa nyingi kwa kuwasomesha wataalamu wetu ili kuweza kutumikia wananchi wa kisiwa hiki, lakini hatimaye inafika pahali kwa kisingizio cha maslahi madogo kuacha nafasi zile na kuondoka.

Kwa hivyo tunaitaka serikali kupitia hili basi kuwepo na mikataba maalumu ambayo kuwa watawachukua wataalamu hawa kuwasomesha ili serikali iepukane na tatizo hili. Kwa hivyo ningelimuomba Mhe.Waziri hili alione na waliangalie sana.

Lakini jengine katika ripoti hii Idara ya Mipango na Raslimali watu suala kubwa ambalo kamati imetaka kusisitiza hapa ni maadili ya watumishi wa umma, ingawa tunapiga kelele hapa maslahi ya watumishi wa umma yaimarishwe bado kuna tatizo la kuporomoka kwa kasi za maadili ya utumishi wa umma hasa katika sekta zinazohusika moja kwa moja kwa huduma za wananchi.

Mheshimiwa hili mimi nataka nizungumzie kwa upande wa Wizara ya Afya. Wizara ya Afya imekuwa kero kwa kutoa huduma zilizokuwa si nzuri kwa wananchi wake hasa katika masuala ya usafi. Kwa hivyo hawa na wao ni watumishi wa umma na wamewekwa pale kuwatumikia wananchi lakini hatimaye mgonjwa kaenda kule kalazwa hospitali anataka kile choo kinamshinda.

Kwa hivyo hilo tumeshalipigia sana kelele kwa Mhe. Waziri wa Afya lakini hatimaye tukizunguka huku mahospitali matatizo yanabakia kuwa yale yale

na hatuoni ufanisi unaofanyika. Kwa hivyo nakuomba Mhe. Waziri hili ulione na uliangalie na ukiwa unataka majaribio kuona hili basi zunguka kwenye mahospitali utaona tatizo hilo na kero hiyo kwa wananchi wetu.

Mhe. Mwenyekiti niende katika Idara ya Mafunzo na maendeleo ya raslimali watu, katika *paragraph* hii ya 48 ameeleza Mhe. Waziri hapa katika kitabu chake kuwa maafisa wawili kwa kupitia programu za ITEC, wanawake wanne kutoka vijiji vya Kandwi walipatiwa mafunzo ya miezi sita huko India kuhusu kutengeneza umeme wa jua na uvunaji wa maji ya mvua. Baada ya kupata mafunzo hayo wamekuwa wataalamu wa kufunga umeme wa jua kijijini kwao na nyumba zaidi ya 100 zimefanikiwa na mradi huu.

Mheshimiwa mimi niipongeze serikali kwa juhudi zake hizi lakini naamini kuwa badala ya kuwachukua wanawake hawa wanne wakawapeleka kwenda kujifundisha mafunzo haya tulitaka wawe walimu wa Zanzibar, kama walifundisha katika kijiji chao nyumba mia wakaweza kuzimudu kwa kutekeleza hilo basi wasiishie hapo, kwa sababu wananchi wetu wengi hasa vijijini hawawezi huduma hizi za umeme. Kwa hivyo ningemuomba Mhe. Waziri hawa wawe walimu hasa wa maeneo ya vijijini ili haya mafunzo yanayopatikana yawe endelevu.

Lakini jengine nije katika Idara ya Utawala Bora ukurasa wa 30. Mhe. Naibu Mwenyekiti Mhe. Waziri katueleza hapa kuwa Idara imerusha hewani vipindi vya elimu ya uraia kupitia Shirika la Utangazaji Zanzibar. Aidha imetoa elimu kwa njia ya redio na televisheni kuhusu mambo yanaeleza hayo. Mheshimiwa hili jana alilizungumzia Mhe. Mohammed ni tatizo bado tunalo katika kisiwa cha Pemba. Kwa hivyo Mhe. Waziri nakuomba sana mambo ya televisheni kwa kisiwa cha Pemba bado inakuwa ni changamoto la kupata habari hizi, hasa ukizingatia kuwa sasa hivi ni utamaduni wa kupata habari kwa kupitia redio na televisheni. Kwa hivyo bado hili ni tatizo serikali tunaiomba ikae ilione tatizo hilo kuwa wananchi wa Pemba bado hawapati matangazo yoyote kupitia vyombo hivyo viwili vya ZBC.

Mheshimiwa jengine Idara ya Nyaraka na kumbukumbu za taifa ukurasa huu 34 Mhe. Waziri ametueleza hapa kuwa ukaguzi wa ofisi za kuhifadhia kumbukumbu katika mikoa na wilaya kuzifanyia matengenezo nyaraka na kumbukumbu chakavu na mambo mengine. Mhe. Waziri hili nalo ni tatizo lipo. Sasa hivi kwenda pale Wilaya ya Micheweni ukawa unataka kumbukumbu kama umeharibikiwa na cheti cha mwanao unataka ile kumbukumbu mtoto anayezaliwa pengine mwaka wa 80 au ngapi haipatikani.

Sasa sijui tatizo hili ni vipi sijui uhifadhi huu wa nyaraka unahifadhiwa vipi kwa kusema kweli. Kwa hivyo Mhe. Waziri hili ni jambo zuri kwa hivyo

naomba serikali ifanye kama inavyowezekana ili kuwapa elimu wakuu hawa wa wilaya na watendaji wao wahifadhi kumbukumbu vizuri kwa ajili ya maslahi ya wananchi, kwa sababu hakuna anayeweza kuhifadhi lakini saa nyengine mtu anatokewa na matatizo ikabidi anakwenda pale kumbukumbu hazionekani.

Mhe. Mwenyekiti la mwisho nizungumzie kuhusu hii mamlaka iliyoanzishwa ninafikiri ishazungumziwa na watu wengi na kwenye Kamati ripoti wametoa, lakini nasisitiza Mhe. Waziri kuwa mamlaka hii iliyoanzishwa basi serikali ijitahidi nayo kwa kuwashughulikia watumishi hawa wa mamlaka ya kuzuia rushwa ili na wao wasijekuwa ni chanzo cha matatizo katika nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti kwa hayo machache ninakushukuru naunga mkono hoja asilimia mia kwa mia.

Mhe. Mbarouk Wadi Mussa: Ninakushukuru Mhe. Mwenyekiti na mimi kunipa nafasi ili niweze kuchangia katika hotuba hii ya Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Mhe. Mwenyekiti nichukue nafasi hii kumshukuru Mhe. Waziri pamoja na watendaji wote wa Wizara yake kwa kutuandalia kitabu hiki au hotuba hii na leo akaja akaiwasilisha hapa.

Mhe. Mwenyekiti mimi kuanza kwangu kwanza naanza kwa kuunga mkono hoja ya Mhe. Salmin Awadh Mnadhim wangu wa Chama cha Mapinduzi. Ninaunga mkono hoja yake na mimi niko pamoja naye katika kulizuia fungu lile na ninafanya hivyo kwa sababu.

Mhe. Mwenyekiti sisi kule kwenye Chama cha Mapinduzi tuna taratibu ya uongozi, unapoona kiongozi wako katoa mfano wa namna kama ule kwa sisi wanachama wale wajumbe wake tunatakiwa kufuata. Nitawashangaa sana Wajumbe wa Chama cha Mapinduzi wenzangu wasipomuunga mkono Mheshimiwa Mnadhimu wa Chama hichi katika hotuba yake hii.

Mhe. Mwenyekiti mimi mchango wangu utakuwa si mkubwa sana maana yake umefilisiwa filisiwa na wale wachangiaji waliotangulia. Mimi nitaanza na ukurasa wa 5 kitabu hiki cha Mhe. Waziri wenye *paragraph* ya kumi kwenye majukumu makuu ya wizara, anasema Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais Utumishi wa Umma na Utawala Bora ina jukumu la kusimamia haki na wajibu wa watumishi wa umma ili waweze kuwahudumia wananchi kwa kiwango cha juu hiyo ndio nukuu yangu.

Lakini mengi yameelezwa na wenzangu waliotangulia na mimi nisingependa niyachambue tena nilikuwa nasoma hii Mhe. Mwenyekiti kuoanisha na yale

ambayo wenzangu waliotangulia waliyazungumza. Lakini mimi Mhe. Mwenyekiti nitasogea kwenye ukurasa wa 12 wa kitabu cha Mhe. Waziri kwenye Idara ya Uendeshaji na Utumishi. Ninafikiri Mhe. Mwenyekiti katika Idara hii ndipo panapokaa mshahara hapa wa Mhe. Waziri. Mimi Mhe. Mwenyekiti nataka kuuzuia mshahara wa Mhe. Waziri kwa kutowajibika kwake.

Mhe. Mwenyekiti kama utakumbuka kwenye mwezi wa Aprili, 2011 tulipitisha sheria ya kuweka miundo na uendeshaji na usimamizi wa utumishi wa umma Zanzibar na mambo mengine yanayohusiana na hayo. Ninafikiria ilipita kabla ya hapo kidogo na uniwekee kumbukumbu vizuri kidogo. Lakini Mhe. Mwenyekiti baada ya kuipitisha sheria ile, ile sheria ilielekeza kwamba kutatungwa kanuni na kazi ile alipewa Mhe. Waziri ya kutunga kanuni kwa ajili ya kuitafsiri sheria ile. Lakini cha kusikitisha mpaka hii leo kanuni ile Mhe. Waziri hajaitunga bado. Sasa ndio maana nikasema ninalizuia fungu la mshahara wa Mhe. Waziri kwa kutowajibika kwake.

Kwa sababu Mhe. Mwenyekiti ukiitizama ile sheria mle ndani sheria yoyote ile huwa ina kitu kinachoitwa kanuni, sheria nyingi sana. Hata katika kur-ani utakuta kuna mambo tumeamrishwa waislamu mule labda salini, lakini ufafanuzi wa namna wa kusali mwenyewe Mtume Muhammad ndio ameelekeza mtasali katika utaratibu huu, mtafanya hivi ile inaitwa kama ndio kanuni yetu.

Sasa na sheria hii nayo imewekewa kwamba kutakuwa kuna kanuni kama zitakavyotungwa na Waziri. Lakini Waziri sasa hivi ni miaka 2 ninasikitika sana Mhe. Mwenyekiti kwamba hajatunga kanuni zile kwa ajili ya utekelezaji wa sheria hii. Sasa mimi napata shaka kidogo juu ya uwajibikaji wa Waziri ninahisi Mhe. Waziri labda sijui ana majukumu mengi sijui wana kitu gani. Sasa naomba atakapokuja hebu aje atupe ni kwa nini mpaka hii leo sheria hii hajaitungia kanuni zake.

Mhe. Mwenyekiti ukiangalia hii sheria humu ndani mna vitu vinahitaji ufafanuzi mkubwa lazima iwepo kanuni ili viweze kutekelezeka, ama tutakuwa tuna sheria ambayo haitekelezeki. Mheshimiwa ukiangalia katika kifungu namba 79 cha ile sheria kwenye viwango vya kazi kuna mambo mengi hapa yameorodheshwa hasa kutoka kwenye mabano 3 pale kuanzia (a) mpaka (u) yanahitaji ufafanuzi wa kanuni. Sasa leo utaweza kumuhukumu vipi mfanyakazi kwamba kakawia kwenda kazini kama kanuni hazijaelekeza saa ngapi anatakiwa kuingia kazini na saa ngapi anatakiwa kutoka.

Kuna mambo mengi sana hapa Mheshimiwa, kuna sheria namba 78 kwenye kifungu cha sheria namba 78 kinaeleza kuwepo kwa afisi ya usalama wa

serikali. Mhe. Mwenyekiti ukiangalia hapa kwenye kifungu hicho kutakuwa kuna Afisi ya Usalama wa Serikali ambayo muundo, uongozi na uwajibikaji wa kazi zake zitaelezwa na Waziri katika kanuni. Sasa sheria hii itafanyaje kazi kama kanuni zile hazijawa tayari.

Sasa Mhe. Mwenyekiti hii nilikuwa naonesha msisitizo wangu wa kumtaka Waziri aje atupe maelezo ya uhakika ya kututosheleza kuonesha kwa nini mpaka hii leo hajaweza kutunga kanuni ili sheria hii iweze kufanya kazi yake sawasawa.

Mhe. Mwenyekiti nikisogea mbele kidogo hapo nije kwenye ukurasa wa 55 *paragraph* ya 124 Tume ya Utumishi Serikalini. Katika kitabu chake hapa Mhe. Waziri ameeleza kwamba Tume ina jukumu la kuajiri na kusimamia utaratibu wa ajira serikalini kupitia na kuthibitisha miundo ya utumishi serikalini. Mhe. Mwenyekiti sasa mimi hapa nina hoja kidogo, Tume hii ya Utumishi serikalini ni miongoni mwa zile Tume 4 ambazo zinaundwa. Kuna Tume ya Utumishi ya Baraza, Tume ya Utumishi ya Mahkama, Tume ya Utumishi ya Idara Maalum na Tume ya Utumishi Serikalini. Tume hizi zote zina mamlaka moja yaani nguvu zake ziko sawa kwenye sheria huku. Sasa kama Tume hii ilipewa jukumu kama alivyotwambia Mhe. Waziri hapa, jukumu la kuajiri kusimamia utaratibu wa ajira serikalini Tume ile ya serikali, kupitia na kuthibitisha miundo ya utumishi serikalini, sasa hii nahisi ni kazi ambayo inafanywa na Kamisheni.

Sasa nilikuwa nahitaji ufafanuzi hapo kwa sababu ukiangalia kazi za Kamisheni nazo alizieleza hapa Mhe. Waziri kupitia, kuidhinisha miundo ya utumishi, miundo ya taasisi na miundo ya mishahara kama itakavyopendekezwa na Tume za Utumishi. Lakini huku anatueleza kwamba Tume ya Utumishi Serikalini ina jukumu la kuajiri, kusimamia utaratibu wa ajira serikalini, kupitia na kuthibitisha miundo ya utumishi serikalini. Mimi nilikuwa ninamuomba Mhe. Waziri hebu atakapokuja hapa atupe ufafanuzi je, hii Kamisheni ndio basi haifanyi kazi zake au hii Kamisheni inafanya kazi kwa zile Tume Tatu tu? Ya mahkama, ya Baraza na ile ya Idara Maalum hii ya serikali inajitosheleza wenyewe? Maana kwenye kitabu chake ndio kaeleza sasa Mhe. Waziri nilikuwa nakuomba sana utakapokuja hebu utupe ufafanuzi katika hili. Maana yake kama hujatupatia ufafanuzi mzuri hapa tutapata shaka kidogo Mhe. Waziri.

Lakini Mhe. Mwenyekiti ukiangalia ile sheria ya kuweka miundo ya uendeshaji na usimamizi wa utumishi wa umma kule mwisho kule kwenye kifungu cha 105 ilieleza wazi kabisa kwamba nanukuu,

"Maamuzi ambayo yaliamuliwa na sheria zilizofutwa yatachukuliwa kuwa ni halali kama kwamba yamefanywa na sheria hii".

Sasa mimi nilikuwa hoja kidogo nimuulize Mhe. Waziri je ule muundo wa Baraza ulikuwa haupo? Je, wale wakuu wa Idara katika Baraza la Wawakilishi walikuwa hawapo? Na kama walikuwepo sasa kitu gani kinachosababisha kuwepo kwa mikwaruzo ya namna hii, maana sheria iko wazi kabisa inaeleza kwamba yale ambayo yalikuwepo kule au yalishaamuliwa basi yatakuwa yameamuliwa kama yaloamuliwa na sheria hii ambayo iliyotungwa hivi sasa. Sasa hivi vitu vilikuwepo, kulikuwa kuna muundo, kulikuwa kuna wakuu wa hizo Idara katika Baraza sasa tatizo linakuwaje tena leo inakuwa hivi.

Kwa hivyo nakuomba sana Mhe. Waziri utakapokuja hebu uje na maelezo yatakayonitosheleza ili niweze kuridhia na mimi nimkiuke Mnadhimu wangu kama itawezekana.

Mhe. Mwenyekiti sasa nisogee kwenye ukurasa wa 45 kwenye Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Mhe. Mwenyekiti bahati nzuri mimi ni Mjumbe wako wa Kamati ya *PAC*, kawaida Mhe. Mwenyekiti Kamati hii huwa inazipitia zile ripoti zinazowasilishwa na *CAG* hapa Barazani, huwa tunafuatilia yale ambayo yamejitokeza na kuweza kutolea maamuzi. Lakini cha kusikitisha Mhe. Mwenyekiti ripoti ya mwisho ambayo tuliifanyia kazi ni ya 2010/2011 hadi hii leo ripoti ya 2011/2012 haijawasilishwa Barazani na tukiuliza tunajaribu kumuuliza *CAG*, mwanzo alikuwa aa maana yake tunamaliza lakini anachosema hivi sasa ripoti iko tayari.

Kama yeye *CAG* ripoti iko tayari lakini utaratibu anatakiwa akaikabidhi kwa Mhe. Rais. Lakini nataka nikwambie Mhe. Mwenyekiti kikwazo kipo hapo *CAG* kutoka mguu wake mpaka pale Mnazi Mmoja vigingi alivyoekewa mpaka kufika kumuona Rais kumkabidhi ile ripoti ingawa katiba ndivyo inavyomtaka. Amenukuu vipengele hapa Mhe. Hamza sina haja kurejearejea hayo maneno. Lakini kuna wakubwa kwamba lazima wao waipate kabla haijapelekwa kwa Mhe. Rais, ingawa sheria Katiba kabisa ndivyo inavyomuelekeza *CAG* kwamba ripoti yake ataiwasilisha kwa Mhe. Rais kasoma Mhe. Hamza na Mhe. Rais ataiwasilisha Barazani kupitia kwa watu wake. Lakini kapewa mamlaka *CAG* kwamba ataiwasilisha kwa Mhe. Rais ndani ya siku 7 na kikao kama hivi kinaendelea Mhe. Rais hajaiwasilisha hapa basi yeye mwenyewe aje aiwasilishe kwa Mhe. Spika, au Naibu Spika. Lakini cha kushangaza ripoti ile mpaka leo sisi kama *PAC* ambao tunashughulika na ripoti ile haijawasilishwa hapa. Kwa hivyo nilikua namtaka Mhe. Waziri akija

atueleze kumekwama nini hasa ripoti ile mpaka leo haijawasilishwa na ripoti imeshakuwa tayari.

Mhe. Mwenyekiti nikiendelea mbele hapo nije kwenye maslahi ya wafanyakazi katika ofisi hii. Mhe. Mwenyekiti maslahi ya wafanyakazi katika ofisi hii bado ni madogo ukilinganisha na majukumu waliyopewa na serikali. Majukumu yao ni wakaguzi na kwenye kukagua haiwezekani Mhe. Mwenyekiti unakwenda kumkagua mtu anachezea mamilioni ya shilingi pale wewe unayekwenda kukagua pale unaenda na viatu vyako vya kanda mbili atakughilibu tu! Sasa nilikua nataka niombe sana Mhe. Mwenyekiti niiombe serikali katika hili hebu iwaangalie vizuri hawa watendaji wetu katika Ofisi hii.

Kwa kweli ni watu ambao wanatufanyia kazi moja nzuri sana. Kwa sababu mtu kwenda kukwambia huyu hapa amefanya dhambi moja, mbili, tatu. Huyu mtu ni muaminifu kama hukumtunza vizuri basi uhakikishe baada ya muda mchache sana anaweza kukutoroka. Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti mimi nilikuwa naiomba sana serikali katika hili iliangalie vizuri namna ya maslahi katika ofisi hii.

Mhe. Mwenyekiti mengi yamezungumzwa na wenzangu, sasa nikianza kuyarejea rejea yale yale nitakua naanza kukiuka kanuni. Mimi nitoe nafasi kwa michangio ya wenzangu wengine waliokuwa wameomba kuchangia ili waweze kuchangia wengi zaidi. Lakini Mhe. Mwenyekiti siiungi mkono hoja. Ahsante sana.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kunipa fursa hii kwa jioni hii na mimi nishukuru kwa hilo na kabla ya kuja kusahau nianze kuwaunga mkono wenzangu waliotangulia kwa kuundwa Kamati Teule kuhusu *E Government* na *payment* na Kamati ya *Pay Roll* ya Wizara zote nisije nikasahau.

Mhe. Mwenyekiti, mazito leo yamezungumzwa hakutumwa mtoto dukani.

Mhe. Mwenyekiti, nianze na Ofisi ya Wanasheria ya Ofisi ya *DPP*. Hawa ni watu muhimu katika jamii wanafanya kazi muhimu katika utumishi na asasi za kiraia. Aidha wanasheria wamekuwa na wanakuwa hadi sasa ni watetezi wakuu wa wanyonge kwenye vyombo vya sheria aidha pale wanapodai haki zao. Mimi nilidhani kuwa Serikali yetu ingewathamini, cha kushangaza Ofisi ya *DPP* mshahara ni shilingi laki nne, Hakimu wa Mahakama ya Mwanzo ni milioni moja laki tano *basic salary* vitu viwili tafauti mbingu na ardhi. Watu tunawahitaji na watetezi wa wanyonge, na si mara yangu ya mwanzo kupiga

kelele suala hili hii ni mara ya tatu au ya nne, Mhe. Waziri mwenyewe shahidi anajua hilo, atakapokuja hapa atanieleza ni sababu gani.

Mhe. Mwenyekiti, nikitoka hapo nije kwa watu walioniajiri na wakaniamini na wakanituma kuja kuwafanyia kazi hiyo wananchi wa Jimbo la Muyuni. Nitakuwa sijawafanyia haki na huko mbele ya safari pengine huenda nikaulizwa, hawa walipanga foleni wakati wa mvua na jua kutupigia kura sisi, ni dhamana nzito hii Mhe. Mwenyekiti. Wananchi hawa walikuwa na kilio cha Daktari wao, nimehangaika kwenda rudi mpaka viatu vyote vimelika kwa safari. Wananchi hawa walikaguliwa na Mhe. Rais wetu Dkt. Ali Mohammed Shein, katika ziara ya mabonde ya mpunga, wakaambiwa waeleze kilio chao na wakabahatika kulia wakalia daktari muda wake umekwisha. Lakini cha kusikitisha na cha kutia unyonge hawa tuseme sijui wamebaguliwa au hatakiwi, ikiwa agizo la Rais halifuatwi atafuatwa nani nchi hii.

Mhe. Mwenyekiti, ndugu yangu Haji Omar Kheri ananiambia kesho, kesho kutwa, kesho, kesho kutwa nasubiri jawabu, lakini labda atakapokuja hapa si kwa nia mbaya kabisa, haya tunazungumza mimi na wewe wananchi wangu wa Jimbo la Muyuni watakuwa hawanisikii, huu ndio ushahidi tosha labda utakapokuja hapa utaniambia kesho kutwa ataanza kazi muajiri huyo Dkt. Makame. Wananchi wanateseka kule kuna Muyuni A, Muyuni B, Muyuni C, Muyuni D, hospitali yenyewe ni moja. Alhaji Haji Omar Kheri hili fungu lifikirie ndio utapata fungu kwa Mwenyezi Mungu, hawa wananchi wetu ndio tunawahitaji.

La mwisho Mhe. Mwenyekiti, kuhusu kilio cha walimu wa sayansi. Mimi nafikiri hili suala tunalipigia kelele kwa muda mrefu na hivi sasa mimi nafikiri uchukue watu japo kwa mkataba, umeshafika wakati huo japo watu wetu wazima kina Maalim Saleh walimu wa sayansi hao. Vielelezo vyangu vilikuwa vitatu Mhe. Waziri, utakapokuja utaponieleza ndio nitapounga hoja mkono.

Mhe. Suleman Hemed Khamis: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana na mimi kwa kunipatia nafasi ya kuweza kutoa mchango wangu ingawa muda umebakia ni mfupi sana, labda unipatie na kesho niweze kuendelea tena.

Kwanza napenda nikushukuru kwa kunipatia nafasi lakini la pili pia napenda nimshukuru Waziri wa Nchi (OR) Utumishi wa Umma na Utawala Bora, kwa kazi nzuri ambayo aliyoifanya ya kitabu chake hichi ambacho kina maelezo mengi na mazuri.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya shukurani hizo niseme kwamba nizungumzie juu ya suala zima la watumishi. Kwa kweli Mhe. Waziri, amejitahidi sana katika

kufanikisha masuala yote ya kuwaendeleza watumishi wa sekta mbali mbali katika Wizara zetu, jambo la kumpongeza Waziri kwa jitihada zake na hakuacha kitu, kila mahala amejitahidi kuhakikisha kuwaendeleza wafanyakazi ili kuweza kupata mafunzo mbali mbali ya watumishi katika sekta zetu mbali mbali.
Hizo ni jitihada kubwa zake yeye na tunampa pongezi takriban Wizara zote zimeweza kufaidika.

Na katika mafunzo haya pia tunashukuru kwamba mafunzo yameandaliwa ya muda mfupi ya kati na mafunzo ya muda mrefu. Lakini katika haya vile vile yameweza kupatikana mafunzo ya nje vile vile na ni moja katika jambo zuri la kwamba wafanyakazi wetu wameweza kupelekwa nchi mbali mbali kwa mfano Korea, India, Ethiopia, Australia, Japan na Israel, watu wengi wameweza kupata mafunzo hayo.

Mhe. Mwenyekiti, mimi suala langu liko hapa moja tu nataka niulize. Katika mafunzo haya ambayo watu wamepelekwa katika nchi mbali mbali kuweza kupata taaluma ili kuweza kufanya shughuli zao kwa vizuri zaidi. Je wafanyakazi wa upande wa pili wa kisiwa ambacho ni Pemba je wameweza kupelekwa watu wakaweza kupata Mafunzo? Kwa sababu katika maelezo hatukuweza kuona kwamba mafunzo haya yameweza kubainishwa kwa Unguja na Pemba, kwa hivyo ilikuwa lazima tuweze kumuuliza Waziri katika mafunzo haya waliopelekwa watu nje, je imeweza kufanikisha vile vile kwa upande wa pili yaani kisiwa cha Pemba.

Mhe. Mwenyekiti, lakini suala la pili ambalo ninataka nilizungumze ni suala zima la ugawaji wa ajira katika Taasisi za Muungano. Mhe. Mwenyekiti, kabla sijazungumzia ugawaji wa ajira katika Taasisi za Muungano, nilikuwa na wazo kwanza kutaka kumueleza Mhe. Waziri, kwamba kuna kilio cha Wazanzibari wengi waliomo ndani katika suala la ajira. Ni suala mpaka hivi sasa lenye utata, utaratibu wake haujaeleweka vizuri kwa wanajamii wengi, kwa vijana wetu wengi ambao waliomaliza masomo yao nchini. Kwa hivyo Mhe. Waziri, malalamiko yamekuwa mengi kwa vijana wetu ambao wamemaliza mafunzo yao ya elimu na wengi wamekaa hawana ajira na hapo zinapopatikana hizo ajira zina utata hazieleweki. Kwa hivyo ningemuomba Mhe. Waziri kwenye suala la ajira, suala la ajira angeliweka wazi, likawekwa bayana ni ajira gani ambayo kwa mwaka huu zinapatikana ili kila mtu akapeleka *application* yake akaweza kuomba aina ya ajira hizo.

Vile vile Mhe. Mwenyekiti, pakaweza kuwa na utaratibu wa kuweka *data* ili kuwatambua wale ambao tayari wameshapata ajira na wangapi hawajapata ajira. Kwa sababu katika nchi hii mpaka sasa hivi hatuwezi kuelewa vijana wangapi hawajapata ajira, sasa ningemuomba Mhe. Waziri kama atakuwa na

nafasi wakati wa majumuisho aweze kutusaidia kuweza kupata taarifa ni vijana wangapi hawajaweza kupata ajira, haya ni masuala ya ndani ambayo hayo ni malalamiko makubwa vijana wetu wengi hawana kazi.

Mhe. Mwenyekiti, suala jengine ambalo ugawaji wa ajira katika Taasisi za Muungano ni suala zito sana kwa Zanzibar, lakini sasa tunaambiwa kuwa suala la ajira kuna makubaliano ya mgao wa ajira baina ya nchi ya Zanzibar na nchi ya Bara. Sasa tunaambiwa kwamba Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora inashirikiana na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma ya Serikali ya Muungano wa Tanzania. Na tunaelezwa vile vile kwamba sekretarieti iko tayari imepatiwa ofisi katika jengo la Makamo wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania liliopo Tunguu. Sasa Mhe. Waziri, Ofisi ya Rais ya Utumishi wa Umma imeshatoa toleo kwa Taasisi za Muungano kuhusu utekelezaji wa makubaliano hayo ya mgao wa ajira.

Sasa Mhe. Waziri, suala linakuja ni mara ngapi makubaliano ya ajira katika Taasisi za Muungano yamewahi kufanyika, na kama mazungumzo yaliwahi kufanyika je, imekuwaje wakati huo wa makubaliano, kwa sababu hili tunaliona leo, je kwa miaka yote hiyo iliyopita hakukuwa na makubaliano ya aina hii katika suala zima la ajira baina yetu sisi na wao.

Mhe. Mwenyekiti, pia Mhe. Waziri, leo tuko mwaka 2013 unadhani suala hili la ajira katika Taasisi za Muungano linaweza kufanikiwa kwa muda mfupi ili na sisi tuweze kufaidika katika ajira hizo? Naomba Mhe. Waziri atakapokuja hapa katika majumuisho yake aweze kutupatia maelezo maalum.

Mhe. Mwenyekiti, Mhe. Waziri,

(Saa 1.45 usiku Baraza liliakhirishwa hadi tarehe 03/07/2013, Saa 3.00 asubuhi)